# Nipashe

Jumanne Machi 3, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580169

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



## Tanzania yajivunia mambo manne SADC

UKURASA 3




UKURASA 13

# CCM yamfungulia milango Membe



• **Mwenyewe** aeleza kushangazwa akiwa ughaibuni kwamba...*Endelea ukurasa 2*


## YALIYOMO

UKURASA WA 7

**KIGOGO TAKUKURU AMWANDIKIA UPYA DPP KUKIRI UTAKATISHAJI**

MKURUGENZI wa zamani wa Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini wa Taasisi ya...

UKURASA WA 8

**ACT-WAZALENDO KUJADILI TUME HURU MKUTANO MKUU**

CHAMA cha ACT-Wazalendo, kimeeleza mambo manne yatakayojadiliwa...


## Wafungwa wapelekwa shamba la michikichi

UKURASA 3



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Mhandisi Hamad Masauni (wapili kulia), na Mkuu wa Gereza la Kwitanga, Mrakibu Mwandamizi, Dominick Kazmil, wakiangalia matunda ya mchikichi, yaliyovunwa katika gereza hilo, wilayani Kigoma jana, ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa la kutaka gereza hilo kuwa kituo kikuu cha uzalishaji wa zao hilo nchini. **PICHA: WMNN**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store




## Mzee Mwinyi ataja dawa ya rushwa

UKURASA 2

**MICHEZO** SABABU AZAM FC KUMTIMUA CHECHE UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Mwinyi ataja dawa ya rushwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

RAIS mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, amesema Tanzania bado ina deni la kupambana na rushwa, akiamini mkakati uliozinduliwa jana utakomesha vitendo hivyo.

Akizungumza kwenye uzinduzi wa mkakati wa kupambana na rushwa kwa kuwatumia vijana wa Skauti nchini jijini hapa jana, Rais Mwinyi alisema Tanzania ina aina nyingi za rushwa, hivyo ni vyema jamii ikaona namna ya kumsaidia Rais John Magufuli kupambana nazo.

Mkakati huo unatarajiwa kuwafikia wanafunzi milioni 16 wa kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu.

"Kuna aina nyingi za rushwa wizi, ufisadi, hongo na nyingine nyingi, hivyo ni vyema kupambana nazo," alisema.

Mwinyi alisema mkakati huo unapaswa kuwa chachu ya kila mmoja kuhakikisha unatumika kwenye mapambano hayo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na utawala bora, Kapteni mstaafu George Mkuchika, akizindua kwa niaba ya Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, aliwataka vijana kuwa mabalozi katika mapambano hayo.

Mkuchika alisema rushwa ni ugonjwa unaoitafuna jamii na kusababisha baadhi yao kupoteza haki zao za msingi na wakati mwingine kusababisha mauaji.

"Ili tuwe na jamii yenye maadili, ni jukumu la kila Mtanzania kufichua wapokeaji wa rushwa na wale wanaoomba rushwa kwani mapambano dhidi ya rushwa ni jukumu letu sote, hivyo ni lazima kila mtu ashiriki katika vita hii," alisema.

Alisema rushwa ni ugonjwa unaofifisha maendeleo kwa uchumi wa taifa na hivyo serikali haina budi kuchukua hatua kwa kushirikisha makundi ya vijana.

"Mkakati huu unalenga kuwafikia wanafunzi zaidi ya milioni 16 wa shule za msingi hadi vyuo Vikuu, watapatiwa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa na kupitia wao, tutawafikia Watanzania zaidi ya milioni 40," alisema.

Kiongozi Mkuu wa Skauti, Mwantumu Mahiza, alisema mkakati huo utawafikia wanafunzi hao milioni 16 ndani ya mwaka mmoja, akisisitiza kuwa rushwa lazima ikemewe ili kizazi kijacho kisiathirike.




Aliyekuwa Katibu Mwenezi wa Baraza la Vijana la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAVICHA), Edward Simbeye, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akitangaza kujiunga na chama cha NCCR-Mageuzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# CCM yamfungulia milango Membe

**Na Romana Mallya**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, amesema anasubiri kutia saini barua ya kuomba radhi kutoka kwa Bernard Membe, ambaye chama hicho kilitangaza kumfuta uanachama Ijumaa iliyopita.

Dk. Bashiru aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam na kubainisha kuwa tangu ateuliwe kushika wadhifa huo, amesha tia saini barua 14 za wanachama waliofukuzwa na kuomba radhi, hivyo anasubiri ya 15 kutoka kwa Membe.

"Namtakia maisha marefu, matarajio yangu atarudi CCM, nikiwa hai ama nimekufa kwa sababu milango ya kuwapokea wanachama wapya iko wazi na milango ya wanachama kuondoka kwa hiari iko wazi, milango kwa wanachama waliofukuzwa na kuomba radhi iko wazi.

"Nimeshasaini barua za wanachama waliofukuzwa na kuomba radhi 14, ninasubiri ya 15 ya Membe. Kama akitaka, nitaisaini tu.

"Nimempokea (Edward) Lowassa (Waziri Mkuu mstaafu), (Frederick) Sumaye (Waziri Mkuu mstaafu), Dk. (Wilbroad) Slaa (aliyekuwa Katibu Mkuum wa Chadema), siku moja ninaweza kuja kumpokea hata Membe, nikianza kubwabwaja hapa, ni kama sina picha pana," alifafanua.

**KAULI YA MEMBE**

Kutokana na kauli hiyo ya Dk. Bashiru, Nipashe ilimtafuta Membe kuzungumzia suala hilo na alijibu kwa kifupi akisema: "Ndiyo unaniambia! Mimi nipo nje (ya nchi) nauguza mwanangu. Sijasoma mitandao inasema nini. Kwa leo (jana) na kesho (leo) siwezi kusema chochote mpaka kijana wangu atoke hospitali."

Katika mahojiano hayo, Dk. Bashiru aliwaambia wanaCCM kuwa kumpoteza mwanachama ni msiba, hivyo huu si wakati wa kuzomea au kufurahia.

"Membe alishawahi kupewa adhabu ya onyo kali, ni hatua ya kumpa nafasi ya kujirekebisha, inapofika hatua ya kumfukuza mwanachama, ni ngumu, hatuwezi kusherehekea, nisingependa wanaCCM kujiingiza kwa kusherehekea adhabu mbaya aliyopewa mwanachama.

"Tunafanya sherehe kupokea na ninapanga kufanya sherehe kubwa ya kumpokea Sumaye maana atapata kadi mpya Dodoma. Tukimpokea mwanachama, ni sherehe, tukifukuza ni msiba, tusherehekee kwamba ni jambo zuri, lilipangwa? Hapana! Tunataka kuongeza idadi ya wanachama kadri inavyowezekana," alionya.

Dk. Bashiru alisema uamuzi uliochukuliwa na chama chake dhidi ya Membe na makatibu wakuu wastaafu, Yusuph Makamba na Abdulrahman Kinana, ni mapendekezo yaliyotolewa na kamati ya nidhamu iliyowahoji na yametangazwa hadharani kwa mujibu wa kanuni na yalithibitishwa na Halmashauri Kuu.

"Ninamwona Membe amesahau kabisa, nadhani tumpe muda kwa sababu ni binadamu na ana haki yake, asitapetape, anahitaji ushauri nasaha kwa sababu hili siyo jambo dogo.

"Sikutaka kulizungumza kwa ushabiki kwa sababu lingenipata mie ningehitaji marafiki zangu wa karibu niwashirikishe. Kama nina busara ya kutosha, ningepata nasaha kutoka kwa mke wangu na jamaa zangu, kwa marafiki zangu wa kiasiasa washauri namna ya kulimudu.

"Vyombo vya habari sina uhakika kwa sababu hajazungumza, yeye ni tweets na kama mnavyojua, sidhani kama ni hitimisho kwa sababu hajawa wa kwanza wala wa mwisho kufukuzwa au hata kuondoka.

"Yamesemwa mengi, wanaoondoka husemwa mengi na wanaofukuzwa husema mengi pia wengine huamua kunyamaza," alisema.

Bashiru alisema mchakato huo wa kuwafukuza uanachama wanachama wa CCM ni kama wa kimahakama na una nafasi ya rufani kwa wasioridhika na uamuzi.

"Nikianza kusema wakati mimi ndiye napokea rufani, ni kama ninatoa hukumu mchakato wa haki, watasema umemsikia huyo Katibu Mkuu maana katika majibu niliyosema, Membe anasema wabaya wake ni Katibu Mkuu na Mwenyekiti.

"Sisi ni wawili, lakini kikao kinachofanya uamuzi ni cha watu 24, ana haki ya kusema watu wawili kwa sababu Mwenyekiti na Katibu ndiyo wanaandaa ajenda na kuzisimamia," alisema.

Alisema Halmashauri Kuu ambayo ndiyo inahitimisha adhabu, ina wajumbe 170 na ndiyo iliwatuma kufanya kuwahoji watuhumiwa Desemba 13 mwaka jana.

# Serikali yakiri kudaiwa bil. 6/- malipo korosho

**Na Said Hamdani,** LINDI

SERIKALI mkoani Lindi, imekiri kudaiwa na wakulima Sh. 6,930,549,278 zikiwa ni malipo ya mauzo ya korosho, msimu uliopita 2018/2019 na kuwa ucheleweshaji huo umechangiwa na uhakiki. Kauli hiyo imetolewa na Mkuu wa Mkoa huo, Godfrey Zambi, wakati wa kikao cha Kamati ya Ushauri (RCC) kilichofanyika mjini hapa.

Zambi alisema hayo kufuatia wajumbe kutaka wapewe maelezo kinachokwamisha wakulima wa korosho mkoani humo kutolipwa fedha zinazotokana na uuzaji korosho kwa msimu wa mwaka 2018/2019.

Akijibu hoja za wajumbe hao, alisema katika madai hayo, wapo wakulima waliokwisha lipwa sehemu ya fedha zao na wengine bado hawajalipwa huku akitaja sababu kubwa kuwa ni utaratibu wa uhakiki.

Aliwaambia wajumbe wa kikao hicho kwamba wakulima wa korosho ambao bado hawajalipwa wanadai Sh. 4,869,550,801 huku waliopunguziwa kulipwa wanadai Sh. 1,224,493,477.

Akitaja viwango kwa kila halmashauri, alisema Liwale ndiyo inayoongoza wakulima wake kudai Sh. 1,771,544,094 ikifuatia Nachingwea, Sh. 1,605,348,226, Ruangwa Sh. 1,398,682,428, Lindi Vijijini Sh. 669, 973,916, Kilwa Sh. 599,544,924 wakati Manispaa ya Lindi, wakidai Sh. 48,453,690.

Alisema ucheleweshwaji huo, umechangiwa na mambo mbalimbali, yakiwamo uhakiki ili kuwafahamu wahusika halisi wanaostahili kulipwa fedha hizo, huku akisisitiza serikali kutambua deni la wakulima hao na litalipwa fedha zitakapopatikana.

"Tunajua wamechelewa kulipwa, lakini tunawaomba wavumilie na pale fedha itakapopatikana watalipwa," Zambi alisisitiza.

Awali, wakichangia hoja katika kikao hicho, wabunge Hamidu Bobari (Mchinga), Mohamedi Kuchauka (Liwale) na Selemani Said Bungara (Bwege) (Kilwa kusini), walihoji sababu za wakulima wa korosho kuchelewa kulipwa fedha zao zinazotokana na uuzaji wa zao hilo, msimu wa mwaka 2018/2019.

HABARI KITAIFA

# Tanzania yajivunia mambo manne Sadc

**Na Gwamaka Alipipi**

TANZANIA imetaja mafanikio manne yaliyopatikana katika kipindi cha miezi sita tangu ilipokabidhiwa uenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (Sadc), mojawapo ni upatikanaji wa ajira.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akielezea ujio wa Mkutano wa Baraza la Mawaziri la Sadc utakaofanyika kuanzia Machi 16 hadi 17, mwaka huu.

Rais John Magufuli alikabidhiwa uenyekiti wa Sadc wakati wa Mkutano wa 39 wa wakuu wa jumuiya hiyo uliofanyika Agosti mwaka jana jijini Dar es Salaam, baada ya Rais wa Namibia, Hage Geingob, kumaliza muda wake.

Prof. Kabudi alisema tangu wakati huo mafanikio manne makubwa yamepatikana ambayo ni Kiswahili kuwa lugha ya mawasiliano, Umoja wa Ulaya (EU) kufanya mazungumzo na Zimbabwe kuhusu kuondoa vikwazo, upatikaji wa ajira, mwingiliano wa biashara kwa nchi wanachama.

"Kwa sasa Tanzania inafanya biashara sana na nchi za Sadc, ufanyaji wa biashara za anga nazo zimeongezeka, baadhi ya nchi za Sadc kama vile Comoro zimeanza kuleta wagonjwa hapa kwetu," alisema Prof. Kabudi. Kuhusu Mkutano wa Baraza la Mawaziri, Prof. Kabudi alisema Mawaziri wa Mambo ya Nje, Fedha na Mipango, Viwanda na Biashara kutoka nchi 16 zinazounda Sadc watakutaka kwa siku mbili kujadiliana ajenda mbalimbali.

"Ajenda watakazojadiliana ni mambo ya fedha, utekelezaji wa kauli mbiu ya Sadc, utekelezaji wa mkakati wa viwanda, kupokea mapendekezo ya vikao vya maofisa yaliyopendekezwa, kupitia taarifa mbalimbali na kupeleka taarifa katika mkutano mkuu wa wakuu wa nchi,' alisema Prof. Kabudi.

Kuhusu ajenda ya fedha, Prof. Kabudi alisema mawaziri hao watajadiliana kuhusu michango ya nchi jumuiya wanachama ambao hawajalipa ada, kupitia bajeti, kupitisha matumizi ya dharura.

"Kwa mfano, kuna fedha zilitolewa kuisaidia Madagascar ilipokumbwa na mafuriko, hivyo fedha hizo zitaingizwa kwenye taarifa rasmi wakati wa kikao hicho," alisema Prof. Kabudi.

Wakati huo huo, Mkurugenzi wa Kazi na Ukuzaji Ujuzi wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu), Ali Msaki, alisema Makatibu Wakuu na maofisa waandamizi wa sekta za ajira na kazi wa Sadc wameanza vikao jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kupitia ajenda zitakazojadiliwa katika Mkutano wa Mawaziri wa sekta hiyo utakoanza Machi 2 hadi 6, mwaka huu.

Alisema ajenda hizo ni ukuzaji wa fursa, ujuzi, ajira kwa vijana, pamoja na uhamishaji nguvu kazi kwa nchi za Sadc.

Alisema ukosefu wa ajira ni changamoto kubwa, na kwamba watu milioni 200 sawa na asilimia 5.1 hawana kazi duniani, kwa nchi za Sadc ukosefu wa ajira ni asilimia 11, Tanzania ikiwa ni asilimia 9.7.

# Wafungwa sasa wapelekwa kulima shamba la michikichi

**Na Mwandishi wetu,** KIGOMA

WAFUNGWA 150 kutoka katika mikoa ya Mwanza, Shinyanga na Tabora, wamepelekwa Gereza la Kwitanga mkoani Kigoma, kwa ajili ya kuanza uzalishaji wa zao la mafuta ya michikichi nchini. Hatua hiyo imechukuliwa ukiwa mkakati wa kulifanya gereza hilo kuwa kituo kikuu cha uzalishaji wa michikichi.

Hayo yalielezwa jana na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya mkakati huo.

Mkakati huo ni utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, mwaka 2018 alipofanya ziara gerezani hapo kwa lengo la kulifanya Jeshi la Magereza kuingia katika mfumo wa uzalishaji mali. "Katika kutekeleza agizo hilo la serikali, wizara tumeongeza nguvu kazi hapa kwa kuleta wafungwa 150 na muda si mrefu tutaongeza wengine 300 kutoka magereza mbalimbali nchini ili kuongeza uzalishaji huku eneo lenye ukubwa wa ekari 6,000 linatarajiwa kulimwa zao hilo," alisema na kuongeza: "Kusambaza mbegu zinazozalishwa gerezani hapo kwenda Halmashauri za mikoa, taasisi za umma, asasi za Kiraia na Sekta Binafsi."

"Lakini pia ili kuliwezesha gereza hili tumeliagiza Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Magereza kulichukua gereza la Kwitanga na kuliingiza katika kundi la magereza yanayowezeshwa na shirika ili kutatua matatizo yao ya kifedha badala ya kusubiri bajeti kuu kutoka serikalini ambayo inakua haitoshi," alibainisha. Naye, Mkuu wa Magereza mkoani Kigoma, Kamishna Msaidizi Leonard Bushiri, aliunga mkono hoja ya gereza Kwitanga kuchukuliwa na shirika la uzalishaji mali, huku akikiri baadhi ya masuala kukwama kutokana na changamoto za kibajeti.

"Nafikiri suala la gereza kuchukuliwa na shirika litatatua mambo mengi ya kibajeti na kiuendeshaji maana gereza halina gari kubwa kwa ajili ya uvunaji na usafirishaji wa mafuta kutoka gerezani kwenda kwa mtumiaji,"alisema na uongeza:

"Hakuna bajeti ya uendeshaji kwa mfano kukamua lita 100 mpaka 120 za mafuta tunahitaji maji lita 1000 hivyo fedha kwa ajili ya kununulia umeme ili kusukuma maji ni changamoto, kwahiyo kuingizwa kwenye shirika itasaidia mambo mengi."

Aidha, gereza la Kwitanga lina shamba la mchikichi, mahindi, mpunga, mihogo, maharage na bustani za mboga.




TOLEO MAALUMU

# O&OD ILIYOBORESHWA

## Tanzania inaweza kuendelea kwa kasi na kujenga Taifa la kuigwa katika Karne ya 21 kupitia

### "Jitihada za Jamii"na "Mashirikiano kati ya Serikali na Wananchi"

***Makala hii inawajulisha Watanzania kuhusu moja ya shughuli muhimu za zinazofanywa kwa ushirikiano kati ya mataifa mawili ya Tanzania na Japani kupitia Shirika la Maendeleo JICA, inayojulikana kama O&OD Iliyoboreshwa.***

**O&OD Iliyoboreshwa ni nini?**

Kwa Zaidi ya miaka 10, JICA, (Shirika la misaada ya maendeleo) imeshirikiana kwa karibu sana na Serikali ya Tanzania, kujaribu kuandaa mtindo imara na endelevu wa maendeleo ya jamii na utoaji wa huduma kupitia Utawala wa Serikali za Mitaa bunifu na "Ushirikiano kati ya Serikali na Wananchi". Njia hii inaitwa O&OD Iliyoboreshwa.

O&OD ni kifupisho cha "Opportunities and Obstacles to Development" kwa lugh ya kiingereza yaani "Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo" na dhana hii ilianzishwa na Serikali ya Tanzania mwaka 2001 kukuza upangaji shiriki wa mipango ya maendeleo katika jamii.

Tangu mwaka 2009, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) na JICA wamekuwa wakitekeleza mradi wa ushirikiano kuboresha mfumo wa "O&OD" ili kuhuisha kwa ufanisi zaidi "Jitihada za Jamii" pamoja na kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali za Mitaa na Jamii. Dhana hii ya "O&OD Iliyoboreshwa" ipo katika msingi na urithi mkubwa wa kipekee wa nchi kutoka kwa Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

**Faida ya Kipekee Duniani kwa Tanzania**

JICA ilitambua kwa shukrani kubwa kuwa katika Tanzania, kuna jamii nyingi ambazo watu wanajipanga na kufanya maamuzi ya kuboresha maisha yao na kuendeleza jamii bila kusubiri Serikali iwafanyie. Taasisi nyingi mfano shule za msingi, zahanati, barabara za Vitongoji, skimu za umwagiliaji, miradi ya maji n.k. zimejengwa kwa nguvu ya wananchi.

Aidha, tumejifunza kwamba huu ni urithi kutoka kwa Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere aliyeamini kwamba: "Maendeleo ni ushiriki wa wananchi katika kujifunza kwa pamoja kupitia uzoefu walionao, wakitumia nguvu zao, rasilimali asilia zilizopo, mawakala wa mabadiliko na rasilimali kutoka nje. Watu hawawezi kuendelezwa bali wanajiendeleza wenyewe kwa kushiriki katika shughuli zinazochangia maendeleo. Watu hawaendelezwi kwa kuwaburuza kwenye miradi mipya kama wanyama."

Hata hivyo, inasikitisha kuona siku hizi watu wengi wameacha utaratibu huu bora wa shughuli za maendeleo.

"O&OD Iliyoboreshwa" inalenga kukumbuka na kuhuisha utamaduni huu mzuri wa Taifa uliofifia.



*Mwezeshaji wa kata (kushoto) akaimsaidia mwakailishi wa kundi la kitongoji (kulia) wakati wa shughuli ya umwagiliaji (kata ya Mughunga, Wilayani Singida)*

**Taifa la Japani limepata Maendeleo kupitia njia sawa kama ya Tanzania**

Utamaduni huu muhimu wa Tanzania unatukumbusha uzoefu wetu wenyewe wa maendeleo katika nchi ya Japani.

Mwanzoni, katika kujenga nchi na maendeleo yake mwishoni mwa Karne ya 19 na mwanzoni mwa Karne ya 20, Serikali ya Japani ilikuwa maskini sana na rasilimali chache za nchi zilielekezwa kwenye Mpango Mkakati wa Maendeleo hasa viwanda na majeshi kuepuka kutawaliwa na zilizokuwa Dola zenye nguvu za Ulaya.

Kwa kuwa Serikali haikuwa na uwezo wa kutosha kushughulikia mahitaji ya watu, kila jamii ilijaribu kukabiliana na umaskini na kuboresha maisha kupitia "Jitihada za Jamii", viongozi na ushirikiano baina yao. Serikali za Mitaa zilitimiza jukumu muhimu la kuongoza jitihada za jamii, kuwatia moyo na kuwasaidia. Serikali Kuu pia ilijaribu kuhakikisha mazingira wezeshi kwa Serikali za Mitaa kutekeleza jukumu hili.

Kama ilivyoonekana hapo juu, maendeleo ya Japani hayakufikiwa kwa jitihada za Serikali pekee, bali kimsingi ni kila mwanachi, jamii na makundi (kampuni ndogondogo) waliofanya jitihada za kujiletea maendeleo. Serikali ilishukuru, ikasaidiana nao, kuwatia moyo na kukuza jitihada hizo.

**Serikali haiwezi kufanya kila kitu peke yake**

Kama ilivyokuwa kwa Serikali ya Japani wakati huo, Serikali ya Tanzania inakumbana na changamoto zilizo sawa za uhaba wa rasilimali kwa suala la bajeti na upungufu wa watumishi katika kutekeleza majukumu mbalimbali na makubwa. Haiwezekani Serikali kufanya kila kitu peke yake.

Kutokana na msingi wa uchambuzi huo, OR-TAMISEMI na JICA walitambua wazi kuwa njia sahihi na ya ufanisi ya kuleta maendeleo katika nchi hii ni kutumia kikamilifu faida ya utamaduni mzuri uliopo wa "Jitihada za Jamii" ili kuongezea nguvu za Serikali kuelekea maendeleo ya kijamii na kitaifa na kuboresha maisha ya watu.



*Wanakijiji wa Kijiji cha Mang'ula B wakitengeneza barabara ya Kijiji mwaka 2015*

# TOLEO MAALUMU

Kwa sababu hiyo, Mradi wa "O&OD Iliyoboreshwa ulitambua kuwa msingi mkuu ni kujenga uwezo sahihi wa Watumishi wa Ugani katika Kata (Kilimo, Maendeleo ya Jamii, Elimu, Afya, Mifugo n.k.) ambao wapo mstari wa mbele katika kuongoza jamii na kushirikiana nao. Wanatarajiwa kuwa daraja kati ya jamii na Serikali.

### Kutoa Mafunzo kwa Watumishi wa Ugani wa Kata namna ya kuiwezesha jamii

Mradi ulianzisha mfumo bunifu wa kutoa mafunzo kwa watumishi wa ugani kwa njia ya vitendo. Njia hii iliwajengea uwezo na mbinu za kuiwezesha jamii katika kutambua na kuthibitisha mahitaji yao ya msingi, kujipanga na kutekeleza shughuli mbalimbali kila inapowezekana badala ya kungoja Serikali iwafanyie. Watumishi wa ugani waliopatiwa mafunzo haya wanaitwa "Wawezeshaji wa Kata"(WFs). Baada ya kupatiwa mafunzo, Wawezeshaji wa Kata hutembelea Vitongoji mara kwa mara. Baada ya kuwezeshwa na Wawezeshaji wa Kata, jamii huanza kutekeleza miradi ya vipaumbele kulingana na uwezo walionao.

Ifuatayo ni mifano kadhaa ya mambo ambayo yamekuwa yakifanyika katika vijiji husika (tunasikitika kuwa tutaonyesha mifano miwili tu kati ya mingi iliyopo)

### Vijiji vinabadilika kwa kasi kupitia O&OD Iliyoboreshwa

### Kijiji cha Maseyu - Shule za Awali katika Kitongoji vyote vitano na ukamilishaji wa ujenzi wa Zahanati.

Ukisafiri kutoka Morogoro kuelekea Dar es Salaam kwa muda wa dakika 30 utaona Kijiji cha Maseyu kandokando ya barabara kuu. Hofu ya muda mrefu ya wanakijiji ilikuwa kuwapeleka watoto katika darasa la awali lililopo umbali mrefu kuvuka barabara kuu yenye hatari nyingi. Baada ya ajali mbaya ya mvulana mmoja kuuawa na nyoka akiwa anarudi nyumbani kutokea shuleni, wananchi walisimama na kuamua kujenga darasa la awali katika kila Kitongoji. Wawezeshaji wa Kata walitekeleza jukumu kubwa la kuwezesha jamii kukubaliana na kuamua kujipanga kufikia ndoto yao. Baada ya miaka miwili, Vitongoji vyote vitano vilikamilisha ujenzi wa Shule za Awali jambo liliopunguza muda wa watoto kutembea kwenda shuleni, hatari ya kupata ajali na pia kuongeza uandikishaji kwa kasi. Haikuwa ujenzi wa madarasa ya awali tu, lakini pia wanakijiji walitafuta mtu mwenye uwezo wa kufundisha watoto katika Kitongoji na kumlipa mshahara.

Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro ilitambua jitihada kubwa ya watu wa Maseyu kwa upendeleo mkubwa. Shule za Awali zote zimesajiliwa na Serikali kisheria na Halmashauri imepanga waalimu katika shule hizo kwa sasa.

Kutokana na uzoefu walioupata katika ujenzi na ukamilishaji wa Shule za Awali, wanakijiji walishawishika kukamilisha Zahanati ya Kijiji iliyokuwa imetelekezwa kwa miaka kadhaa. Kazi hii imewachukua karibu miaka 7 lakini waliendelea bila kukata tamaa, wakiendeleza kidogo kidogo, hatua kwa hatua na hatimaye wamekamilisha hivi karibuni. Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro ilisaidia vifaa vya kuezeka na kupanga watumishi. Zahanati ilianza kutoa huduma rasmi mwezi July 2018.

Wananchi wana Imani kubwa kwa Wawezeshaji wa Kata na Halmashauri ya Wilaya na wanajivuna kwa kusema kuwa Kijiji chao ni BORA katika Tanzania. Zaidi ya hayo, Afisa Mtendaji wa Kijiji aligombea na kushinda katika Uchaguzi Mkuu mwaka 2015 na kwa sasa ni Diwani anayeongoza maendeleo ya Kata yake.

### Mang'ula B na Mshikamano: Mabadiliko chanya ya mtazamo wa Wanakijiji

Kijiji cha Mang'ula B kipo katika Wilaya ya Kilombero kandokando ya barabara kuu ya kutoka Mikumi kwenda Ifakara. Kijiji kikiwa mkabala na lango kuu la kuingia Hifadhi ya Udzungwa, kinafikiriwa kuwa mazingira ya mji unaokua kwa kasi kikiwa na mwingiliano na uhamiaji wa watu. Kutokana na hali hii, Wawezeshaji wa Kata walipata changamoto kubwa kuhamasisha "Jitihada za Jamii".

"Hatukuwahi kuiamini Serikali na watumishi wake hapo awali". Mwanamke mmoja wa Kijiji hiki alituambia na kuendele; Walitutembelea mara chache sana na walipofika walitulazimisha kufanya mambo tusiyoyakubali. Lakini hawa Wawezeshaji wa Kata ni tofauti. Tunawaona kila siku wakituongoza katika shughuli zetu, wanatusikiliza na kwa sasa ni sehemu ya jamii. Tunawachukulia kama sehemu ya familia yetu. (Hali kama hii inaonekana kwenye picha) Sikutoa ardhi yangu kipindi ambacho TASAF walikuja kutengeneza barabara. Lakini kipindi hiki nimetoa ardhi yangu kwa sababu tuliamua wenyewe kutengeneza hii barabara pamoja na Wawezeshaji wa Kata."

Kijiji cha Mang'ula B kwa sasa ni Kijiji bora katika mradi. Wanakijiji wana umoja. Wanawaamini Wawezeshaji wa Kata na Viongozi wa Kijiji. Mwenyekiti wa Kijiji Bw. Hamisi alichaguliwa kwa sababu alikuwa kiongozi mahiri wa kikundi katika shughuli za maendeleo.

Wananchi walifanya ujenzi wa barabara yenye urefu kilometa 14 katika Kijiji na kujenga madaraja ya kuwezesha watoto kuvuka wakati wa kwenda shuleni (angalia picha), wametundika mizinga ya kisasa kandokando ya hifadhi kuzuia Tembo kuingia katika mashamba na kuharibu mazao. Wananchi waliamua kujenga jengo la biashara lenye vyumba vya kupangisha ili kuwa na mapato ya ziada yatakayokuwezesha kugharimia miradi mingine zaidi.

"Sikuwahi kuhudhuria Mkutano Mkuu wa Kijiji". Mmoja wa viongozi wa kikundi cha wanawake alituambia; "Sikufikiri kuwa Mkutano huu ni kwa ajili yetu. Mkutano ulikuwa wa viongozi. Lakini kwa sasa nahudhuria kwa sababu katika kufanya shughuli za kikundi, niliona kuwa nahitaji kushiriki katika kufanya maamuzi ya masuala yanayotuhusu hapa kijijini." Kwa sasa anahudhuria mikutano siyo kwa sababu "anatakiwa kuhudhuria" ila kwa sababu "anataka kuhudhuria."

### Tunayo NDOTO

Ndoto ya kweli tuliyonayo ni kuwa Tanzania itakuwa na vijiji vizuri kama hivi nchi nzima vyenye nguvu na umiliki wa maendeleo yao katika misingi imara ya uzalendo, kujivunia na kuipenda jamii yao. Tunaamini kuwa inawezekana

kabisa katika nchi hii, kuendeleza mahusiano na ushirikiano wa karibu kati ya jamii na Serikali za Mitaa, pamoja na usaidizi imara kutoka Serikali Kuu ili kuhakikisha mazingira wezeshi ya ushirikiano huu.

Kwa kufanya hivyo, Serikali itaweza kutoa huduma bora kwa wananchi kwa gharama ndogo, huku ikielekeza nguvu na rasilimali chache zilizopo kwenye miradi mikubwa ya Kitaifa ya Maendeleo kama Japani ilivyoendeleza uchumi na ustawi wa watu wake.

***[O&OD iliyoboreshwa imeidhinishwa na Serikali Octoba 2019 kama sehemu ya mfumo wa kitaifa wa Upangaji Mipango na Utekelezaji. Mfumo huu utaenezwa kwa Sekretarieti za Mikoa yote 26 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 Tanzania Bara kupitia Warsha za kanda kuanzia Januari 2020.]***



*Wanakijiji wa Kijiji cha Mshikamano walianza kutengeneza daraja la Kijiji mwaka 2016, kwa sasa daraja hilo wanalitumia kwa shughuli za kiuchumi na ni kiungo muhimu cha elimu cha vijiji jirani*



*Ujenzi wa daraja ukiendelea Kijiji cha Mshikamano*

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Sheria mpya izibane taasisi hizi za fedha

**MKUU** wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, ametangaza kupiga marufuku taasisi ndogo za kifedha ambazo huwakopesha watumishi wa umma wakiwamo walimu, kuacha utaratibu wa kushikilia kadi zao za benki kama dhamana wanapowakopesha.

Kutokana na usumbufu huo kwa watumishi wa umma, Mtaka alisema taasisi ambayo itabainika au kukutwa na kadi hizo, haitaruhusiwa tena kufanya kazi hiyo katika mkoa wake.

Alitangaza marufuku hiyo mwishoni mwa wiki wilayani Itilima wakati wa hafla ya kuwapongeza walimu, wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wilaya ya Itilima waliofanya vizuri mitihani ya kitaifa mwaka jana.

Aliwataka wamiliki wa taasisi hizo kuacha mara moja utaratibu huo kwani utawagharimu na kwamba taasisi hizo zimekuwa zikiwapatia mikopo watumishi, wengi wao wakiwa walimu, huku sharti likiwa kuweka rehani kadi zao za benki na nywila (Password).

Alisema taasisi yoyote ya fedha ambayo imemkopesha mwalimu ikikutwa na kadi ya benki ya mwalimu aliyepewa mkopo, hatua kali tutazichukua ikiwamo kuzifukuza kufanya kazi Simiyu.

Vitendo hivyo  na vingine vya kitapeli vimekuwa vikifanywa na taasisi kadhaa za kukopesha fedha dhidi ya wakopaji, lengo likiwa ni kuchukua mali za wakopaji baada ya kushindwa kurejesha mikopo hiyo.

Sababu kubwa inayosababisha taasisi za aina hii kuchukua mali za wakopaji zilizowekwa kama dhamana, ni kuwaingiza katika mikataba ya ovyo ambayo haina uwazi.

Katika hali hiyo, wakopaji wanajikuta wakishindwa kurejesha mikopo hiyo kutokana na riba zisizo na uhalisia. Kwa hiyo tunakubaliana na hatua alizozitangaza Mtaka zenye lengo la kuwanusuru watumishi wa umma dhidi ya utapeli huo.

Kimsingi, utaratibu wa kukopa ni kwamba mkopaji anatakiwa kuweka dhamana ya mali zinazohamishika na zisizohamishika kama nyumba, shamba, kiwanga, gari, mashine na mali zingine kadiri mkataba na taratibu  za ukopeshaji zinavyotaka.

Hata hivyo, haiwezekani mtu akopeshwe fedha halafu anatakiwa kuweka dhamana ya kadi ya benki na nywila. Hapa lazima mkopaji ajiulize kwanza lengo la sharti hilo ni nini?

Kuna matukio mengi ya namna hii yamewakuta wakopaji wengi na kujikuta wakipoteza mali zao nyingi zikiwamo fedha, kutokana na akaunti zao kukosa usalama kutokana na kadi zao na namba za siri kubakia kwenye mikono ya wakopeshaji.

Tunampongeza RC Mtaka kuliona hili na kuamua kuchukua hatua, hivyo tunawashauri viongozi wengine wenye dhamana ya kulinda usalama wa raia na mali zao kufanya hivyo katika maeneo yao ya kiutawala.

Jambo la kushukuru ni kuwa serikali imeshaona umuhimu na kuanza kuchukua hatua za kuiwekea sheria sekta ndogo ya huduma za fedha ambayo ilitungwa mwaka 2028 na kanuni zake kupitishwa mwaka 2019.

Sheria hii itaanza kutumika rasmi Novemba Mosi, mwaka huu baada watoa huduma ndogo za fedha kuwa wameomba leseni na wengine kuomba usajili ifikapo Oktoba 31, mwaka huu.

Lengo la sheria hii ni kuwatambua watoa huduma ndogo za fedha wakiwamo wakopeshaji, Saccos na Vikoba. Lengo pia ni kuwaendeleza na kuwawezesha. Kanuni za sheria hii zinawataka watoa huduma kuwa wawazi katika riba na uendeshaji wa shughuli zao kwa ujumla.

Ni sheria iliyokuja kwa wakati, kutokana na kuwapo sintofahamu katika suala zina la utoaji wa huduma ndogo za fedha katika maeneo mengi nchini. Bila shaka watoa huduma hizo watajisajili na wengine kuomba leseni kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT) katika muda uliowekwa kisheria.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com







## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Wanafunzi watambue mimba ni adui wa elimu

**MIMBA** ni miongoni mwa matatizo yanayoendelea kuwakumbuka wanafunzi wa shule za msingi na sekondari nchini na kusababisha wakatishe masomo, hali inayoonyesha kuwa tatizo hilo bado halijapata dawa.

Usugu wa tatizo hilo unatokana na kuwapo kwa taarifa kutoka maeneo mbalimbali nchini zinazoonyesha kuwapo kwa mimba hizo zinachodaiwa kuchangiwa na sababu kadhaa.

Taarifa za kuwapo za mimba za wanafunzi zipo karibu kila kona ya nchi, lakini nagusia sehemu moja tu ya Wilaya ya Liwale mkoani Lindi, ambako kwa tangu shule zifunguliwe, zaidi ya wanafunzi 10 wamekutwa na mimba.

Shule zilifunguliwa Januari 6 mwaka huu na wilaya ikaendesha zoezi la kuwapima mimba wanafunzi wa shule za sekondari ambalo bado linaendelea, lakini tayari zaidi ya wanafunzi 10 wamekutwa wana ujauzito.

Hiyo ni kwa kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya ya Liwale, Sarah Chiwamba, kwamba lengo ni kutambua ukubwa na kutafuta njia za kuwasaidia watoto wa kike kuepuka kuingia katika mtego huo.

Inaonekana walipata mimba hizo wakiwa likizo, hivyo bado wazazi, walezi na jamii kwa ujumla inatakiwa kutambua umuhimu wa kaulimbiu ya Mama Salma Kikwete ili kumuokoa mtoto wa kike kutoka kwa adui huyo.

Inaumiza kuona mwanafunzi anapata ujauzito na kulazimika kukatisha masomo, hivyo ni vyema wazazi, walezi na jamii kwa ujumla kutambua kuwa mtoto wa kike anatakiwa kuthaminiwa ili atimize ndoto zake.

Hatua hiyo inaweza kuwa njia mojawapo ya vita dhidi ya mimba hizo, na vilevile ni muhimu kutambua kuwa vita hiyo kwa nchi hii haikuanza leo wala jana, bali ni ya muda mrefu.

Mimba hizo zinapigiwa kelele na wadau mbalimbali wa elimu na watetezi wa haki za mtoto wa kike kwa lengo la kumwacha asome, lakini bado mimba zimeendelea kuripotiwa maeneo mbalimbali.

Kuna haja ya kuamka na kuunga mkono kampeni za kukemea mimba na pia wazazi, walezi na jamii kwa ujumla isizibe masikio kwa lengo la kukwepa ujumbe wa kuwasaidia kuachana na tabia ya kukumbatia tabia hiyo chafu.

Vilevile wanafunzi wa kike wanatakiwa kutochanganya mapenzi na shule kwa wakati mmoja, kwa sababu kufanya hivyo mbali na kupata mimba, wanaweza kupata maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU).

Wanafunzi wanatakiwa kutumia muda wao wa masomo kwa manufaa ikiwa ni pamoja na kusoma kwa bidii, kwani itawasaidia katika maisha yao ya baadaye kuliko kuendekeza mambo ambayo watakutana yao baada ya masomo.

Jambo la msingi ni kuepuka kuwa katika mazingira yanayoweza kuwasababishia kupata mimba na kukatisha masomo, kutokana na ukweli kwamba mimba ni adui wa maendeleo ya elimu kwa watoto wa kike.

Watu wazima wenye tabia ya kunyemelea wanafunzi wa kike, wakumbuke kaulimbiu ya  mke wa Rais wa Awamu ya Nne, Mama Salma Kikwete kwamba: "Mtoto wa mwezio ni wako".

Kaulimbiu hii ililenga kuikumbusha jamii kutambua kuwa watoto wote wanapaswa kuonyeshwa upendo, hajjalishi siyo wa kumzaa au uliyemkuta barabarani, hivyo walindwe.

Wanafunzi pia waepuke tamaa na kuridhika na maisha halisi ya nyumbani kwao, badala ya kukubali kurubuniwa na kujikuta wakiingia kwenye mtego wa mapenzi, ambayo mwisho wake ni kupata mimba.

Hawaishii kupata mimba tu , wakati mwingine ni kupata Ukimwi na pia kukatisha masomo kwa sababu ya tamaa ya kutaka kupata vitu vingi kwa njia mkato na kumbe ni mtego wa kuwaharibia maisha.

Iwapo kila upande utasimama kwenye nafasi yake, adui huyu wa wanafunzi wa kike anaweza kupungua kama siyo kumalizika, na njia mojawapo wa kukabiliana naye ni kuzingatia kaulimbui na Mama Salma Kikwete.

Wazazi, walezi na jamii kwa ujumla kutimiza wajibu, lakini pia wanafunzi wenyewe kuwa makini, watambue kuwa wako shuleni kwa ajili ya masomo na si zaidi ya hapo, vinginevyo ni kutafuta matatizo.

Kikubwa ni kwamba mtoto wa kike aachwe asome atimize ndoto zake, na jamii itambue kuwa mimba ni adui wa maendeleo ya elimu kwa mtoto wa kike, asipewe nafasi, apigwe vita kila kona.

# Mansoor amwandikia upya DPP kukiri kosa

**Na Hellen Mwango**

MKURUGENZI wa zamani wa Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Kulthum Mansoor, amemwandikia barua upya Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) ya kukiri na kuomba msamaha dhidi ya tuhuma za kutakatisha Sh. bilioni 1.477.

Mapema Januari 6, mwaka huu, Wakili wa Utetezi, Elia Mwingira, alidai katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Mfawidhi Godfrey Isaya.

Jana kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa na iliahirishwa na Hakimu Mkazi, Vick Mwaikambo, baada ya Hakimu Isaya kuwa na udhuru wa kikazi. Awali, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Simon Wankyo alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika aliomba tarehe ya kutajwa.

Hakimu Mwaikambo alisema kesi hiyo itatajwa tena Machi 16, mwaka huu na mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu.

Hata hivyo, baada ya kuahirishwa kesi Wakili Utetezi Mwingira, aliieleza Nipashe kuwa tayari mteja wake ameandika upya barua kwa DPP kuomba kuanza mchakato upya wa kukiri na kuomba msamaha na kwamba anasubiri kuwasilisha taarifa hiyo mbele ya Hakimu Isaya, anayesikiliza kesi hiyo.

Oktoba, 2019, kigogo huyo wa Takukuru wa zamani aliandika barua ya kukiri mashtaka na kuomba msamaha kwa DPP, lakini walishindwa kufikia muafaka wa makubaliano.

Katika kesi ya msingi, Mansoor anakabiliwa na mashtaka manane ya kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha Sh. bilioni 1.477.

Ilidaiwa katika tarehe tofauti kati ya Januari 2013 na Mei 2018, msitakiwa alighushi barua ya ofa ya Agosti 13, 2003 kwa madhumuni ya kuonyesha kuwa, barua hiyo imetolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo huku akijua kuwa sio kweli.

## Masauni kuwabana wakimbizi wadanganyifu

**Na Pendo Thoma,** KIGOMA

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, ameviagiza vyombo vya ulinzi na usalama mkoni Kigoma kuwachukulia hatua kali za kisheria baadhi ya wakimbizi wanaovunja sheria za ukimbizi na kutekeleza vitendo vya uhalifu ikiwamo wizi, utekaji wa magari, uporaji na mauaji.

Masauni aliyasema hayo jana wakati wa majumuisho ya ziara yake mkoani hapo na kueleza kuwa vyombo vya ulinzi na usalama vinapaswa kuendelea kudhibiti uvunjifu wa amani na kuharakisha kuwarudisha nchini kwao wakimbizi watakaobainika kujihusisha na vitendo hivyo.

"Huwezi kuwa mkimbizi unavunja amani ya nchi yetu kuna haja ya kuhakikisha sheria zinafuatwa ili kuwachukulia hatua hawa watu na kuwaondoa hawa watu haraka niwaelekeze vyombo vya ulinzi na usalama kutekeleza hilo," alisema. Masauni alizungumza na wakimbizi kutoka nchi jirani ya Burundi na kuwataka kurudi kwa hiari nchini kwao kwenda kutekeleza haki yao ya kuchagua kiongozi wanayemtaka katika uchaguzi mkuu utakao fanyika mwezi Mei, mwaka huu.

Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Brigedia Jenerali mstaafu Emmanuel Maganga, alisema zoezi la kuwarudisha wakimbizi nchini kwao liaendelea kwa kuwasafirisha mara mbili kwa wiki ingawa makubaliano ya idadi ya wakimbizi 2,000 kwa wiki haifikiwi.

Maganga alisema kumeibuka tabia ya baadhi yao kufanya udanganyifu wakati wa kujisajili kuondoka hivyo baadhi ya familia kuondoka nusu na wengine kubaki jambo ambalo linaweza sababisha waliorudishwa nchini kwao kurudi kwa njia za panya na kuendelea kuishi.

"Tumegundua kwamba kuna ujanja wa kugawa hizi familia tukisema familia 80 wanazigawa baadhi wanabaki sisi hilo hatukubali, nimuagize mkuu wa kanda idara ya wakimbizi alisimamie vizuri," alisema.

**Letshego**

**PRE- QUALIFICATION OF SUPPLIERS FOR PROVISION OF GOODS AND SERVICES FOR THE YEAR 2020**

**REF: LBT/FIN/2020/02/0517**

**LETSHEGO BANK (T) LIMITED** is requesting interested reputable and competent Vendors and Service Providers to submit their proposal to provide the following services listed below:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Consultation services | 16 | Refurbishment works |
| 2. | Event management | 17 | Electrical equipment supplies / service and maintenance |
| 3. | General office stationery | 18 | Money Counter supply, maintenance and services |
| 4. | Accommodation/Lodging Services | 19 | Health Insurance |
| 5 | Computer & IT supplies and services | 20 | Recovery and Auction services |
| 6. | Office furniture | 21 | Services to perfect loan security documents |
| 7. | Repair and Maintenance of Buildings (plumbing, paintings etc.) | 22. | Valuation services |
| | | 23. | Motor vehicle/ motor bike repair and maintenance |
| 8. | Promotional materials | 24. | Training and development services |
| 9. | Printing of Brochures, booklets, posters and related products | 25. | Recruitment services |
| | | 26. | Supply, maintenance and services of Generators |
| 10. | Air conditioning supply & services | 27. | Kitchen and general office supplies (tea sugar, coffee milk, cleaning items etc.) |
| 11. | Travel and tours services (Air ticketing, vehicles hiring, tourism services etc.) | 28. | Safe & Vault |
| 12 | Physical security(Guards, Intruder alarm, Alarm response) | 29. | Structured Cabling |
| 13 | Cash In Transit | 30. | Leasing of printers/Scanners |
| 14 | Fire extinguisher supply and services | 31. | Courier services |
| 15 | Catering services | 32. | Cleaning and Fumigation |

**Documents required and information**
Interested and competent Vendors wishing to provide their services in line with the above listed services must submit the following documents for verification, without which the company will be disqualified:

Company profile, Certificate of incorporation, tax clearance certificates, TIN, VRN, Business license, Memorandum and articles of association, company registered address, functional contact E-mail address, telephone number and contact person, Reference letters from three previous clients of similar projects satisfactorily executed, reference letter from the bank, Three Years Company's audited financial statements, duly stamped by a registered auditor and insurance cover.

**SUBMISSION**
Application for the expression of interest accompanied by the above listed documents should be submitted in a wax sealed envelope boldly marked **REF NO: LBT/FIN/2020/02/0517.................addressed to:**

**Chief Financial Officer**
**Letshego Bank (T) limited**
**P.O.BOX 34459**
**PLOT NO 395 URSINO**
**MWAI KIBAKI ROAD**

**Contacts:**
**For more information please use contacts below**
**E-mail:TZ.logistics@letshego.com**
**Phone no: +255 22 2225048**

**CLOSING DATE:**
All submissions must be received at the above office not later than 15/03/2020 at 4:00pm.

215652802

# ACT-Wazalendo kujadili tume huru mkutano mkuu

**Na Enock Charles**

CHAMA cha ACT-Wazalendo, kimeeleza mambo manne yatakayojadiliwa kwenye kikao cha mkutano mkuu wa chama hicho unaotarajiwa kufanyika mwezi huu.

Kimetaja mambo hayo kuwa ni mabadiliko ya Katiba ya chama hicho, kuwahimiza wanachama kudai tume huru ya uchaguzi, kuitaka serikali kujiandaa kukabiliana na virusi vya corona na uteuzi wa wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Kiongozi Mkuu wa chama hicho, Zitto Kabwe, alisema mkutano huo uliofanyika jana ni maandalizi ya mkutano mkuu wa chama hicho uliotangazwa kuanza Machi 14 na 16, mwaka huu.

"Ni wajibu wa kikao hiki kuandaa mkutano mkuu wa chama ambao tayari umetangazwa kuwa utafanyika Machi 14 na 16 na utakuwa na ajenda mbalimbali," alisema Zitto.

Alisema pamoja na mambo mengine ya kikatiba kikao hicho kitafanya uteuzi wa wagombea wa ngazi za kitaifa katika uchaguzi mkuu wa chama hicho, ikiwamo wazee, vijana na wanawake ambao tayari wanachama mbalimbali wameshachukua fomu kuwania nafasi hizo.

Ajenda nyingine ni kupokea taarifa ya azimio la kupitia upya katiba ya chama hicho ili kuifanyia marekebisho iendane na sheria mpya ya vyama vya siasa na mazingira ya sasa ya kisiasa nchini na ukuaji wa chama hicho alichodai kimepata mafanikio makubwa kisiasa mwaka huu ikilinganishwa na miaka iliyopita hasa kwa kupata wanachama wapya Zanzibar na Bara.

Aliwataka wajumbe kuweka mazingira sawa kwa kuwa dunia ya sasa inataka uwiano wa kijinsia katika uongozi, huku akionya uwezekano wowote wa ubaguzi katika uongozi ndani ya chama hicho na kuhakikisha kunawekwa mazingira sawa kwa kila mwanachama kwa kuwa kila mwanachama atakayeteuliwa na chama hicho anafaa kuwa kiongozi.

Kuhusu tume huru ya uchaguzi, aliishauri halmashauri kuu ya chama hicho kuweka azimio la kuwataka wanachama kudai tume hiyo kwa kuwa ni ya lazima ili kuhakikisha uchaguzi unakuwa huru na wa haki, na kuto kuwapo kwa tume huru ni vigumu kuwa na uchaguzi huru na wa haki.

Kiongozi huyo pia alizungumzia tishio la ugonjwa wa corona duniani na kuiomba halmashauri kuu iazimie kuitaka serikali kujiandaa kikamilifu kukabiliana na ugonjwa huo akieleza kuwa unaweza kuwa na athari mbaya katika uchumi wa nchi.



Wafagiaji wa barabara wakiwa kazini eneo la Mwenge, jijini Dar es Salaam jana, huku wameweka alama ya tahadhari kwa vyombo vya moto kwa ajili ya usalama wao. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mabilioni yaokolewa kituo waraibu dawa za kulevya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KUANZISHWA kwa kituo cha kuhudumia waathirika wa dawa za kulevya Itega mkoani Dodoma, kumeondoa kwenye mzunguko kiasi cha Sh. bilioni 2.7 zilizokuwa zikitumiwa na waraibu kila mwaka kununua dawa aina ya Heroin.

Kituo hicho kina waraibu 367 ambao kwa sasa wanatibiwa kwa kutumia dawa ya Methadone.

Meneja wa Asasi Isiyo ya Kiserikali inayopambana na dawa za kulevya (Mefada), Alex Chitawala, aliyasema hayo alipojibu baadhi ya hoja za wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi na Dawa za Kulevya alipotembelea kituo hicho jana.

Alisema asasi zisizo za serikali zina mchango mkubwa katika kupambana na dawa za kulevya na wamekuwa wakiwafuata kwenye vijiwe watumiaji wa dawa hizo ili kuwaondoa katika baa hilo. "Kete moja ya Heroin Dodoma inauzwa kwa Sh. 7,000 na kiwango cha chini cha matumizi kwa mtu mmoja ni kete tatu kwa siku, hivyo zaidi ya Sh. milioni 7.7 zimeokolewa kwa siku na Sh. milioni 231 kwa mwezi na kwa mwaka ni Sh. bilioni 2.7 tumeiondoa kwenye mzunguko wa dawa za kulevya," alisema.

Alibainisha kuwa kwa Mkoa wa Dodoma, Dodoma mjini inaongoza kwa kuwa na waathirika wengi zaidi ikifuatwa na Kibaigwa na Mpwapwa.

Alisema tiba kwa waathirika hao hufanyika kila siku na hivyo wanakabiliwa na tatizo la usafiri wa kila siku kufika kwenye kituo.

Mkurugenzi wa Idara ya Kinga, Dk. Leonard Subi, alisema serikali inaendelea kupambana na matumizi ya dawa za kulevya na inatarajia kufungua kituo cha Methadone mkoani Tanga mwezi ujao. Alisema dawa za kulevya ni vita ambayo inahitaji ushirikishaji wa sekta mbalimbali.

Awali, akitoa taarifa ya kituo hicho, Mkurugenzi wa Hospitali ya Mirembe na Kituo cha Itega, Dk. Erasmus Mndeme, alisema waraibu hufika kituoni hapo kupitia asasi zisizo za serikali zikiwamo Mefada, Yovaribe na YCR.

Alibainisha kuwa kwa sasa, kituo kina waraibu 479. Kati yao, 367 wanatumia dawa ya Methadone kila siku.

Alisema waraibu 26 wanaishi na Virusi vya Ukimwi (VVU) na wanne waligundulika kuwa na maambukizo kifua kikuu.

"Wengine 176 walipimwa homa ya ini ambapo 64 sawa na asilimia 36 waligundulika kuwa na homa ya ini aina ya B na C," alisema. Dk. Mndeme aliomba kamati hiyo kuwa mabalozi katika upatikanaji wa ajira na ushirikishwaji wa waraibu katika shughuli za kijamii ili wajiongezee kipato.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Oscar Mukasa, aliitaka serikali kuangalia kwa makini maambukizo ya homa ya ini kwa waathirika hao kutokana na kuwa nayo kwa kiwango kikubwa. "Pia, tunahitaji kipimo cha pamoja ili kujua kiwango cha dawa za kulevya kikoje nchini kwa sasa kutokana na jitihada zilizopo, maana tunaona kuna takwimu za malaria, Ukimwi, kifua kikuu lakini kwa dawa za kulevya hazipo," alisema.

## Mwekahazina Mkinga akalia kuti kavu

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amemwagiza Katibu Tawala wa Mkoa wa Tanga, Judica Omari, achunguze utendaji kazi wa Mwekahazina wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga, Juan Mening.

Amesema hajaridhishwa na utendaji wake kutokana na kushindwa kusimamia ukusanyaji wa mapato na hata hicho kidogo kinachokusanywa hakifikishwi serikalini.

Alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga pamoja na wananchi baada ya kufungua jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Tanga.

Waziri Mkuu amesema serikali inataka kila mtumishi wa umma nchini awajibike kwa kufanya kazi kwa bidii na kwamba Serikali ya Awamu ya Tano haitowavumilia watumishi wezi, wabadhirifu, wavivu na kuwachukulia hatua.

"Watumishi fanyeni kazi kwa bidii na msitarajie kuundiwa tume pale mnapofanya vibaya, ukiharibu kazi tunakushughulikia hapo hapo na huu ndio msimamo wa serikali."

Aliwaambia watumishi hao kuwa wanatakiwa wafanye kazi kwa kuzingatia sheria na kanuni za utumishi wa umma na pia watambue dhamana kubwa waliyonayo, ambayo ni kuwahudumia wananchi wote bila ubaguzi.

Pia aliwataka madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga kuwa wakali wanaposimamia makusanyo ya mapato pamoja na matumizi.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu ametoa siku 18 kuanzia jana kwa watumishi wa halmashauri hiyo wanaoishi jijini Tanga wawe wamehamia katika kituo chao cha kazi na watakaoshindwa wabaki waliko.

Alisema serikali inataka watumishi wa umma wawajibike na waishi katika vituo vyao vya kazi. "Nawataka watumishi wote wa wilaya hii wanaoishi jijini Tanga wawe wamehamia hapa ifikapo Machi 20, mwaka huu na wasiohamia waendelee kubaki huko huko."

# Taasisi za fedha zaonywa urasimu kwa wawekezaji

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amezitaka taasisi za kifedha nchini kuacha urasimu katika utoaji wa mikopo kwa wawekezaji wa viwanda vya ndani.

Amezitaka kuwakopesha ili kukuza mitaji yao na kuongeza ajira kwa vijana.

Balozi Iddi alibainisha hayo wakati wa ziara yake ya kutembelea na kukagua eneo la ujenzi wa viwanda vitatu katika eneo la Chapulwa, Halmashauri ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga, vinavyojengwa na wawekezaji wa ndani wa Kahama Oil Mills (KOM).

Alisema baadhi ya taasisi hizo zimekuwa zikitoa masharti magumu kwa wawekezaji wa ndani wanapohitaji kukopeshwa fedha kwa ajili ya kukuza biashara zao na kusababisha wengi wao kushindwa kuwekeza kwa tija.

"Nizitake taasisi hizi zitambue umuhimu wa wawekezaji wetu wa ndani kama vile kampuni hii ya KOM, ambayo inaendelea na uwekezaji katika eneo hili...riba ipunguzwa ni Watanzania wengi watanufaika kwa kupata mikopo ambayo itasaidia kukuza uwekezaji wao," alisema Balozi Idd.

"Mkoa wa Shinyanga umetia fora katika uhamasishaji wawekezaji wa ndani katika ujenzi wa viwanda...nimekagua eneo hili ambako kunajengwa viwanda zaidi ya vitatu na Watanzania zaidi ya 2,000 watapata ajira," aliongeza Balozi Idd.

Aidha, Balozi Idd alisema sera ya awamu hii ya tano imejikita katika uanzishwaji wa viwanda, hivyo taasisi hizo hazinabudi kuunga mkono juhudi za kueleka katika uchumi wa kati na kuwawezesha wananchi wengi kupata ajira za kudumu na kuongeza uchumi wa Taifa.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, alitoa rai kwa wawekezaji wa ndani na nje kuja kuwekeza katika mkoa huo kutokana na wingi wa fursa zilizopo.

Meneja wa kampuni hiyo, Braison Edwad, alisema gharama za uwekezaji wa kiwanda kinachojengwa katika eneo hilo ni zaidi ya Dola za Marekani milioni 10 na viwanda vitakavyojengwa ni vya maji, soda na kusaga nafaka.



Uchafu ukiwa umekithiri kwenye Soko la Kambarage, Manispaa ya Shinyanga na kutishia usalama wa afya za wafanyabiashara wa soko hilo pamoja na wateja. **PICHA: MARCO MADUHU**

# DC awataka wanafunzi wa kike kuwaepuka wanaume

**Na Elizabeth Zaya**

MKUU wa Wilaya ya Iringa, Richard Kasesela, amewataka wanafunzi wa kike kutojirahisisha kwa wanaume ili waepukane na kufanyiwa vitendo vya ukatili.

Kasesela aliyasema hayo mwishoni mwa wiki mkoani Iringa wakati akipokea msafara wa kijinsia wa kutokomeza ukatili huo mkoani humo.

Alisema vitendo vya kikatili vimekuwa vikiongezeka siku hadi siku hasa katika familia na vimekuwa vikifumbiwa macho na kumalizana kimya kimya.

"Msijirahisishe watoto wangu mnatupa tabu sana maana tumekuwa tunapambana na vitendo vya ukatili halafu ninyi nanyi mnajirahisisha," alisema Kasesela.

Kasesela alisema kumekuwa na ongezeko la mimba na ndoa za utotoni na ulawiti kwa watoto wa kiume ambao wamekuwa wakiharibiwa na kusababishiwa maumivu na ukatili wa kisaikolojia.

Alisema serikali imejipanga kuhakikisha inasimamia ustawi wa jamii ikiwamo kuwalinda watoto, wanawake na watu wenye ulemavu dhidi ya vitendo hivyo.

"Tusikae kimya tuseme na tutoe taarifa kwa vyombo vya kisheria kuhusu vitendo vya kikatili vinavyotokea katika familia na jamii zetu," alisema.

Mwakilishi wa Katibu Mkuu Idara Kuu, Maendeleo ya Jamii wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Imelda Kamugisha, alisema vitendo vya ukatili vimekuwa vikitokea kwenye jamii, na kwamba takwimu zinaonyesha wanawake asilimia 30 walio kwenye ndoa wanafanyiwa ukatili wa kijinsia.

"Kutokana na kuongezeka kwa vitendo vya ukatili, serikali imeongeza vituo vya huduma jumuishi na namba ya kutoa ripoti ya vitendo vya ukatili kwa watoto ili kuchukua hatua katika mapambano dhidi ya vitendo hivyo vya kikatili," alisema.

Kwa upande wake wakili kutoka Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (Rita), Janeth Mandawa, alitoa wito kwa wanaume kuandika wosia ili kuondokana na vitendo vya kikatili vinavyowakumba wanawake wajane katika jamii ili kuwasaidia kupata haki zao stahili.

"Sisi tunahusika na masuala ya wosia, kuandika wosia sio kufa ila inasaidia kutoa maelekezo baada ya mume au mke kufariki ili tuondokane na vitendo vya ukatili," alisema.

## Tanesco kupeleka umeme mgodini

**Na Restuta Damian,** BIHARAMULO

MWENYEKITI wa Bodi ya Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco), Dk. Alexander Kyaruzi, ameahidi kupeleka nishati ya umeme katika mgodi wa kuchimba na kuchenjua dhahabu wa Stamigold uliopo kijiji cha Mavota Kata ya Nyantakara wilayani Biharamulo mkoani Kagera kwa lengo la kuokoa Sh. bilioni moja inayotumika kununua mafuta ya uendeshaji kwa mwezi.

Dk. Kyaruzi alitoa ahadi hiyo baada ya kutembelea na kujilidhisha na mitambo ya uchenjuaji dhahabu na mashine inayotumia mafuta ya aina ya diseli katika uendeshaji wa shughuli za mgodini huo.

Amesema kama Tanesco itatoa nishati ya umeme wa gridi ya Taifa kwa wateja hao, itaondoa gharama na kubaki Sh. milioni 300 za ununuzi wa umeme na Sh. milioni 700 zinazobakia zitaingizwa katika mfuko wa Serikali Kuu kufanya shughuli nyingine.

"Nimefika nimejiridhisha na kuona kwamba Tanesco tutatoa umeme kwa wateja wa mgodi huo, ambao shughuli zao za uzalishaji zinaonekana, na wao waweze kupunguza gharama na fedha nyingine kuingizwa mfuko mkuu wa serikali ifanye majukumu mengine," alisema Kyaruzi.

Aidha, alisema kama matumizi ya mafuta yatapunguzwa kutokana na kufikiwa umeme, kuna uwezekano wa kodi kulipwa vizuri pamoja na kuongeza uzalishaji.

Meneja Mkuu wa Mgodi wa Stamigold, Mhadisi Gilay Shamika, alisema tangu mwaka 2005, kumekuwa na changamoto ya ufuatiliaji na upatikanaji wa nishati ya umeme wa Tanesco.

Shamika alisema kuwa, ujio wa nishati hiyo utasaidia kutapunguza manunuzi ya mafuta ya Sh. bilioni moja kwa mwezi hadi Sh. milioni 300 na kwamba kiasi kinachobakia cha shilingi milioni 700 itaingia kwenye uzalishaji mwingine.

Msimamizi kitengo cha matengenezo, Daud Hamis, alisema ili kufanikisha uzalishaji wanatumia jenereta nne za mafuta ambazo hutumia lita 190 hadi 200 kwa siku.

# Mzindakaya awapa somo wazee

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

WAZEE mjini Sumbawanga, mkoani Rukwa wameshauriwa kufanya shughuli za kiuchumi ili wajipatie kipato na kuacha tabia ya kuomba omba misaada barabarani.

Akichangia katika kikao maalumu cha wazee wa mji huo, mwanasiasa mkongwe Dk. Chrisant Mzindakaya, alisema baadhi ya wazee wamekuwa na tabia ya kutojishughulisha na shughuli zozote za kiuchumi badala yake wanategemea kuomba mitaani.

Alisema kuwa mzee siyo sababu ya kutojishughulisha na shughuli ndogo ndogo kama kulima bustani za mboga, kufuga mifugo midogo kama kuku, bata na sungura ambayo itawawezesha kujipatia kipato kwa ajili ya matumizi yao.

"Wazee wenzangu nawaomba sana mbadilike ninyi hapo hamna watoto, watoto wenu hawakai nanyi nyumbani wana nyumba zao ambazo wanaishi na wajukuu zenu sasa kilichopo lazima ubuni shughuli yoyote itakayo kusaidia kujipatia kipato ambacho kitakusaidia na baadhi yenu mtaacha na kutembea barabarani kwa ajili ya kuomba misaada," alisema.

Katika kikao hicho, Mkurugenzi wa Manispaa ya Sumbawanga Jacob Mtalitinya, alisema kutokana na halmashauri hiyo kukusanya mapato zaidi ya asilimia 100 la lengo walilojiwekea la Shilingi bilioni mbili, halmashauri hiyo imeamua kuwalipia wazee 300 ili wajiunge na huduma za CHF iliyoboreshwa.

Alisema kumekuwa na changamoto kubwa kwa baadhi ya wazee kupata matibabu hasa katika magonjwa yasiyoambukiza ambayo pia yanakuwa ni ya kudumu na matibabu yake huwa na gharama kubwa hali inayosababisha wazee hao hushindwa kumudu gharama hizo.

Meya wa manispaa hiyo, Justine Malisawa, aliwashukuru wazee hao kuhudhuria kikao hicho na kupata fursa ya kujua mambo mbalimbali ikiwamo taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kujua ni maendeleo gani yamefikiwa kutokana na wao kuwa kundi ambalo halipati taarifa kwa wakati.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa daraja linalounganisha eneo la Magomeni Kwa Harubu na Mwananyamala, Manispaa ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wananchi watakiwa kushiriki upitishaji bajeti

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WANANCHI wametakiwa kushiriki katika mikutano inayoitishwa kwenye maeneo yao hususani ya kupitisha bajeti na kujadili mapato na matumizi.

Pia, wametakiwa kuwa na uhusiano wa karibu na viongozi wao waliopo madarakani ili kuwezesha mipango ya maendeleo kwenda kadiri ilivyopangwa.

Akiongea, katika mafunzo ya kuwajengea ufahamu vijana yaliyofanyika juzi Mjini Kibaha, kuhusu bajeti za serikali na fursa walizokuwa nazo, mtoa mada Bumija Senkondo alisema, ushirikiano kwenye jamii ni chanzo cha kuharakisha maendeleo.

Bumija alisema, wananchi wanatakiwa kushiriki kikamilifu katika uundwaji wa bajeti kabla mapendekezo hayajafikia ngazi za juu, ili waweze kutoa maoni yao na kupendekeza miradi ambayo itakuwa na manufaa kwao.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Hassan Forodha alisema, ni vema elimu kama hiyo ikafika vijijini ili nao wapate uelewa wa umuhimu wa kushiriki mikutano pamoja na kuhoji mapato na matumizi.

Forodha alisema, baadhi ya wananchi vijijini, wanawaogopa viongozi wao wanashindwa kuhoji maendeleo ya miradi kwenye maeneo yao na taarifa za mapato na matumizi, hivyo elimu hiyo itawasaidia kuwa na mabadiliko.

Mkurugenzi wa Shirika la Youth Partnership Countrywide (YPC), Israel Ilunde, waandaji wa mafunzo hayo kwa kushirikiana na Shirika la Action Aid alisema, vijana 25 walishiriki kutoka katika Taasisi za dini, Asasi za vijana, mashirika ya umma na vyama vya siasa.

Ilunde alisema, mafunzo hayo yatakuwa endelevu ya mchakato wa kuwajengea uwezo vijana kiuchumi na kisiasa.

# Ukerewe yapania kutokomeza malaria

**Na Jovither Kaijage,** UKEREWE

MKUU wa Wilaya ya Ukerewe mkoani Mwanza, Cornel Magembe, amesema asilimia 51.2 ya wanafunzi wa shule za msingi wilayani humo wanaugua ugonjwa wa malaria.

Wagonjwa 112,098 kati ya 287,363 sawa na asilimia 39 ya wagonjwa waliopimwa afya zao katika vituo vya afya vya wilaya hiyo mwaka 2019 wamekutwa na vimelea vya ugonjwa wa malaria, huku wajawazito 16 kati ya 100 wanaofika kliniki wanakutwa na ugonjwa huo.

Magembe alisema hayo mjini Nansio jana wakati akizindua shughuli ya kunyunyiza dawa ya kuua mbu majumbani kwa kiuatilifu katika nyumba 87,599 zilizopo kwenye kata 25 za wilaya hiyo.

Alisema kufuatia ukubwa wa tatizo hilo, serikali kwa kushirikiana na Shirika la Abt Associates kwa ufadhili wa Serikali ya Marekani, kupitia Usaid, umeanzishwa mradi huo utakaotekelezwa kwa siku 27 kuanzia Machi 3 kwa gharama ya Sh. bil. 5.015.

Akifafanua, Magembe alisema tayari ameagiza kamati za ulinzi na usalama kuanzia ngazi ya kijiji hadi wilaya zihakikishe mradi huo unatekelezwa bila vikwazo kwa lengo la kutokomeza ugonjwa huo.

Mmoja wa wanyunyizia dawa majumbani, Mariam Taitus, alisema pamoja na kupata kipato pia mradi huo utasaidia kudhibiti malaria ambayo inaathiri zaidi maisha ya watoto na wajawazito.

Alisema watatekeleza kwa vitendo viapo vyao vya kutunza siri na kuomba wananchi wawape ushirikano.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Thomas Rutachubilwa, alisema utekelezaji wa mradi huo unakwenda sambamba na unyunyizaji wa dawa kwenye madimbwi ili kuua mazalia ya mbu pamoja na usafi wa mazingira.

"Miaka mitano iliyopita tulifanikiwa kudhibiti malaria katika wilaya hii hadi asilimia 20, lakini kulitokea upungufu na kusababisha maambukizi kupanda na kuifanya Wilaya ya Ukerewe kuongoza kati ya wilaya nane za Mkoa wa Mwanza kwa asilimia 51.2," alisema.

Akifafanua alisema, kwa uzoefu waliopata katika visiwa vya Zanzibar na Comoro, dawa hiyo ya kiuatilifu ya kunyunyiza majumbani na kuangamiza mazalia ya mbu inaweza kusaidia kudhibiti ugonjwa huo katika visiwa 38 vya wilaya hiyo.

# Mbunge ajipanga kupambana na ngariba

**Na Allan Isack,** HANANG'

MBUNGE wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara, Martha Umbullah, amesema watapambana na ngariba wanaokeketa watoto wa kike na kufanya shughuli hiyo kama njia ya kujipatia mikopo kwenye halmashauri.

Hali hiyo imetokana na baadhi ya ngariba wilayani humo kufanya shughuli ya ukeketaji kama sehemu ya kujipatia kipato.

Mkoa wa Manyara unaongoza kwa ukeketaji kwa wastani wa asilimia 58, huku Wilaya ya Hanang' ikitajwa kuwa ni miongoni mwa wilaya mkoani humo, zinazoongoza kwa vitendo vya ukeketaji, hivyo kusababisha mkoa huo kuwa kinara wa matukio ya ukatili wa kijinsia.

Umbullah aliyasema hayo juzi katika Mji Mdogo wa Katesh, wakati akizungumza na wanawake wanachama wa Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT) Wilaya ya Hanang' na ngariba wanaokeketa watoto wa kike wa eneo hilo.

Alisema endapo ngariba hao wakipatiwa asilimia nne ya mikopo inayotolewa kwa wanawake wa halmashauri ya wilaya hiyo, itawasaidia kujikwamua kiuchumi na wataacha kujihusisha na shughuli za ukeketaji.

Alisema watasimama kidete kupinga vitendo hivyo kwa kuwa matukio ya ukeketaji yanazidi kushika kasi na kusababisha mkoa huo kuwa kinara wa matukio ya kikatili.

"Awali mikoa iliyokuwa kinara kwa matukio ya ukeketaji ilikuwa ni Mara, Dodoma na Singida, kwa sasa mikoa hiyo imeachana na vitendo vya ukatili wakijinsia, tumebakia sisi Manyara pekee, hivyo tunapaswa kubadilika na kuachana na mila potofu kwa kuwa zimepitwa na wakati," alisema Umbullah.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Mkoa wa Manyara, Anna Fissoo, aliwataka wanawake kuwa mstari wa mbele kukemea vitendo hivyo, kwa kuwa ni jukumu lao kuliko kuwategemea wanaume. "Hizi mila potofu zimepitwa na wakati kwa kuwa tendo la ndoa ni paradiso iliyowekwa mwilini, lakini mwanamke akikeketwa hapati raha wakati wa faragha na mume wake kwa sababu tayari ana kovu baada ya kuondolewa kwa kiungo chake," alisema Fissoo. Licha ya kuzungumza hayo, alisema wakati wa kujifungua mwanamke aliyekeketwa anatokwa damu nyingi na kuchanika kwa kuwa amekeketwa.

Mwanamke wa kijiji cha Wareta, Helena Ruben, alisema kwa sasa baadhi ya wanawake wanawaita mangariba hao usiku ili kuwakekete watoto wenye umri wa miezi miwili mpaka mitatu, wakati wanaume zao wakiwa wamelala.

Amewataka wauguzi wa kitengo cha afya kuwakagua watoto wakati wanapopelekwa kliniki ili kuwabaini watoto waliokeketwa na wazazi wao wachukuliwe hatua za kisheria.

Mmoja kati ya ngariba wa eneo hilo, Tatu Hassan, alisema kwa kiwango kikubwa wameachana na vitendo hivyo kwa kuwa serikali inapiga vita matukio hayo na baadhi yao wameanza kujishughulisha na kazi nyingine za kujiingizia kipato.

"Mimi na wenzangu tunafanya ujasiriamali, ikiwamo kuuza maandazi, lakini bado wamebaki wachache wanaofanya vitendo vya ukeketaji, sisi tulipewa elimu ya madhara ya kazi ya ungariba," alisema.



Mwenyekiti wa Mtaa wa Tanesco, Mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, Justin Abraham (kulia), akizungumza kwenye kikao cha maendeleo cha kata ya Endiamtu, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# DC ajifagilia kupunguza uhaba vyumba madarasa

**Na Jaliwason Jasson,** HANAN'G

MKUU wa Wilaya ya Hanan'g, Joseph Mkirikiti, amesema wilaya hiyo imepunguza uhaba wa vyumba vya madarasa ukilinganisha na mwaka 2018/2019.

Hayo aliyasema mwishoni mwa wiki, wakati wa mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Hanan'g.

Mkirikiti alisema kwa sasa wilaya hiyo, ina upungufu wa vyumba vya madarasa 15, ukilinganisha na mwaka 2018/2019 walikuwa na upungufu wa madarasa 75.

Aidha, alisema awali kulikuwa na uhaba wa vyumba vya madarasa kwa sababu wananchi husussani wanaoishi mjini hawakuwa wanachangia shughuli za maendeleo katika jamii.

Aidha, alisema kwa sasa hali ya siasa wilayani humo ni nzuri na wananchi wote wanachangia shughuli za kimaendeleo bila kujali itikadi za kisiasa, ndio sababu wamefanikiwa kupunguza tatizo la upungufu wa vyumba vya madarasa.

"Ndugu zangu mwanzo baadhi ya kata za mjini hazikuwa zinachangia maendeleo, lakini kwa kipindi hiki ndio maeneo yanayoongoza mfano kata za Ganana na Katesh," alisema Mkirikiti.

Hata hivyo, alisema kwa sasa wananchi wa vijijini wanapigania maendeleo na mambo ya siasa kama ilivyokuwa mwanzo. "Mfano mzuri nilikuwa nazungumza na Mwenyekiti wa Chadema wa wilaya hii pamoja na baadhi ya madiwani wa chama hicho wameniambia hali ya kisiasa ipo vizuri Hanan'g na wataunga mkono juhudi za serikali," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Hanan'g, George Bajuta, amewataka madiwani hao kuendeleza ajenda ya elimu, ili kuongeza ufaulu kwenye shule zao.

Bajuta alisema katika kata yake ameweka utaratibu wa kutoa zawadi ya Sh. 10,000 kwa walimu wanaofaulisha masomo kwa ngazi ya daraja la kwanza.

Katika kikao hicho, madiwani waliochangia hoja ya elimu walionyesha kuridhishwa na usimamizi wa elimu ya msingi na kumpongeza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, kwa usimamizi bora uliochangia matokeo chanya ya ufaulu.

# Kamishna Zimamoto atoa somo kwa askari

**Na Allan Isack,** BABATI

KAMISHNA Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, John Masunga, amewataka askari wa jeshi hilo kutoa elimu kwa umma ili kuzuia na kupunguza majanga ya moto.

Rai hiyo ameitoa kutokana na kuongezeka kwa majanga ya moto katika jamii na kusababisha madhara makubwa na hasara.

Masunga aliyasema hayo Mjini Babati mkoani Manyara, wakati wa ziara yake ya kikazi kutembelea ofisi za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji za Kanda ya Kaskazini.

Alisema kuna haja ya wananchi kupewa elimu ya kujikinga na majanga ya moto kwa kuwa kuna uwezekano mkubwa wa ajali hizo, kutokea, lakini bado uwezekano wa kuzuia ni mdogo kwa kuwa jamii haina elimu ya kujikinga na majanga hayo.

Aliagiza shule kuanzisha vilabu vya marafiki wa zimamoto na vilabu hivyo, viimarishwe sambamba na wanafunzi kupewa elimu hiyo na wao waende kutoa elimu kwa wazazi na walezi kuhusu namna ya kukabiliana na majanga ya moto.

"Pamoja na kutoa elimu hiyo, maofisa na askari wanapaswa kuongeza bidii kwenye kazi za uzimaji moto, kwa kuzingatia nidhamu ya utekelezaji wa majukumu ya jeshi," alisema Masunga.

Hata hivyo, ametaka maofisa na askari wa jeshi hilo, kujiepusha na vitendo vya rushwa kwa kuwa wanachafua taswira ya jeshi katika jamii inayowazunguka.

"Tatizo lililopo ni la vitendea kazi tunafahamu hilo, bado serikali inaendelea kulifanyia kazi...naomba msikatishwe tamaa kutokana na vikwazo mnavyokutana navyo, ongezeni bidii ya kuwatumikia wananchi," alisema. Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, aliwapongeza askari wa Zimamoto kwa kutimiza wajibu wao ipasavyo, japokuwa wanakabiliwa na upungufu wa vifaa.

Mnyeti alisema askari hao wamekuwa wepesi wa kushughulia majanga mbalimbali wakati yanapotokea kwenye eneo hilo.

Kamanda wa Zimamoto na Uokoaji wa Mkoa wa Manyara, Julishael Mfinanga, alisema wanafanya shughuli zao katika wilaya tano za Babati, Mbulu, Kiteto, Hanang' na Simanjiro.

# Uvamizi shoroba chanzo wanyama kuvamia mazao

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MAOFISA wanyamapori wamesema mwendelezo wa uharibifu wa mali na mazao ya wakulima katika maeneo mbalimbali nchini, kuvamiwa na kushambuliwa na tembo kunatokana na wananchi kujenga makazi yao kwenye mapito ya wanyama maarufu kama shoroba. Kamishna Mwandamizi wa Shirika la Hifadhi la Taifa (Tanapa), Kanda ya Kaskazini, Herman Batio, alisema maeneo mengi yaliyokuwa mapito ya wanyama hao hapa nchini yamevamiwa, na ndio maana wanyama hao wanarejea katika mapito yao kutafuta malisho. Batio alikuwa akizungumza jana, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanyamapori Duniani ambayo yalifanyika katika Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka, Wilaya ya Moshi. Alisema katika maeneo ambayo tayari wananchi wamejenga makazi ya kudumu ni vigumu kuwazuia wanyama hao kupita kwenye njia hizo.

"Unapojenga katika mapito ya wanyama hasa tembo, unasababisha madhara ya ulemavu na vifo kwa watu na hususani kwenye maeneo ambayo wanyama hao wanapitia," alisema.

Miongoni mwa mapito ya wanyama (shoroba), yaliyozibwa mpaka sasa na kuathiri shughuli za uhifadhi ni Ndarakwai na Meru na maeneo mengine ya shamba la TBL lililopo Enduiment mkoani Kilimanjaro. Ndarakwai iliyopo kati ya Mkoa wa Kilimanjaro na Meru ya Mkoa wa Arusha, hakuna mjumuiko kwa sababu ya kuzibwa kwa shoroba za wanyama, vivyo hivyo eneo la Enduiment nako hakuna mjumuiko.

Shoroba nyingine inayokabiliwa na tatizo hilo ni ile iliyopo kati ya Kilimanjaro na Tsavo West, wakati shoroba pekee ya wanyama ambayo ipo na inapitika kwa sasa ni ya Kitendeni iliyopo kati ya Kilimanjaro na Amboseli ya nchini Kenya. Awali, Mratibu wa Malihai Klabu ngazi ya Taifa, Benjamin Kijika, alisema uvamizi huo pia umesababisha uharibifu wa mazingira kwenye makazi ya watu na vyanzo vya maji.

Ofisa Usafi na Mazingira wa Wilaya ya Moshi, Peter Tungu, akizungumza katika maadhimisho hayo, alisema kwa sasa serikali kwa kushirikiana na Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori (Mweka), wameanza juhudi za kupanda miti katika maeneo yanayozunguka vijiji vinavyopakana na Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro (Kinapa) ili kuhifadhi uoto wa asili ambao ulikuwa hatarini kutoweka.

# TFS yarudisha uoto wa asili Same

**Na Ashton Balaigwa,** SAME

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Kanda ya Kaskazini imeanza kurudisha uoto wa asili katika Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro, baada ya kuanza kupanda miti 4,000 ya asili na matunda katika kila kata iliyopo wilayani humo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa upandaji wa miti hiyo katika Kata ya Kihurio wilayani hapa, Meneja wa Wakala huo, Edward Shilogile, alisema kupitia kampeni ya 'Tokomeza Ukame Same' wameanza kupanda miti katika maeneo yote yanayozunguka kata hiyo kwa kutumia wanafunzi wa shule ya msingi na sekondari katika eneo hilo.

"Hii miti itapandwa katika maeneo yote ya taasisi za serikali ikiwamo shule na zahanati pamoja na pembezoni mwa barabara na nyumba zilizopo katika kata hiyo na kila mwananchi anawajibu wa kuitunza," alisema.

Shilogile alisema wataifuatilia kwa karibu ili miti hiyo itunzwe na kuleta mafanikio kama ilivyokusudiwa kwa ajili ya kurudisha uoto huo wa asili ambao ulikuwa katika tishio la kutoweka.

Kwa upande wake, Balozi wa Kampeni ya Utunzaji wa Maliasili nchini, Nangasu Wallema, alisema wameamua kuwatumia wanafunzi katika kampeni hiyo ili kuwajenga tangu wakiwa wadogo ili kuona umuhimu wa kutunza na kuhifadhi mazingira sambamba na kufikisha ujumbe huo kwa wazazi wao.

Alisema, kampeni hiyo imelenga kupanda miti 4,000 kwa kuanzia kata zote 15 zilizopo katika Jimbo la Same Mashariki na baadaye kuhamia katika Jimbo la Same Magharibi na kila kata itapandwa kiwango hicho cha miti.

Naye Diwani wa Kata ya Kihurio, Mariane Mariane (CCM), alisema athari za kuharibika kwa mazingira katika kata hizo zimeanza kujitokeza na kupitia kampeni hiyo ya kupanda miti itasaidia kuzuia uharibifu wa mazingira.

Alisema kupitia wenyeviti wa serikali za vijiji vyote vilivyopo katika kata hiyo wamekubaliana mifugo yote inayozurura ifungwe katika eneo moja na itakayobainika kuendelea kuwapo mitaani wahusika watachukuliwa hatua kali.



Balozi wa kampeni ya utunzaji wa Maliasili nchini, Nangasu Wallema (aliyepiga magoti kulia), akipanda mti wakati wa kampeni ya tokomeza ukame katika Kijiji cha Uzambara, Kata ya Kihurio, wilayani Same, mkoani Kilimanjaro juzi. Kushoto (mwenye kofia), ni Meneja wa Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), Kanda ya Kaskazini, Edward Shilogile akiwa pamoja na wananchi wa kijiji hicho. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# Wananchi Siha waanza kupata mawasiliano

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

HATIMAYE wananchi wa Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, wameanza kupunguza machungu ya tatizo la mawasiliano duni ya simu, baada ya serikali kuliamuru Shirika la Mawasiliano ya Simu Tanzania (TTCL), kumaliza kero hiyo kwa kuongeza nguvu ya mnara katika Kijiji cha Manio, Kata ya Kashashi.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Mhandisi Atashasta Nditiye, alisema kabla ya kuchukua uamuzi huo, hali ya mawasiliano ya simu katika wilaya hiyo ilikuwa hairidhishi kwa asilimia 70.

Mhandisi Nditiye alikuwa akizungumza jana wilayani hapa, wakati alipokwenda kuzindua mpango huo.

"Asilimia 95 ya wananchi walioko vijijini na mijini kwa sasa wanapata huduma za mawasiliano, lakini kwa Wilaya ya Siha mambo yalikuwa ovyo na walikuwa hawapati mawasiliano ya uhakika kwa asilimia 70, sasa mambo yako sawa," alisema.

Kwa mujibu wa Mhandisi Nditiye, mnara wa mawasilino wa TTCL uliojengwa katika Kijiji cha Manio, Kata ya Kashashi, umeigharimu serikali zaidi ya Sh. milioni 450.

Alisema bado juhudi zinaendelea kuhakikisha maeneo yote ambayo wananchi wanapata shida ya mawasiliano hususani maeneo ya mipakani ambako baadhi ya wananchi simu zao zinasoma mawasiliano ya minara ya nchi jirani.

Alisisitiza kuwa ili kuepuka adha hiyo, katika maeneo hayo patajengwa minara ya mawasiliano ili kuwezesha wananchi wa vijijini kupata huduma za mawasiliano na miamala ya fedha kupitia simu za mikononi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTC), Waziri Kindamba, alisema kwa sasa shirika hilo limeanzisha kampeni ya kununua vocha kwa muamala wa TTC Pesa, taasisi za kibenki na mawakala wa fedha ili kuwezesha wananchi kupata huduma kwa urahisi.

Kutokana na maboresho hayo, baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Manio akiwamo Zaina Mmari, alisema kuanzishwa kwa minara ya mawasiliano ya TTCL katika wilaya hiyo itasaidia wananchi kupatikana huduma za mawasiliano na wameiomba serikali kuboresha huduma za mtandao huo ili kupata huduma mbalimbali kirahisi maeneo ya vijijini.

Nipashe
# TESA
Jumanne Machi 3, 2020
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 18

**Taka kielektroniki, plastiki huenda zi-kaangamiza dunia**



Ukurasa 19

Haya ndiyo yanayowaelemea wanafunzi wenye ulemavu



Ukurasa 15

## Wanawake wawe wafuatiliaji wakuu utekelezaji lengo la 5



# Kipigo kwa waliochoma mabweni chaleta 'neema'

Ukurasa 16

## ELIMU YA KIPOLISI
### NA TAMIMU ADAM – JESHI LA POLIS

# MAFUNZO PAMOJA KUIMARISHA USHIRIKIANO SAPRPCCO

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Simon Sirro, hivi karibuni amesema Tanzania inanufaika kiulinzi na usalama kutokana na kuwa mjumbe wa Shirikisho la Wakuu wa Polisi wa nchi za ukanda wa Kusini mwa Afrika (SARPCCO).

IGP Sirro anayasema hayo wakati akiongea na vyombo vya habari mara baada ya kikao na Mwenyekiti wa Shirikisho hilo, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Polisi Zimbabwe, TG Matanga ambaye alikuwa nchini kwa ziara maalum.

Anaongeza kuwa kutokana na Tanzania kuwa mwanachama wa shirikisho la wakuu wa polisi kwa nchi zilizopo kusini mwa Afrika, imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuzuia na kudhibiti makosa yanayovuka mipaka yakiwamo makosa ya usafirishaji haramu wa binadamu, wizi wa magari pamoja na dawa za kulevya.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Shirikisho ambaye pia ni Mkuu wa Jeshi la Polisi la nchini Zimbabwe, Kamishna Jenerali TG Matanga, alisema alikuwa Tanzania kwa ziara maalum ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa maazimio ya INTERPOL pamoja na maazimio ya SARPCCO.

Kamishna Matanga akizungumzia operesheni za pamoja zinazofanyika kwa kushirikiana baina ya nchi mbili, operesheni za kikanda pamoja na kimataifa kama operesheni usalama zimeonyesha mafanikio makubwa baina ya nchi wanachama katika uhalifu wa ndani na ule unaovuka mipaka , hivyo ameitaka Tanzania kuendelea kuwa mstali wa mbele katika operesheni mbalimbali zinazoratibiwa na shirikisho hilo.

Akaongeza kuwa, ili kuimarisha shirikisho hilo ni muhimu kuwekea msisitizo eneo la mafunzo ya pamoja ili kupambana na wahalifu na uhalifu unaovuka mipaka.



Kamanda Sirro (kushoto) na Matanga, wakati ofisa huyo wa polisi alipozuru Tanzania. **PICHA: JESHI LA POLISI.**



Kamishna wa Operesheni na Mafunzo ya Jeshi la Polisi, CP Liberatus Sabas, akisalimiana na mwakilishi wa kampuni ya utengenezaji wa pikipiki baada ya kulikabidhi jeshi hilo pikipiki 10 kwa ajili ya operesheni mbalimbali. **PICHA: JESHI LA POLISI.**

## JIELIMISHE

# Unawajua wanaoongoza kuzima mtandao duniani?

NI simulizi kutoka chumba cha ofisi iliyopo ghorofa ya juu ambayo inamwezesha Markos Lemma, kuuona vizuri mji wa Addis Ababa.

Huyo ni mwanzilishi wa teknolojia ya IceAddis. Mazingira yake ya kazi huwa yana shughuli nyingi kutokana na wajasiriamali wa kahawa wenye ndoto kubwa wanaofurika katika eneo hilo.

Lakini, intaneti inapofungwa, kila kitu kinakwama. Kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Kutetea Haki Mtandaoni, Access Now, mwaka jana huduma hizo za mtandao zilikuwa zinafungwa makusudi mara 200 katika nchi 33 tofauti.

"Msongamano wa magari hapa unaisha. Hakuna mtu anayekuja, au wakija hawakai sana kwa sababu kama hakuna mtandao, hawana kitu cha kufanya hapa," Lemma anasema.

"Tulikuwa na programu ya maendeleo ambayo mkataba wake ulifutwa kwa sababu haukukamilika kwa wakati, mtandao ulikuwa unazimika kila wakati,"anaeleza.

Anaongeza kuwa wateja wao wa nje ya nchi walidhani kuwa hawako makini katika biashara zao, lakini ukweli ni kwamba hawakuwa na cha kufanya. "

Ni kawaida ya waendesha pikipiki kusubiri katika maeneo hayo kwa ajili ya kusambaza vyakula.

Hata hivyo , inaelezwa ujasiriamali huo wa mtandao wa vyakula hauwezekani pasipo uhai wa mtandao unaitumia program Fulani.

Lemma anaendelea na simulizi: "Kufungwa kwa mtandao kunaathiri biashara zao moja kwa moja na watu wa hapa".

Tatizo la kufungwa tovuti kwa nchini Ethiopia, kitaalamu inaelezwa sio lao peke yao na athari zake haziishii kwenye uchumi pekee.

Unarejewa utafiti kwamba kuzimwa kwa mitandao, kunaathiri mamilioni ya watu duniani, kila moja kwa nafasi yake ilivyo.

Inaelezwa kuwa wenye mamlaka serikalini ndiyo wenye uwezo wa kutawala mifumo ya mtandao, iwe kwa baadhi ya maeneo au namna wanavyotaka.

Tayari wanaohusika na haki za binadamu wameanza kulitolea macho katika tafsiri ya umma kunyimwa haki zao za kibinadamu

Kuna taarifa mpya za utafiti wa wanahabari, zinazoonyesha kuwa hali hiyo huzidi katika mazingira ya msuguano katika baadhi ya maeneo duniani .

Inarejewa takwimu zinazonyesha kuwa mwaka 2019, intaneti ilizimwa wakati wa matukio ya maandamano katika baadhi ya nchi nyingi.

Wakosoaji wa kasoro hizo wamejitokeza wakisema, kuzimwa kwa taarifa mtandaoni kunaathiri shughuli nyingi muhimu.

Umoja wa Mataifa (UN), unasema kuwa upatikanaji wa intaneti ni Haki ya Binadamu na ni miongoni mwa malengo ya maendeleo endelevu.

Hata hivyo, licha ya kukubaliana na wazo hilo inaelezwa kuwa mwaka 2019, Waziri Mkuu wa Ethiopia Abiy Ahmed, alitangaza kutokubaliana na utekelezaji wake.

Mdau wa intaneti, Lemma bado ana msisitizo wake, akitamka: "Serikali haioni kama intaneti ni muhimu? Wanadhani intaneti ni kwa ajili ya mitandao ya kijamii na hawaoni kuwa ina thamani katika uchumi na inausaidia?"

Kimataifa, India inatajwa kuongoza uzimaji mtandao,kwa mujibu wa taarifa ya mwaka 2019, ikiwa na rekodi ya kuzima mtandao wa simu za mkononi mara 21 nchini humo ambayo inatajwa kitaalamu ni sawa na asilimia 67.

Katika matukio ya maandamano yaliyotokea nchini Sudan na Iraki, yaliendana na kuzimwa mtandao.

***Kwa mujibu wa BBC**




Markos Lema, mmiliki wa mfumo wa intaneti, jijini Addis Ababa, Ethiopia. **PICHA: MTANDAO.**

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

SIKU YA WANAWAKE

# Wanawake wawe wafuatiliaji wakuu utekelezaji lengo la 5



Lengo la 5 linahimiza usawa wa kijinsia ili kutimiza azma ya kuondoa njaa ni lazima sheria , mila na taratibu zinazokandamiza wanawake ambao ni wakulima wakuu nchini kumiliki ardhi na mazao wanayozalisha zirekebishwe. **PICHA: MTANDAO.**

KUANZIA mwaka 2015 wanachama wa Umoja wa Mataifa (UN) wanatekeleza malengo ya maendeleo endelevu (SDGs) 17 ambayo ni mwendelezo wa malengo ya maendeleo ya milenia au MDGs yaliyoasisiwa mwaka 2000 yakilenga kupunguza umaskini kwa nusu ifikapo mwaka 2015. Hata hivyo , jitihada zaidi zinahitajika ndiyo maana sasa kuna SDGs ambazo zinaendeleza jukumu hilo hadi mwaka 2030.

Dunia inapoelekea kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, Machi 8, ni vyema kuangalia baadhi ya malengo yanayomhusu mwanamke moja kwa moja . La kwanza ni kuondoa umaskini, la pili ni kutokomeza njaa, tatu afya bora, nne ni elimu bora , la tano ni usawa wa kijinsia, sita maji safi , nishati bora , jingine ni kazi za staha na zenye kipato , 13 mabadiliko ya tabia nchi, usalama wa maisha ya viumbe chini maji na usalama wa ardhi watu watu wanapoishi.

Tanzania imejikita kwenye kusimamia na kufanikisha lengo namba tano ambalo ni usawa wa kijinsia. Ikiamini kuwa kupatikana kwa usawa huo ndiyo utakuwa msingi wa malengo mengine yote 17.

Taifa linaamini kuwa kuanzia kazi ya kuondoa umaskini ambalo ni lengo namba moja, likifuatiwa na kutokomeza njaa na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ambalo ni lengo namba 13 hadi la 17 la ushirikiano wa kimataifa yatafanikiwa iwapo tu kuna usawa wa kijinsia.

Malengo haya ambayo yanatelekezwa na wanachama wa UN kuanzia 2015 hadi 2030 yanasisitiza ushirikishwaji wananchi kwenye kuyatekeleza na kuyafuatilia ili kila mmoja anufaike na ahadi za serikali na viongozi.

Kwa Tanzania wananchi wanatakiwa kuyafahamu na kuhoji serikali imeahidi nini kwenye usawa wa kijinsia na nini ambacho UN imekielezwa na kipi ambacho kinafuatwa.

Tatizo la unyanyasaji wa kijinsia nchini ni kubwa kadhalika ukosefu wa usawa wa kijinsia unatishia ustawi wa wanawake wengi. Mimba za ututoni zipo kwa wingi, kadhalika ndoa za utotoni, kutelekeza wanawake, rushwa ya ngono ofisi, kulawiti watoto na mauaji ya wanawake wazee ni sehemu tu ya ukatili huo.

Mambo mengine yanayoonyesha kuwa kiwango cha ukatili dhidi ya wanawake (VAW) kipo juu ni maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU), wanawake wengi wameambukizwa na hasa mabinti wenye umri wa kuanzia miaka 14 hadi 25, kwa mujibu wa Taarifa ya Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi ya mwaka 2019.

> Serikali inaagiza kila halmashauri na majiji yote kuchukua asilimia tano ya mapato ya ndani ili kutoa mikopo kwa vijana, watu wenye ulemavu na wanawake.

Binti mwenye miaka 14 kuambukizwa VVU inaamanisha ubakaji na ukatili dhidi ya watoto na wanawake. Hata maambukizi mapya na mengi yamewagusa wanawake na hilo linamaanisha kuwa kuna idadi kubwa inaoishi na maradhi. Hivyo kuwa na usawa wa kijinsia kutasaidia kuondoa changamoto hilo kubwa.

Wataalamu wa dimografia wanaamini kuwa kuwekeza dola moja kwa binti serikali, jamii na familia wanavuna mara tano kwa mtaji huo usawa wa kijinsia si kwamba unawanufaisha wanawake pekee yao kwa ujumla ni taifa zima.

### VIJANA WANAWAKE

Katika kutekeleza lengo la tano la usawa wa kijinsia kuliwezesha kuwa na mafanikio ni lazima vijana washirikishwe kwani ndiyo wahusika wakuu kwenye utekelezaji. Lakini , vijana wanawake wanastahili kupewa kipaumbele cha kipekee.

Mathalani, serikali inaagiza kila halmashauri na majiji yote kuchukua asilimia tano ya mapato ya ndani ili kutoa mikopo kwa vijana, watu wenye ulemavu na wanawake.

Kipaumbele cha kipekee kinahitajika kuwalenga na kuangalia iwapo wanawake vijana wanafahamu kuhusu mikopo hiyo hasa vijijini na kama wanafahamu wanaipata? Je wanaelewa kuhusu kuunda vikundi vya kibiashara na kuandika andiko la kibiashara ili kupata fedha hizo?

Vijana wanawake wa vijijini wananufaika kama walivyo wa mijini kwa kufunzwa kuhusu namna ya kuanzisha biashara zenye tija? Biashara endelevu na zinazofanywa kwa ubunifu na ujasiriamali badala ya kuigana na kufanya biashara za aina moja mtaa mzima?

Utekelezaji wa malengo ya kuwawezesha wanawake kiuchumi, kielimu, kiuongozi na kufanya maamuzi, kiutaalamu ukiwamo wa kutumia teknolojia ya mawasiliano ni muhimu kufanikisha malengo mengine yote.

Kama ambavyo Tanzania imechagua lengo la usawa wa kijinsia linawagusa wote ni suala mtambuka. Kwa hiyo hakuna afya bora, tena umaskini hautaondoka, wala njaa haitakwisha na matumizi ya nishati mbadala hayatafikiwa iwapo hakuna usawa wa kijinsia tena unaowashirikisha wanawake vijana.

Malengo yote 16 yatafanikiwa iwapo lengo namba tano litatimizwa. Kwa mfano lengo namba sita la kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na kulinda rasilimali maji linahusika na usawa wa kijinsia moja kwa moja kwani wanawake ndiyo watafutaji wakuu wa maji .

Mathalani, mkoani Mwanza kwa miaka mingi wanawake wanashambuliwa na fisi, chui na hata simba wanapoamka usiku wa manane kufuatilia maji kwenye madimbwi na malambo jirani ambayo pia hutumiwa na wanyama pori.

Ni lazima pia usawa wa kijinsia upatikane kwenye kutekeleza lengo hili kwa kinamama kuwashirikisha zaidi kwenye mikutano ya rasilimali na kuwaelimisha kuhusu sharia za maji na 'water right' za vijiji na kuwafanya kuwa wasimamizi wa maji kwani ndiyo waathirika wakuu wa shida ya maji.

### TABIA NCHI

Hili ni lengo la maendeleo endelevu namba 13 ambalo linahimiza ulinzi wa dunia na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Ulinzi wa mapafu ya dunia au misitu ni kipaumbele. Ni kwa sababu uwepo wa kijani unasaidia kupunguza joto linaloyeyusha tabaka la utandao wa ozone.

Takwimu za Wakala wa Uhifadhi na Huduma za Misitu (TFS) zinaeleza kuwa wastani wa hekari 400,000 za misitu huteketea kila mwaka kwa ajili ya kilimo , mifugo, ujenzi wa makazi na ofisi, mbao na nishati. Lakini pia mkoa wa Dar es Salaam unatajwa kuongoza kwa kutumia kiwango cha juu cha mkaa nchini ikichoma wastani wa magunia 500,000 kila mwezi.

Misitu ikiharibiwa ina athari kubwa kwa mabadiliko ya tabia nchi kwani ndiyo inayotoa oksjeni nyingi na kutumia hewa ukaa kuzalisha chakula hivyo kuwa mhusika mkuu wa kupunguza joto na kishindo cha tabia nchi. Kwa miongo mingi ulinzi wa misitu ni jukumu linalofanywa na kinababa ambao wakati wote wameihujumu.

Ndiyo wanaokata na kuuza magogo, kuichoma kwa kazi za kilimo na ufugaji wa wanyama na nyuki na kwa ujumla kuvamia misitu na kutafuta utajiri. Lakini, jitihada hizo zimerudisha ugumu wa maisha kwa wanawake ambao ndiyo wapishi wa kila familia wanaosumbukia nishati hasa mkaa na kuni kila siku.

ELIMU

NA NEBART MSOKWA, MBEYA

# Kipigo kwa waliochoma mabweni chaleta 'neema'

• Shule yavuna milioni 80, ni nidhamu ya hali ya juu



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo (mwenye suti ya bluu), akitoa maelekezo kwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, pamoja na viongozi wa Wilaya ya Chunya wakati alipotembelea Sekondari ya Kiwanja kukagua ujenzi wa mabweni yaliyoteketezwa. **PICHA ZOTE: NEBART MSOKWA.**

OKTOBA mosi mwaka jana, mabweni ya Sekondari ya Kiwanja iliyoko Chunya mkoani Mbeya yalichomwa na baadhi ya wanafunzi kwa maelezo kuwa walimu waliwapokonya simu walizokuwa wanazitumia mabwenini kwa kificho licha ya kwamba pia ni kinyume cha sharia.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Shule, Elly Mnyarape, wanafunzi wahusika walikuwa wa kidato cha nne, tano na cha sita walichoma mabweni ili kulipiza kisasi baada ya walimu wao kupitisha msako na kukamata simu walizokuwa wanazitumia japo taratibu za shule zilikuwa zinawakataza.

Mwalimu Mnyarape anasema baada ya kuteketeza mabweni mawili pamoja na mali zilizokuwemo, walikuwa wanaendelea na harakati za kuchoma mabweni mengine kabla ya uongozi kuwashtukia.Walinaswa wakati wakiwasha moto kwenye bweni la tatu ambao ulidhibitiwa licha ya kuchoma vitanda vitatu.

"Baada ya tukio hilo wanafunzi watano ambao wanadaiwa kushiriki moja kwa moja walikamatwa na Jeshi la Polisi na kuwekwa mahabusu kusubiri kuchukuliwa hatua za kisheria." Aidha Mkuu wa Mkoa Albert Chalamila, alitoa maelekezo ya kulipa faini kuanzia Sh. 250,000, 500,000 na 1,000,000 baada ya kutembelea shule na kuwacharaza viboko watuhumiwa.

> Nakupongeza sana Chalamila kwa kuwatandika wanafunzi wale na kama kuna sehemu tulikosea basi ni ile sheria, inabidi tuirekebishe wawe wanatandikwa, hata Ulaya wanatandikwa vizuri kabisa.

Pia maonyo makali yalitolewa kuwa watakaojifanya kukimbia na kuhamia shule za binafsi hawatapewa nafasi ya kufanya mitihani ya kitaifa na huo utakuwa mwisho wa maisha ya elimu zao labda wahamie nje ya Tanzania.

Hata hivyo, yaliyopita si ndwele kwani baada ya kupewa adhabu mambo yamebadilika na sasa Kiwanja iko kivingine.

### MATOKEO

Kwa mujibu wa taarifa ya Mkuu wa Shule Mwalimu Mnyarape baada ya kutekelezwa kwa adhabu iliyotolewa na Mkuu wa Mkoa pamoja na maelekezo mbalimbali waliyoyapata kutoka serikalini wameshuhudia matokeo chanya shuleni hapo.

Anasema wanafunzi waliokuwa wametimuliwa, walirejea shuleni hapo wakiwa wameshalipa kiwango cha fedha walichoagizwa na Chalamila ambapo shule hiyo ilipata Sh. milioni 82 kutoka na faini hizo.

Anasema kabla wanafunzi hao hawajarejea shuleni, baadhi ya wadau walijitokeza kwenye harambee iliyokuwa imeitishwa na Mkuu wa Wilaya ya Chunya Maryprisca Mahundi na kutoa michango ya vifaa mbalimbali vikiwemo vya ujenzi na vya malazi.





Mwonekano wa bweni jipya la wanafunzi lenye ambalo linaendelea kujengwa kwa kutumia fedha walizolipa na wanafunzi kama adhabu baada ya kuchoma mabweni mawili.

Anasema baada ya michango hiyo, walikarabati mabweni mawili yaliyokuwa yameungua na yakarejea katika hali yake ya kawaida na kwamba tayari wanafunzi wameshaanza kuyatumia.

Mnyarape anasema waliamua kuzitumia fedha zilizolipwa na wanafunzi hao kujenga bweni jipya ambalo limepewa jina la Chalamila Dormitory na kwamba litagharimu Sh. milioni 70 mpaka kukamilika kwake.

"Tunaendeleana ujenzi wa bweni hilo ambalo tumelipa jina la Chalamila, litakuwa na uwezo wa kuhudumia wanafunzi 124 kwa wakati mmoja na mpaka sasa tumeshatumia milioni 66 na tunaendelea kumalizia maeneo machache yaliyobakia," anasema Mnyarape.

Anasema mbali na matokeo hayo pia nidhamu ya wanafunzi wa shule hiyo imeongezeka kutokana na wengi kuogopa kukumbwa na adhabu kama iliyowakuta wenzao.

### KUHUSU BAKORA

Tukirejea kwenye janga hilo, ikumbukwe kuwa siku tatu baada ya kutokea mkasa huo, Oktoba 3, 2019, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Albert Chalamila, alifanya ziara katika shule hiyo kukagua uharibifu pamoja na kujadiliana na viongozi wakiwamo walimu namna ya kuyarejesha mabweni hayo katika hali ya kawaida.

Anapoingia shuleni hapo na kukagua mabweni hayo baada ya kupata maelezo ya uongozi wa shule hiyo pamoja na wa Wilaya ya Chunya kuhusu namna wanafunzi hao walivyoteketeza mabweni 'kihuni' naye hakufanya ajizi akaanza kuwaadhibu.

Alianza na wanafunzi 14 ambao waliokutwa na simu kwa kuwacharaza bakora tatu kila mmoja na akaagiza watano waliokuwa wanashikiliwa na polisi wafikishwe mahakamani ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

Mbali na kuchapwa pia aliagiza Bodi ya Shule hiyo kukutana mara moja na kuwataka wazazi wa wanafunzi waliokutwa na simu walipe kila mmoja Sh. 1,000,000 kwa ajili ya kukarabati mabweni hayo.

"Mzazi ambaye atakaidi, mwanae afikishwe polisi na hata mahakamani ili sheria ichukue mkondo. Hatuwezi kuvumilia nidhamu mbovu ya wanafunzi namna hii, hatujui baada ya kumaliza kuchoma mabweni haya walikuwa wanakwenda kuchoma nini," anasema Chalamila.

Tukio hilo la Chalamila kuwacharaza bakora wanafunzi hao, lilizua gumzo ndani na nje ya nchi kufuatia video iliyosambaa kwenye mitandao ya kijamii ambako kila mmoja alikuwa anazungumza lake.

Baadhi wachangiaji walimuunga mkono Chalamila kutokana na kukerwa na wanafunzi hao na wengine walikuwa wanamkosoa wakidai kuwa alikuwa amekiuka mwongozo wa elimu unaoeleza utaratibu wa adhabu ya viboko shuleni.

Wakosoaji wake ambao wengi walikuwa ni wanaharakati wa kutetea haki za binadamu, walikuwa wanamshambulia wakidai hakustahili kutoa adhabu hiyo na badala yake ilipaswa itolewe na mkuu wa shule ama na mwalimu wa nidhamu au mwingine kwa idhini ya mkuu huyo wa shule.

Hatahivyo, Chalamila aliendelea na msimamo wake kuwa kitendo alichokifanya alikuwa sahihi kwa maelezo kuwa ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa na msimamizi mkuu wa shughuli zote za maendeleo katika mkoa huo.

"Najua kuwa mwongozo unataka Mkuu wa Shule ndiye angewaadhibu na wanaharakati wamesimamia hapo, lakini mjue kwamba mkuu huyo wa shule bosi wake ni mimi, kama anatakiwa kuwachapa yeye basi mimi natakiwa kuwachapa sana,"anasisitiza Chalamila.

### KUTIMULIWA SHULE

Ilipofika Oktoba 4 ikiwa ni siku moja baada ya kuwashushia bakora wanafunzi hao 14, Chalamila alipigilia msumari wa moto kwa kuwatimua wanafunzi wote 392 wa kidato cha tano na sita.

Kiongozi huyo aliwafukuza wanafunzi hao na kuamuru warejee shuleni hapa baada ya wiki mbili kwa maelezo kuwa baada ya baadhi yao kuchoma mabweni waliyokuwa wanatumia, walikuwa hawana mahali pengine mbadala pa kulala.

"Kama mnawashwa kuchoma nyumba, nendeni mkachome nyumba za wazazi wenu kwa sababu huu ni utovu wa nidhamu, sasa walimu wote mnaofundisha kidato cha tano na sita mnakwenda likizo kidogo ya wiki mbili," anasema Chalamila

Mbali na kuamuru wanafunzi hao kurejea nyumbani, aliaagiza wengine 366 ambao hawakukutwa na simu kurejea shuleni hapo kila mmoja na Sh. 200,000 na wenzao 26 waliokamatwa nazo warejee na Sh.500,000 kwa ajili ya ukarabati wa mabweni.

Aliwataka wanafunzi hao kurejea shuleni Oktoba 18 kila mmoja akiwa amelipa fedha hizo kwenye akaunti ya shule na kupeleka risiti shuleni.

Vilevile akaagiza kuwa mbali na wanafunzi hao kulipa fedha hizo pia kila mmoja alitakiwa kuandika barua ya kukiri kosa na kuahidi kutorudia tena kufanya jambo kama hilo huku wanafunzi 26 waliokutwa na simu akiwataka kufika shuleni wakiwa wameambatana na wazazi wao.

Aidha, akasisitiza kuwa kwa mwanafunzi yeyote ambaye angeamua kutorejea shuleni angefuatwa nyumbani kwao kwa pingu na waliokuwa na mawazo ya kuhamia kwenye shule za watu binafsi alisema serikali ingewazuia kufanya mitihani ya taifa.

### RAIS AMPONGEZA

Baadhi ya watu walikuwa wanafikiria kuwa pengine Rais John Magufuli, angekerwa na adhabu iliyotolewa na Chalamila na kumtumbua ,mambo hayakuwa hivyo, badala yake ikawa kummiminia sifa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa.

Siku chache baada ya Chalamila kuwatimua wanafunzi hao, Rais Magufuli alitua katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (Sia) akielekea Songwe kwa ziara ya kikazi na akiwa katika uwanja huo alizungumza na wananchi waliofika kumlaki.

Moja kati ya vitu alivyozungumza ni pamoja na tukio hilo la wanafunzi wa Sekondari Kiwanja kuchoma mabweni pamoja na adhabu aliyoitoa Chalamila.

Rais Magufuli alimsifu Mkuu wa Mkoa kwa adhabu aliyoitoa kwa wanafunzi hao huku akiikosoa sheria inayozuia viboko shuleni kwa kusema kama inawezekana ibadilishwe ili wawe wakitandikwa.

"Nakupongeza sana Chalamila kwa kuwatandika wanafunzi wale na kama kuna sehemu tulikosea basi ni ile sheria, inabidi tuirekebishe wawe wanatandikwa, hata Ulaya wanatandikwa vizuri kabisa," anaeleza Rais Magufuli.

Akasisitiza kuwa viboko vinasaidia kufundisha wanafunzi kuwa na nidhamu pamoja umakini wanapofundishwa. Pamoja na hatua hiyo alitangaza kuifuta bodi ya shule kutokana na kuchelewa kuchukua hatua dhidi ya wanafunzi hao na akaagiza iundwe upya.

> Nakupongeza sana Chalamila kwa kuwatandika wanafunzi wale na kama kuna sehemu tulikosea basi ni ile sheria...

### WAZIRI JAFO

Hivi karibuni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo, alifanya ziara katika shule hiyo kwa ajili ya kukagua maendeleo ya ukarabati wa mabweni yaliyokuwa yameungua ambapo alishuhudia shughuli mbalimbali zikifanyika.

Anamshukuru Chalamila kwa kuwaadabisha wanafunzi hao waliofanya tukio hilo pamoja na usimamizi mzuri kwenye ukarabati wa mabweni yaliyounguzwa.

Anasema kutokana na tukio hilo serikali itahakikisha inasimamia nidhamu ya wanafunzi shuleni kwa kuona kwamba wanaoharibu miundombinu ya shule wanawajibika kuikarabati pamoja na wazazi wao.

"Kuna matukio kama haya huko Morogoro, wanafunzi walichoma shule mpya kabisa, kuanzia sasa hivi kila mwanafunzi atakayeharibu miundombinu ya shule, mzazi au mlezi wake atawajibika kulipa, nawashukuru hapa mmefanya kazi kubwa sana," anasema Jafo.

Anasisitiza kuwa serikali inatumia fedha nyingi kujenga miundombinu ya elimu, hivyo haitawafumbia macho wanafunzi na wengine wote wanaoshiriki kuiharibu kwa makusudi.

Katika miaka ya hivi karibuni matukio ya mabweni ya shule mbalimbali kuteketea kwa moto yamekuwa yakisikika mara kwa mara na tangu mwaka 2016 shule takribani tano ikiwamo kongwe ya wavulana Iyunga ya jijini Mbeya zimekumbwa na kadhia hiyo.

## Ebola yaelekea kupungua Congo



Madaktari wakitibu mgonjwa wa ebola Congo. **PICHA: MTANDAO.**

NCHINI Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) imethibitishwa kuwa hakuna kisa chochote cha ebola kilichoripotiwa katika siku 7 zilizopita mwezi Februari na hii ni mara ya kwanza tangu mlipuko wa ebola ulipoanza Agosti mwaka 2018 nchini humo.

Shirika la afya Duniani (WHO) linasema: "Haya ni mafanikio makubwa kwa kuwa tangu tarehe 19 hadi 25 ya mwezi Fabruary hakuna kisa kipya cha Ebola kilichothibitishwa. Kisa cha mwisho kabisa kiliripotiwa kwenye ukanda wa afya wa Beni jimboni Kivu Kaskazini.

Hata hivyo WHO inasema kuwa licha ya kutokuwepo kwa mgonjwa mpya wa ebola katika kipindi hicho cha siku 7 , mlipuko wa ebola bado uko hai na hatari za visa vipya kupatikana ni kubwa.

WHO inaonya kuwa pamoja na kuimarishwa kwa operesheni za ufuatiliaji katika maeneo hatari zaidi, maambukizi nje ya maeneo hayo hayawezi kuenguliwa.

Shirika hilo linasema kuwa hatua hiyo ni muhimu kwa kuwa katika tukio moja wakati wa mlipuko wa sasa, mgonjwa wa Ebola aliyepona alionyesha tena dalili za ugonjwa huo, alifuatiliwa na kuibua mnyororo mpya wa maambukizi ambao ulichukua miezi kadhaa kuibuka.

Kwa mantiki hiyo, shirika hilo linasisitiza kuwa ili kupunguza uwezekano wa kuibuka tena kwa mlipuko, ni muhimu kuendeleza hatua za sasa za kubaini na kuchukua hatua haraka dhidi ya wagonjwa wapya na kuwapatia kipaumbele cha kusaidia walionusurika . Aidha pia na kuwasaidia waliopona ugonjwa huo.

WHO inaongeza kuwa ili kuendeleza operesheni za sasa , fedha zaidi zinahitajika ambapo mahitaji ya fedha kwa operesheni hizo kati ya mwezi Januari na Machi mwaka huu ni dola milioni 83.

Mchango wa wahisani umefanikisha kiasi cha fedha na kinachohitajika na sasa ni dola milioni 40 ili kuendeleza operesheni na kutokomeza ugonjwa huo na kujenga mifumo thabiti ya afya.

Tangu kuibuka kwa ebola hadi February mwaka huu watu 3,444 wameambukizwa na kati ya hao waliothibitishwa kuwa na maradhi hayo ni 3,310.

Wagonjwa waliofariki dunia ni 2,264 sawa na asilimia 66. **RADIO UFARANSA**

JE, WAJUA?

# Taka za kielektroniki, plastiki huenda zikaangamiza dunia



Plastiki na vifaa vya kielektroniki vinavyohatarisha uhai baharini. **PICHA: MTANDAO**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Kuhifadhi Mazingira (UNEP), linakumbusha hatua zaidi kuchukuliwa kila wakati ili kuepusha madhara yatokanayo na ongezeko la taka za kielektroniki ambazo zinaiweka dunia hatarini.

Shirika hilo la mazingira la Umoja wa Mataifa, linasema taka za kielektroniki ni mbaya na hatari kwani haziyeyuki na zinachafua mazingira kwa muda mrefu.

Katika taarifa ya utafiti uliofanyika mwishoni mwa mwaka jana shirika hilo linasema baadhi ya vijana katika nchi mbalimbali ikiwamo Nigeria wamekuwa wabunifu na kugeuza taka hizo kuwa mali.

Na kwamba katikati ya Jjiji la Lagos Nigeria taka za elektoniki kwa miaka zilikuwa changamoto kubwa lakini sasa zimegeuzwa kuwa za thamani kwa kutumia mchakato mbadala wa kiuchumi.

Lengo la kuzichakata ni kulinda mazingira na kutoa ajira salama kwa maelfu ya Wanigeria na hasa vijana. Kwa mujibu wa UNEP kila mwaka Nigeria inazalisha tani 290,000 za taka za elektoniki pamoja na kupokea zaidi ya tani 70,000 za vifaa vilivyotumika kwa elektoniki kutoka katika mataifa yaliyoendelea.

Lakini sasa vifaa hivyo vya elektroniki vikifikia mwisho wa matumizi na kutupwa vinakusanywa na vijana kutoka sekta isiyo rasmi na vifaa ambavyo bado vinaweza kutumika vinasafishwa na kuuzwa tena na visivyofaa vinaharibiwa au kuchomwa katika maeneo maalum ya kutupa taka hizo na kuwapatia kipato vijana hao.

> “Makasha au maganda ya plastiki yaliyobandikwa kwenye kompyuta, simu au televisheni hayaozi yanajikusanya baharini na kusababisha matatizo kwa samaki na viumbe wa baharini ambao hushindwa kuzaliana.

**ATHARI**

Hata hivyo, wataalam wa afya wanaonya kwamba kemikali za sumu zilizo katika taka za elektroniki zinasababisha madhara ya ngozi, matatizo ya kupumua, kupunguza maisha ya wanaoziharibu, kuchafua hewa, maji na udongo.

Katika kuepukana na yote haya UNEP inasema Nigeria inaboresha sheria ya uwajibikaji kwa watengenezaji ili kuhakikisha wanawajibika na bidhaa wanazozalisha kwa muda wote wa mzunguko wa maisha ya bidhaa hizo.

Kwa mantiki hiyo sekta salama na yenye ufanisi ya matumizi mbadala ina fursa kubwa kwa uchumi wa Nigeria, kwani vifaa hivyo vya kielektroniki vilivyoharibika vina vitu vyenye thamani kubwa ndani yake kama dhahabu, madini ya platinum na vitu vingine adimu vya thamani.

Sekta hiyo ya kushughulika na taka za elektroniki sasa inatoa ajira kwa watu zaidi ya 100,000 Nigeria.



**TAKA ZA KIELEKTRONIKI**

Taka hizi ni kama betri za simu, maganda yake, nyaya zinazouda simu na kwa ujumla hata chaja na viambato vyote.

Kingine ni kompyuta na betrii zake, vyoo, nyaya na mabati yanayoziunda. Kwenye televisheni kadhalika viambato vyake vyote mpaka rimoti.

Taka nyingine zimo kwenye viyoyozi, friji, redio na vifaa kama microwave vinavyotumiwa kupasha moto chakula.

Kwa hiyo ni changamoto kubwa na ni jukumu la serikali kuzidhibiti na kuepusha athari kwa viumbe hai kwa kuwa taka hizo kama zilivyoelezwa huchangia kuleta matatizo ya ngozi, matatizo ya kupumua, kupunguza maisha ya wanaoziharibu, kuchafua hewa, maji na udongo.

Katika hatua nyingine Shirika la Kazi Duniani (ILO) linaonya kuwa taka za kielektroniki ni hatari kwa mazingira na usalama wa watu na viumbe hai.

Mwishoni mwa mwaka Guy Ryder, Mkurugenzi wa ILO, anakaririwa akisema kuwa kuna haja kwa Jumuiya ya Kimataifa kuhakikisha kwamba, inaweka sera na mikakati ya kuchakachua taka za kielekroniki, ili ziweze kutumia tena.

Shirika la ILO na UNEP pamoja na wadau mbali mbali wanabainisha kwamba, licha ya plastiki zinazoendelea kuchafua mazingira kiasi cha kutishia usalama wa viumbe hai, kuwapo kwa wimbi kubwa la taka za kielektroniki takribani tani milioni 50 zinazozalishwa kila mwaka kunaongeza hofu na kitisho zaidi.

Taka hizo zinazoweza kuchambuliwa kitaalamu, hazijaweza kuchambuliwa kikamilifu.

Guy Ryder, Mkurugenzi wa Shirika la Kazi Duniani anasema kuna haja kwa jumuiya ya kimataifa kuhakikisha kwamba, inaweka sera na mikakati ya kuchakata taka hizo.

Taka hizi zinapaswa kukusanywa, kurudishwa tena kwenye mzunguko wa uzalishaji, ili hatimaye, zitengenezwe na kuwa ni bidhaa mpya, tayari kuuzwa sokoni.

Juhudi hizi zifanyike kwa kuzisaidia nchi maskini kwani ndizo zenye mzigo mkubwa zaidi.

Kazi ya kurejeleza au kuzichakata tena itasaidia kusukuma mbele gurudumu la uchumi wa kimataifa, huduma kwa binadamu sanjari na utunzaji bora wa mazingira au nyumba ya wote. Anakumbusha kuwa taka hizo ni hatari mno .

Makasha au maganda ya plastiki yaliyobandikwa kwenye kompyuta, simu au televisheni hayaozi yanajikusanya baharini na kusababisha matatizo kwa samaki na viumbe wa baharini ambao hushindwa kuzaliana.

**ATHARI MAJINI**

Katika mito na baharini, zina madhara kwa samaki kwa sababu wananaswa na kushindwa kutoka kutafuta chakula.

Takataka hizo zilizoko ufukweni mwa bahari husababisha vifo vya viumbe wengi wa bahari. Na kwa mujibu wa UNEP asilimia 80% ya plastiki zinaishia baharini, ikiwa ni karibu tani milioni nane hadi milioni 12 kila mwaka.

Kwa msingi huo inakadiriwa kuwa ifikapo mwaka 2050 idadi ya plastiki kwenye bahari iwe ni viroba, mabeseni , matairi na chochote kingine chenye asili ya plastiki, wingi wake utakuwa ni mkubwa zaidi kuliko kiasi cha samaki.

Hali hiyo ambayo itatokea miaka 29 kuanzia sasa kama haitadhibitiwa kuna hatari na kitisho kikubwa kwa hatma viumbe vinavyoishi maziwani, baharini na mtoni.

Takwimu za UNEP zinaonyesha kwamba, mwaka 2016 tani 480 bilioni za plastiki zilitumika na makadirio ni tani 560 bilioni zinatarajiwa kutumika ifikapo 2021.

Kiasi kikubwa cha taka hizi, kitaishia kwenye bahari, ziwani na mitoni, kiasi hata cha kuhatarisha maisha ya viumbe hai kuanzia biandamu, wanyama wafugwao na wa porini na mimea pia. **MITANDAO**

UCHAMBUZI

**NA GRACE MWAKALINGA, KYELA**

# Haya ndiyo yanayowaelemea wanafunzi wenye ulemavu Kyela



Mwalimu wa kitengo maalum cha kuwahudumia watoto wenye ulemavu Shule ya Msingi Kyela, Butwa Kasesela akiwafundisha na kuwahudumia watoto wenye mahitaji maalum ndiye pekee ambaye amebeba jukumu la kuwahudumia watoto hao. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

WAKATI dunia ikishuhudia miaka 31 ya utekelezaji wa mkataba wa kimataifa wa haki za mtoto (CRC) tangu ulipopitishwa na Umoja wa Mataifa mnamo mwaka 1989, watoto wengi wenye ulemavu wameendelea kutaabika kutokana na kukosa haki zao.

Wilaya ya Kyela ni miongoni mwa maeneo ambayo haki za watoto wenye ulemavu ni changamoto kupatikana hasa huduma ya elimu katika mazingira bora.

Mazingira katika shule ya Kyela kwa watoto wenye mahitaji maalum, yanathibitisha kuwapo kwa adha kubwa wanazopata walimu na wanafunzi katika utoaji na upokeaji wa elimu kutokana na mazingira kutokuwa rafiki.

Mwalimu wa kitengo cha kuwahudumia watoto hao shuleni hapo, Butwa Kasesela, anasema anawahudumia wanafunzi wenye ulemavu 19 miongoni mwao wako wenye matatizo ya akili, wengine ni bubukiziwi na usonji (autism).

"Kama unavyoona mazingira, natumia darasa moja kuwafundishia watoto wote, miundombinu si rafiki kwao ni vigumu kuwahudumia wote kwa wakati mmoja kwa sababu kila mtoto na tatizo lake," anasema mwalimu kasesela.

"Licha ya kubeba jukumu hili la kuwafundisha watoto hawa, lakini vilevile nalazimika kuwapikia chakula cha mchana kwani hakuna yeyote aliyeajiriwa kuwapikia watoto hawa wenye mahitaji," anaongeza Mwalimu Kasesela.

Kasesela anasema kwa mujibu wa sera ya elimu, mwalimu mmoja anatakiwa ahudumie mtoto mmoja mwenye tatizo la usonji na wenye shida ya viungo na bubukiziwi wanatakiwa wawe watano katika darasa moja.

Anasema mbali na tatizo la miundombinu ya madarasa, vyoo na vifaa vya kujifunzia na kufundishia Shule ya Msingi Kyela, kuna mwalimu mmoja pekee wa kuwahudumia watoto wenye mahitaji maalum licha ya shule hiyo kuwa miongoni mwa zilizotengwa kwa ajili ya kuwafundisha wenye ulemavu.

Kasesela ambaye ni mwalimu pekee wa kufundisha watoto wenye mahitaji maalum, anasema kwa kawaida anatumia dakika 10 hadi 20 kuwafundisha watoto wote, muda ni mfupi lakini umejaa mbinu mbalimbali za kufundishia kwa sababu ya hali walizonazo wanafunzi hao.

Anasema anatumia muda huo ambao unavichangamshi ikiwamo michezo ili watoto wapate hamu ya kupenda shule hasa wenye matatizo ya akili. Anaongeza kwa mujibu wa sera ya elimu watoto wenye mahitaji maalum hususani tatizo la akili na wenye usonji wanasoma kwa mfumo wahatua ambazo huanzia ya kwanza hadi ya tatu wakifikia ya nne hupelekwa katika madarasa ambayo huchangamana na wenzao wasiokuwa na matatizo.

> Kama unavyoona mazingira, natumia darasa moja kuwafundishia watoto wote, miundombinu si rafiki kwao ni vigumu kuwahudumia wote kwa wakati mmoja kwa sababu kila mtoto na tatizo lake.

"Kitengo maalum cha watoto wenye ulemavu kilianza mwaka 2008 hapa shule ya msingi kyela baada yakufanya kampeni ya kuhamasisha wazazi na walezi kuwapeleka watoto shule, mimi ni mwalimu pekee ambaye nilikabidhiwa jukumu la kuwahudumia licha ya kuwa mbobezi wa kufundisha watoto wenye magonjwa ya akili," anasema Kasesela.

Anaeleza kazi ya kuwafundisha watoto wenye mahitaji maalum ni ya wito kwa sababu ina vikwazo vingi hasa ukizingatia anatumia darasa moja, ratiba za ufundishaji zinapishana wakati wote wakiwa darasani.

### HALI YA UFAULU

Mwalimu Mkuu wa Shule, Degratius Mpalile, anasema maendeleo ya kitaalum kwa watoto wenye mahitaji maalum sio ya kuridhisha kwa sababu ya miundombinu ya shule ilivyo lakini pia wazazi kuchelewa kuwaandikisha shule.

Anasema serikali inatoa fedha kila mwezi Sh. 300,000 hadi 400,000 kwa ajili ya chakula kwa watoto wenye mahitaji maalum na walianza hivyo tangu mwaka 2016.

Lakini bado, hawafanyi vizuri kitaalum na kutolea mfano kwa mwaka 2019/2020 matokeo ya darasa la jumla ya wanafunzi 168 walifanya mtihani,waliofaulu ni wavulana 57 na wasichana 74 lakini hakuna mwenye ulemavu yeyote aliyefaulu, 37 walifeli akiwemo mwenye ulemavu ambaye alikuwa bubukiziwi.

Anasema wanaendelea na jitihada za kuhakikisha watoto wenye mahitaji maalum hasa wenye usonji wanapata maarifa ya kujitegemea kwa sababu ni vigumu kufaulu mitihani hivyo wanahitaji kupata stadi za maisha ikiwamo ufundi ili wajiajiri.

"Serikali na wadau wengine wasaidie ujenzi wa bweni kwa ajili ya watoto hao pamoja na madarasa na vifaa vya kufundishia lakini pia kujengwa uzio ili wasitoroke au kuleta vurugu kwa wenzao,"anasema Mwalimu Mpalile.

Hata hivyo, Mpalile aliwatupia lawama wazazi na walezi wanaowaficha watoto wenye ulemavu nyumbani badala ya kuwapeleka shule, anasema kupitia kamati ya shule na wadau wengine wamekuwa wakihamasisha waandikishwe, lakini bado muitikio ni mdogo.

### MAONI YA WAZAZI

Miongoni mwa wazazi wa wanafunzi hao, Ramadhan Sanga, anampongeza Kasesela kwa kujitoa kufanya kazi ya kuwafundisha na kuwahudumia watoto hao ambao wana matatizo makubwa hasa namna ya kuwalea wawapo shuleni.

Sanga anasema mwanae ana matatizo ya akili anahitaji uangalizi mkubwa kumhudumia kwa sababu ya hali yake anaweza kupiga watu, kula vitu vichafu, lakini tangu aanze shule kuna mabadiliko makubwa ameyaona kwa mwanaye.

### KUBORESHA MIUNDOMBINU

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewana Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Dk. Hunter Mwakifuna, Kyela ina jumla ya shule za msingi 104. kutokana na sera ya elimu bila malipo, kumekuwa na ongezeko la uandikishwaji wa wanafunzi ambapo ngazi ya awali, wameandikishwa wanafunzi 6,947 sawa na asilimia 102 ya uandikishaji ikilinganishwa na uandikishaji wa mwaka 2018/2019 uliofikia asilimia 89.4.

Anasema kumekuwa na ongezeko la ufaulu, takwimu zikionyesha kuwa mwaka 2018/2019 asilimia 67.08 ya wanafunzi waliofanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi walifaulu na kuchaguliwakujiunga na kidato cha kwanza ukilinganisha na ufaulu wa asilimia 63.07 ya mwaka 2017/2018.

Ufaulu huo uliifanya halmashauri hiyo kushika nafasi ya tatu katika halmashauri saba za mkoa wa Mbeya.

Mwenyekiti huyo anasema katika kuboresha miundombinu ya sekta ya elimu msingi, mwaka wa fedha 2018/2019 wilaya hiyo ilitumia Sh. milioni 264 kujenga vyumba vya madarasa 38 na matundu 56 ya vyoo.

Anasema kufuatia maelekezo ya Wizara ya Elimu kutengeneza mazingira wezeshi halmashauri kwa kushirikiana na wadau wengine imejenga vyoo maalum kwa watoto wenye ulemavu katika shule ya msingi mwenge na kyela.

Ofisa Elimu Wilaya ya Kyela, Palemon Ndarugiliye, anasema watoto wenye mahitaji maalum bado wanakabiliwa na changamoto ya miundombinu ya shuleni hali inayosababisha kutofanya vizuri kwenye masomo yao.



WADAU
SABATO KASIKA

# Sauti za wadau

**Uhusiano mzuri kati ya wazazi na walimu ni jambo la muhimu kwa maendeleo ya elimu kwa mwanafunzi. Lakini hilo halipo kwenye baadhi ya shule nchini. Wadau wanasemaje?**



### RAHEL MGALLA (MHITIMU WA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM)

KWANZA kabisa, uhusiano mzuri kati ya wazazi na walimu ni mwanga kwa maisha na mipango ya elimu ya mtoto. Kwa hiyo wazazi inatakiwa wawe karibu sana na mtoto pamoja na walimu shule ili kumwezesha kufanya vizuri.

Mfano ni hizi shule za English Medium kila mzazi lazima ampende na kumthamini mtoto, ndiyo maana ni lazima ampeleke na umfuate au umpokee mara gari la shule linapomrudisha baada ya muda wa masomo. Kama mtoto amekosea, mzazi ataambiwa.

Kwa hiyo kama mzazi kwanza hutapenda mtoto wake asiwe na tabia mbaya au afeli atakuwa anamfuatilia, kwani hiyo njia ndiyo itamfanya pia mwalimu ampende na kumsaidia zaidi.

Vilevile ieleweke kwamba mzazi au mlezi ni mtu anayekaa na mtoto kwa malezi au malengo hulani. Kwa mfano anakaa na watoto au mtoto ili amfunze na kumfundisha maadili mema na pia anampa elimu isiyo rasmi.

Hii inasaidia mtoto kujitambua na kujenga mazingira, ambayo yatamjengea upevu wa akili popote atakapokua na akienda shule atapata mlezi, ambaye ni mwalimu, huyu atampatia elimu rasmi, ambayo itampa upevu wa kujua dunia zaidi.

Kwa hiyo basi mzazi na mwalimu wanakutana wapi? Ni pale mzazi atakapokua anafuatilia nini mtoto wake anafanya shuleni na makosa yake ni yapi, maendeleo yake, hivyo kumfanya mwalimu naye kuwa karibu na mtoto huyo. Ikumbukwe kuwa kuna watoto walioshindikana nyumbani hata shuleni.

Sasa mtoto kama huyo iwapo mzazi atamwachia mwalimu amdhibiti, naye atashindwa.



### JOHN SAMBU (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

UHUSIANO mzuri kati ya wazazi na walimu ni miongoni mwa mambo ya msingi sana, kwa sababu hatua hiyo inaimarisha na kuboresha kazi za walimu na kuleta matokeo au maendeleo mazuri ya elimu ya wanafunzi, kutokana na ukweli kwamba walimu wanakuwa huru kufanya kazi yao bila wasiwasi au woga na kushindwa kutimiza wajibu wake inavyotakiwa.

Kwa hiyo uhusiano mzuri kati ya watu hawa wawili ni wa muhimu ikizingatiwa kuwa wote ni wazazi na wanategemewa katika malezo bora ya mwanafunzi.

Lakini mmojawapo asipotimiza wajibu, mwanafunzi anaweza kukwama kufikia malengo yake aliojiwekea kwenye elimu. Kumekuwa na mtindo wa baadhi ya wazazi kuwaonea walimu hata wakati mwingine kuwapiga, kwa sababu tu wameadhibu watoto wao.

Sasa katika mazingira kama hayo, uhusiano kati ya makundi hayo mawili unaweza kuwa mbaya, kwa sababu mmojawapo kutotambua kile anachopaswa kufanya.

Kama kweli mwalimu amemuadhibu mtoto na kumuumiza, basi mzazi afuate taratibu ili kumaliza tatizo, siyo kwenda shule kufanya ugomvi.

Ninatambua kwamba wapo baadhi ya walimu ni wakorofi, yaani kuna wazazi wakorofi, walimu wakorofi na wanafunzi wakorofi.

Wote hawa kila mmoja anatakiwa kutimiza wajibu wake ambao utawafanya waendelee kuwa na uhusiano mzuri utakaomuwezesha mwanafunzi kusoma bila usumbufu usio wa lazima.



### RACHEL GRABAYA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

MAENDELEO mazuri ya mwanafunzi shuleni yanategemea mambo mengi kuanzia mahudhurio yake mwenyewe, ufundishaji na ujifunzaji na pia suala la usimamizi wa mwanafunzi katika elimu.

Jambo hili la usimamizi katika elimu linahitaji ushirikiano kati ya wazazi na walimu. Kila upande ukijitenga na kudhani hauwajibiki kudhibiti nidhamu ya mwanafunzi au kutoona umuhimu wa kufuatilia kwa karibu mienendo ya mwanafunzi kuanzia nyumbani hadi shuleni, basi hali inaweza kusababisha mhusika kuwa na maendeleo mabovu katika masomo.

Kwa hiyo msingi wenye maendeleo mazuri ya kielimu kwa mwanafunzi ni ule uliojengwa katika uhusiano mzuri kati ya mzazi wa kwanza na wa pili ambaye ni mwalimu.

Kwa uhusiano wao mzuri wanaweza kuwarekebisha watoto wakorofi na hata kumaliza utoro unaofanywa na baadhi ya wanafunzi, kwani watabanwa kuanzia nyumbani hadi shuleni.

Lakini pia niweke wazi kuwa ushirikiano mdogo wa wazazi na walimu ni sababu mojawapo ya wanafunzi kufanya vibaya katika masomo au mitihani.

Walimu na wazazi wanatakiwa kuzungumza lugha moja kwa lengo la kujenga maadili ya watoto. Maadili ya wanafunzi yanaweza kuwa imara hasa kutokana na ushirikiano wa karibu kati ya wazazi, walimu na jamii kwa ujumla.



### THOMAS NGAWAIYA (MKURUGENZI MTENDAJI WA CEGODETA)

KUNA msemo kwamba umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu. Msemo huu una unagusa sehemu nyingi katika maisha yetu ya kila siku ikiwamo suala la uhusiano mzuri kati ya wazazi na walimu. Unaposemа mahusiano mazuri, mimi ninachukulia kama ushirikiano, kwani ukikuta watu wanashirikiana, basi jua kwamba wana mahusiano mazuri.

Hivyo hata kwenye suala hili la maendeleo mazuri ya mwanafunzi shuleni linategemea pia uhusiano mzuri kati ya walimu na wazazi, kwani iwapo wawili hawa hawatakuwa kitu kimoja, wanaweza kumkwamisha mwanafunzi aidha iwe ni walimu kumkomoa mwanafunzi ili akate tamaa katika masomo, kwa sababu hawaelewani na mzazi wake ama kwa namna yoyote ile. Mara nyingi chanzo cha mahusiano mabaya kati ya walimu na wazazi huwa kinaanzia kwenye adhabu.

Wapo baadhi ya wazazi wasiotaka watoto wao waadhibiwe na wakisikia hilo wanakuja juu. Lakini mimi ninaamini kwamba adhabu kwa mwanafunzi ni sehemu ya kutoa onyo ya kutoa na siyo kukomoa ingawa wapo baadhi ya walimu ambao ni kama wanakomoa wanafunzi, na mwisho wa siku adhabu zao zinaleta madhara.

Sasa katika mazingira kama hayo mzazi hawezi kukubali mtoto wake aumizwe, na adhabu za aina hiyo pia zinaweza kumfanya mtoto akawa sugu. Nihitimishe kwa kusema kuwa, jambo la msingi ni walimu na wazazi kujenga uhusiano mzuri kwa ajili ya maendeleo ya wanafunzi kielimu na kila upande itumize wajibu wake na kuacha lawama zisizo na msingi.



### JUDITH MREMI (MWALIMU MNAZI MMOJA SEKONDARI DAR)

SISI walimu kama walezi tuna jukumu kubwa la kuwalea wanafunzi katika maadili mema yatakayowajenga.

Lakini bahati mbaya baadhi yetu tunakuwa na wakati mgumu sana kwa kukosa ushirikiano kutoka kwa baadhi ya wazazi, hasa linapokuja suala la kuwarekebisha watoto wao. Unaweza kukuta mwanafunzi amefanya makosa, halafu walimu wakawashirikisha ili kujua kinachoendelea na kushirikiana katika kutoa maamuzi.

Lakini unaweza kukuta baadhi ya wazazi wanalalamika kuwa sisi walimu ni waonevu, kwamba tunawaadhibu watoto wao bila sababu, na hivyo kuwa na chuki zisizo na msingi kwetu kutokana na hatua tunazochukua za kutaka kuwarekebisha au kuwasaidia watoto wao. Wanasahau kwamba wana nafasi ya kushirikiana nasi kwa ajili ya kuwasaidia watoto wao kuwa na maadili bora. Walimu tunajikuta katika wakati mgumu tunapotimiza wajibu wetu na kuonekana kama hatufai, tunatesa watoto wao na kumbe lengo letu ni zuri.

Na mimi nakuhakikishia kuwa mahusiano mazuri kati ya wazazi na walimu yana manufaa makubwa kwa wanafunzi, kwani mzazi mwenye mahusiano mazuri na walimu, lazima anafuatilia maendeleo ya mtoto wake shuleni na kama walimu wanaona kuna kitu ambacho hakikosa sawa kwa mwanafunzi, watamuambia mzazi wake na watasaidiana kumkerebisha iwapo wataona anakwenda vibaya.



## HABARI MBEYA

# Barabara yakwamisha malori 30 ya viazi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MADEREVA zaidi ya 30 wa magari yanayosafirisha viazi kutoka katika vijiji mbalimbali vya Kata ya Ilungu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameiomba serikali kuiboresha barabara ya Mbeya - Makete kupitia Isyonje kwa madai kuwa imeharibika na inahatarisha usalama wao.

Wakizungumza na Nipashe katika Kijiji cha Igoma wakati walipokuwa wanafukia mashimo madereva hao, walisema wamekwama katika kijiji hicho kwa zaidi ya wiki moja baada ya moja ya malori kukwama kwenye tope na kuzuia njia.

Mmoja wa madereva hao, Abdallah Juma, alisema barabara hiyo kwa sasa imeharibika kutokana na mvua inayoendelea kunyesha katika maeneo hayo na kwamba katika eneo hilo la Igoma ndio hatari zaidi.

Alisema waliamua kukubaliana na madereva wote na makondakta wao kuanza kufukia mashimo kwenye baadhi ya maeneo ili wayatowe magari yaliyokwama na kuendelea na safari lakini kazi bado ni ngumu.

"Tumekaa hapa kwa muda wa wiki moja na siku kama mbili, kitendo cha kukwama hapa kimetuongezea gharama za maisha na hata viazi tulivyobeba kuna hatari vikaharibika tukiwa bado tupo njiani, tunaomba serikali itusaidie kuirekebisha," alisema Juma.

Naye Raphael Mwandembwa, alisema baadhi ya magari yamekuwa yakiharibika kutokana na ubovu wa barabara hiyo na kwamba wanatumia muda mrefu kusafiri kipande kidogo.

Alisema eneo hilo linazalisha viazi kwa wingi kuliko maeneo yote ya Mbeya na Serikali inakusanya fedha nyingi kutokana na viazi hivyo, lakini hakuna anayekumbuka kuboresha barabara hiyo.

"Tunamwomba Waziri mwenye dhamana ya miundombinu hii atusaidie maana gari ikiingia kwenye haya mashimo unaweza ukakata hata springi, sasa hivi tuna wiki hapa tunahangaika na magari haya na gharama zinaongezeka," alisema Mwandembwa.

Alisema magari hayo yakikwama wanalazimika kuwaajiri vijana kwa ajili ya kusombelea magunia kwa kujitwisha ili mzigo upunguwe na wakishalikwamua gari wanaanza tena kupakia na hivyo gharama kuwa kubwa.

Hivi karibuni, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (anayeshughulikia Ujenzi), Elius Mwakalinga, alimwagiza Meneja wa Wakala wa Barabara nchini (Tanroads) Mkoa wa Mbeya, Eliazary Rwekaza, kuifanyia matengenezo ya dharura barabara hiyo. Alisema itengenezwe kwa kiwango cha changarawe kwa zaidi ya kilomita 90 ili wananchi wanaoitumia waendelee kupata huduma bora ya usafiri kama ilivyo kwa maeneo mengine.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (mwenye balaghashia), akipongezwa na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa Mkoa huo, Jacob Mwakasole, kwa kusimamia vizuri ujenzi wa miundombinu ya barabara mkoani humo ikiwamo barabara ya viwandani katika eneo la Iyunga, wakati wa ziara ya kamati ya siasa ya chama hicho mkoa ya kukagua miradi, jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wanawake waapa kutekeleza wajibu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WANAWAKE katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameapa kusimamia na kutekeleza wajibu wao ndani ya jamii ikiwamo kukubaliana na vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya watoto pamoja na wenye ulemavu.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa Vituo vya Taarifa na Maarifa, Flora Mlowezi, alipokuwa akizungumza na Nipashe kuelekea sikukuu ya wanawake duniani ambayo maadhimisho yake ni Machi tatu mwaka huu.

Mlowezi alisema miongoni mwa ajenda ambazo wanawake wamezivalia njuga ni vita dhidi ya vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na walemavu, ambavyo mara nyingi hufanywa ndani ya familia husika.

Alisema katika kukabiliana na suala hilo, kupitia maadhimisho watatoa elimu juu ya madhara ya vitendo hivyo na kuwasisitiza watoto na wenye ulemavu kuripoti kwenye vyombo vya sheria.

"Siku ya Wanawake imebeba tafakuri kubwa ya kujadili maendeleo na vikwazo vinarudisha nyuma jitihada zetu ni wazi sasa tumeanza kuona mabadiliko katika nyanja mbalimbali za kielimu, afya, maji na kilimo lakini bado tunaendelea na vita dhidi ya vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na wenye ulemavu," alisema Mlowezi.

Alisema mbali na kukabiliana na vitendo vya ukatili, lakini wamebeba ajenda ya uchaguzi kupitia ilani ya wanawake ya mwaka 2019/2020 iliyozinduliwa mwaka 2019 na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), ambayo ndani yake imeeleza mikakati ya 50/50 baina ya mwanaume na mwanamke katika uongozi.

Alifafanua kuwa ilani hiyo imetoa dira kwa wanawake kugombea nafasi mbalimbali za uongozi wakiwa wanabeba ajenda za maendeleo zenye kukubalika.

Diwani wa Kata ya Mshewe, Esther Mbega, alisema yeye ni miongoni mwa wanawake waliopigwa vita wakati anagombea nafasi ya udiwani mwaka 2015, alisema licha ya vitisho na kejeli alisimamia ajenga za maendeleo na hatimaye akamshindwa mpinzani ambaye alikuwa ni mwanaume.

Alisema katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Dunia, lazima kujadili mikakati ya kuhakikisha wanawake wengi wanajitokeza kugombea uchaguzi katika nafasi mbalimbali kuanzia udiwani hadi urais.

## Wapewa zigo udhibiti mifugo mashambani

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

VIONGOZI wa Serikali za Mitaa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, wametakiwa kuhakikisha mifugo haingii kwenye mashamba ya mipunga ambayo yamelimwa ili kuepuka migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

Agizo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Mtendaji wa Mamlaka ya Mji wa Rujewa, Tuntufye Chamba, wakati akizungumza na wenyeviti wa mitaa wa mamlaka hiyo, alisema kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wakulima kuwa wafugaji wanaingiza mifugo kwenye mashamba yao.

Alisema wafugaji wanaotajwa kuingiza mifugo kwenye mashamba wanatumia kisingizio cha kufuata majani ya malisho ambayo yako kando kando ya mashamba ya mpunga, lakini kutokana na usimamizi mbovu wa wafugaji hao ng'ombe huvamia mashamba na kutafuta mazao.

Aidha, mtendaji huyo alisema katika kipindi hiki cha msimu wa kilimo ni vyema mifugo ikazuiliwa kuingizwa kwenye mashamba yote mpaka pale shughuli za kupanda hadi kuvuna mpunga zitakapomalizika na kama ni kuruhusu mifugo basi iwe ni ridhaa ya wakulima wote.

"Hatutaki migogoro kwenye mji wetu baadhi ya sehemu tuna wafugaji na kwingine kuna shughuli za kilimo hasa mpunga, pande hizi mbili lazima tuzisimamie ili tusiingie kwenye migogoro," alisema Chamba.

Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji huo, Chameta Godigodi, alikiri kuwapo kwa malalamiko ya baadhi ya wenyeviti kutumia madaraka yao kuruhusu mifugo kuingizwa kwenye mashamba yanayolimwa.

Aliwataka wenyeviti kuwa na msimamo katika kutekeleza majukumu yao, huku wakiweka usawa kwenye maamuzi ili kuepuka migogoro itokanayo na mwingiliano usiofuata utaratibu.

Baadhi ya wenyeviti wa mitaa wa mji huo, walisema wapo baadhi ambao wamekuwa wakiendekeza rushwa ya kupokea fedha kutoka kwa wafugaji ili kuruhusu mifugo itafune mazao bila kuchukuliwa hatua.



## HABARI DODOMA

# Tanzania yapunguza maambukizi TB

Na Mwandishi Wetu, DODOMA

IMEELEZWA kuwa Tanzania ni nchi ya pili barani Afrika kwa kupunguza maambukizi na kutibu ugonjwa wa kifua kikuu (TB) na kufikia asilimia 75 ya malengo yaliyowekwa.

Hayo yalielezwa juzi na Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto-Idara Kuu Afya, Dk. Zainabu Chaula, alipokuwa akipokea ripoti ya tathmini ya mapitio ya mpango mkakati wa kifua na ukoma uliofanyika jijini hapa.

Alisema Shirika la Afya Duniani (WHO), limefanya tathmini kwa kushirikiana na wataalamu wengine kutoka nje na ndani ili kuona malengo yaliyowekwa kupambana na ugonjwa huo kama yamefikiwa. "Wanaangalia jinsi gani tumeyafikia malengo tuliyojiwekea kwenye mpango mkakati wetu wa mwaka 2015 ikiwamo kuongeza kasi ya kuwafikia wagonjwa kwa asilimia 29 zaidi," alisema.

Aidha, alisema tathmini hiyo ilikuwa ikiangalia malengo ya kidunia ya kumaliza tatizo la TB pamoja na ukoma.

"Asilimia nyingine tumepewa maelezo na tutaenda kuyaweka kwenye mpango mkakati mwingine tunaoenda kuuandaa na kuweza kushughulikia," alisema.

Hata hivyo, Katibu Mkuu huyo alisema bado kuna tatizo la uelewa kwa wananchi kwa kuwa ugonjwa wa TB unaenezwa kwa njia ya hewa.

"Tunashauri wananchi kuepuka misongamano, kulala kwenye nyumba zenye madirisha yenye hewa, kuzingatia usafi wa mazingira na kwa watu wenye dalili ni vyema kuwahi kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kupata matibabu kwani huduma za TB zinapatikana kuanzia ngazi za zahanati," alisema. Naye Kaimu Meneja wa Mpango wa Taifa wa kudhibiti na kutokomeza kifua kikuu na ukoma (NTLP), Dk. Zuweina Kondo, alisema wamefanikiwa kugundua wagonjwa kutoka asilimia 37 mwaka 2015 hadi asilimia 53 hivi sasa.

"Tulikuwa tumeweka mkakati wa kuwafikia wagonjwa na tumefikia kwa asilimia 43 zaidi kwa mwaka 2018 tuliwafikia wagonjwa 75,545 na mwaka 2019 tuliwafikia wagonjwa 82,140 , kadri unavyogundua wagonjwa wengi ndio tunapunguza maambukizi," alisema. Kwa upande wa watoto, Dk. Kondo alisema kuwa wamefikia lengo la WHO kwa asilimia 15 ambalo ni lengo la juu lililotajwa kidunia ambapo Tanzania ni kati ya nchi saba.

Alieleza kuwa kwa upande wa ukoma hivi sasa wameondoa ugonjwa huo kutoka halmashauri za wilaya 19 mwaka 2015 kubaki halmashauri 16 kwa kutoa elimu na kutafuta njia nyingine za kuwafikia wagonjwa.



Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, (SACP) Narcis Missama, kutoka Makao Makuu ya Jeshi hilo, akizungumza wakati wa kufungua mkutano wa wakurugenzi wa sekta binafsi Tanzania, uliofanyika jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Waonywa kwa ukaidi wa kuishi mabondeni

Na Peter Mkwavila, CHEMBA

JUMUIYA ya maridhiano ya viongozi wa dini, imewashauri wananchi wanaoishi mabondeni kuacha kung'ang'ania kuishi kwenye maeneo hayo ili kujiepusha kukumbwa na mafuriko.

Rai hiyo ilitolewa na Katibu Mkuu wa jumuiya hiyo, Askofu Osward Mlay, alipokuwa akitoa misaada mbalimbali kwa ajili ya waathirika wa mafuriko katika vijiji vya wilaya hiyo vyenye thamani ya Sh. milioni 100.

Alisema ni vyema wakazingatia ushauri wa serikali unaotolewa kwa wanaoishi mabondeni kwa kuwa kumekuwa na madhara makubwa pindi mvua zinaponyesha.

Alibainisha kuwa jumuiya hiyo imetoa vitu mbalimbali ikiwamo magodoro, vyandarua, mchele, sukari na mafuta ya kula ili kusaidia wananchi hao.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa jumuiya hiyo mkoa wa Dodoma, Askofu Evance Chande, aliwataka Watanzania kuona umuhimu wa kuwasaidia waathirika wanaopatwa na majanga mbalimbali yakiwamo mafuriko.

"Sisi Watanzania ni waumini wenye upendo na huruma, hivyo inapotokea majanga kama haya tujitokeze kwa kutoa mali na fedha kwa ajili yao," alisema.

Akizungumza baada ya kupokea msaada huo, Mkuu wa wilaya hiyo, Saimon Odunga, alisema atahakikisha inawafikia walengwa hao.

Odunga alitaja baadhi ya vijiji vilivyokumbwa na mafuriko kuwa ni Kelema, Farkwa, Kwa Mtoro na Handa.

Alisema wakazi wa vijiji hivyo walishapewa tahadhari na kutakiwa kuhama, lakini wamekuwa wakaidi wa kuondoka kwenye maeneo hayo.

# Viuatilifu vya sumukuvu vyapatikana

Na Renatha Msungu, DODOMA

SERIKALI imefanikiwa kupata viuatilifu aina mbili kwa ajili ya kudhibiti sumukuvu kwa asilimia 90 kwenye mazao ya mahindi na karanga.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Ofisa Kilimo wa Wizara ya Kilimo, Beatrice Palangyo, katika mkutano wa wadau wa sekta hiyo Afrika Mashariki uliofanyika jijini hapa.

Alisema viuatilifu hivyo vimepatikana baada ya utafiti uliofanywa na Wizara ya Kilimo na kwa sasa wanaomba visajiliwe ili vianze kutumika katika udhibiti wa sumukuvu.

"Tunaomba hivi viuatilifu vipate usajili tumevifanyia utafiti na kuona vinafaa kwa ajili ya sumukuvu, kwa kuwa kimethibitishwa kwa asilimia 90 uhakika huu utasaidia wakulima katika kudhibiti sumukuvu ambayo imekuwa kero kwa wakulima hususani katika mazao ya mahindi na karanga," alisema.

Alieleza katika mpango wa miaka mitano utasaidia kudhibiti tatizo hilo ambalo limekuwa kero kwa wakulima kwa muda mrefu.

Naye Meneja wa Udhibiti wa Sumukuvu, Idd Khatibu, alisema elimu inahitajika ili kurahisisha uelewa kuhusu sumukuvu.

Alisema watu wengi hususani wakulima hawana elimu ya sumukuvu, kitendo ambacho kinawaumiza wengi kwa kukosa elimu hiyo.

"Elimu zaidi inatakiwa kwa jamii ili wajue namna ya kujikinga na tatizo hili, lengo ni kuona kila mkulima anakuwa na uelewa juu ya madhara ya sumukuvu," alisema.

Kwa upande wake, mkulima John Mchau, alisema sumukuvu imekuwa ikisumbua wakulima na kuharibu mazao yao.

"Wakulima wengi hawana elimu ya utunzaji mazao hasa wa vijijini, na wamekuwa wakihifadhi mazao kiholela," alisema.



# Serikali kutatua changamoto Shule ya Mchangani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mkoa wa Kusini Unguja imeahidi kuondoa changamoto zinazowakabili wanafunzi wa Shule ya Msingi Mchangani, kufuata elimu masafa marefu wanapoingia sekondari.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohamed Mahmoud, aliyasema hayo wakati alipokuwa akizungumza na walimu na wanafunzi kwenye sherehe za kuwapongeza wanafunzi waliofaulu vizuri na kutoka michepuo katika shule hiyo ya Mchangani, Wilaya ya Kati Unguja.

Alisema kutokana na usumbufu unaowapata wanafunzi hao serikali ya mkoa huo itahakikisha inalisimamia suala hilo kwa lengo la kuondoa changamoto hiyo ya kufuata elimu ya sekondari kwa masafa marefu.

Aliwapongeza wanafunzi hao kwa kufaulu michepuo na kuingia madarasa ya sayansi na lugha ambayo imeleta faraja kwa Mkoa wa Kusini Unguja baada ya kuwa matokeo hayakuwa mazuri katika shule nyingine.

Ayoub aliwaomba walimu wazidishe juhudi katika elimu na wanafunzi wengi wafaulu ili maendeleo ya elimu yazidi kupatikana ndani ya mkoa huo.

Aliwataka wazazi na walezi kuacha tabia ya kuwapa watoto kazi nyingi za nyumbani ili wawe na muda mwingi wa kusoma na kufanya vizuri katika mitihani yao ya taifa.

"Kuna baadhi ya watoto hawana hata muda wa kudurusu masomo yao kutokana na kuelemewa kazi za nyumbani hivyo niwaombe wazazi kuwapunguzia kazi watoto wao ili waweze kupata muda mwafaka wa kujisomea na kupata mafanikio mazuri," alisema.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Mchangani, Sharif Suleiman Amour, alisema kutokana na ufaulu wa wanafunzi hao, shule hiyo imekuwa ya kwanza kwa Mkoa wa Kusini Unguja kwa kufanya vizuri katika mitihani ya taifa ya darasa la sita.

Akielezea changamoto zinazowakabili alisema kipindi cha mvua wanafunnzi wanashindwa kufika shule kutokana na ubovu wa barabara.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati ya shule hiyo, Ali Ahmada, aliiomba serikali ifanye juhudi za kuwasogezea shule ya sekondari kwa sababu wanafunzi hulazimika kufuata elimu ya sekondari masafa marefu na hutembea zaidi ya kilomita tisa.

Jumla ya wanafunzi saba kati ya 579 wa darasa la sita shuleni hapo wamepasi michepuo na ni kwa mara ya kwanza kwa shule hiyo kutoa idadi ya wanafunzi saba waliopasi darasa la sita na kwenda kidato cha kwanza vipaji maalumu.



Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Muhammed Said (kulia), akiangalia maonyesho ya zana za kufundishia na kujifunza kwa wanafunzi wa fani ya ualimu wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), yaliyofanyika chuoni hapo, Vuga, mjini Zanzibar, juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# 'Mafunzo kutumia zana hujenga kumbukumbu'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali, imesema kusomesha kwa kutumia zana za kufundishia husaidia wanafunzi kujenga kumbukumbu ya muda mrefu.

Akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Naibu Waziri wa wizara hiyo, Simai Mohammed Said, alisema ili kumjenga mwanafunzi ni muhimu kutumia vifaa hivyo, ambavyo husaidia kupata ufaulu wa daraja la juu.

Aliyasema hayo wakati wa maonyesho ya sita ya zana za kufundishia na kujifunza kwa wanafunzi wa fani ya ualimu wa Chuo cha Taifa (SUZA).

Alisema, kutumia zana za kufundishia na mbinu shirikishi kwa wanafunzi huleta uhusiano mzuri baina ya walimu, wanafunzi na mada iliokusudiwa kusomeshwa.

Simai alisema kutumia vitendea kazi ipasavyo kwa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi, kutawawezesha wanafunzi kufikia lengo la kujifunza kwa ufanisi mkubwa.

Hata hivyo, aliwataka wanafunzi kuwaheshimu walimu wao ambao ndio chimbuko la wataalamu wa fani zote.

Akisoma risala kwa niaba ya walimu wenzake, Yunus Mwalimu, alisema lengo la kuweka maonyesho hayo ni kuwajenga wanafunzi waweze kutumia zana na kufundisha kwa vitendo wakati wakiwa darasani.

Kwa upande wao wanafunzi walioshiriki walisema maonyesho hayo huonyesha ubunifu wao wa hali ya juu wanaotumia ili wafikie lengo la kutoa elimu bora kwa wanafunzi wenzao.

Maonyesho hayo ya sita yamejumuisha masomo mbalimbali yakiwamo lugha, sayansi na hesabati na ujumbe wa mwaka huu ni 'Walimu zana wakitumia, wanafunzi hawatasinzia'.

# Uadilifu, nidhamu kutumikia wananchi muhimu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MJUMBE wa Bodi ya Shirika la Bandari Zanzibar, Khalfan Othman, amewataka wafanyakazi wa shirika hilo kufanya kazi kwa uadilifu na nidhamu wanapotumikia wananchi.

Aliyasema hayo katika hafla ya kuwaaga wafanyakazi sita waliomaliza muda wao wa utumishi katika shirika hilo, iliyofanyika Malindi, Mjini Unguja.

Alisema Shirika la Bandari linategemewa na serikali kwa kufanya kazi zenye uzalishaji na viwango, hivyo aliwaomba wakuu wa idara na vitengo kuhakikisha wanafanya kazi kwa nidhamu, uaminifu na upendo.

Alisema, jambo la msingi kwa wafanyakazi wa shirika hilo kufuata nyayo za wastaafu ambao walikuwa wakifanya kazi kwa kujituma katika kuendesha shirika hilo.

Mjumbe huyo, alisema wastaafu hao wameacha pengo kubwa katika bandari, hivyo wale ambao watakamata nafasi hizo wazitendee haki kama walivyozitendea haki wastaafu hao.

Akizungumzia utaratibu wa kuwazawadia wafanyakazi hao waliomaliza muda wao wa utumishi, alisema ni mfumo mzuri unaonyesha wazi kuwa shirika linawajali wafanyakazi wake kipindi chote cha utumishi wao.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hilo, Abdalla Juma, aliwataka wafanyakazi wanaoendelea na utumishi kufanya kazi kwa bidii kwa kufika kazini mapema ili kuhakikisha huduma wanazozitoa zinakuwa na viwango.

Aliwashauri wafanyakazi wanaostaafu kutambua kuwa kumaliza muda wa utumishi sio mwisho wa maisha na kuwaomba pale wanapohitajika kuendeleza ushirikiano walionao tangu wakiwa wafanyakazi wa shirika hilo.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi Shirika la Bandari (COTWU), alisema wafanyakazi hao wameacha kumbukumbu kubwa ya kuendelezwa yale waliyoyaacha kwa maendeleo ya shirika lao ikiwa kama ni taasisi ya serikali.

Alitumia muda huo kuwaomba wafanyakazi ambao wanaendelea na utumishi wao kuhakikisha wanafanya kazi kwa nidhamu, uaminifu na upendo.

Aliwaomba wastaafu hao kutumia vizuri pesa zao za kiinua mgongo kwa kuwekeza ili kuwasaidia katika maisha yao ya baadaye.

Akizungumza kwa niaba ya wastaafu wenzake, aliyekuwa Mkurugenzi Ufundi, Maneno Mohammed Maneno, alipongeza uongozi wa shirika hilo kwa kuwa kitendo hicho cha kujumuika pamoja katika hafla ya kuwatunuku zawadi kimeonyesha dhahiri kuwajali wafanyakazi wake na kuahidi kuwa wapo tayari kushirikiana watakapohitajika wakati wowote.

# Majaliwa awasha moto ujenzi jengo TRA

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema jengo la kituo cha pamoja cha huduma za forodha kilichopo kwenye mpaka wa Tanzania na Kenya eneo la Horohoro, Tanga ambacho ujenzi wake umegharimu Sh. bilioni 7.6, limejengwa chini ya viwango.

Aidha, ameagiza Ofisa Miliki wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Haruna Sumwa, mkandarasi aliyejenga jengo hilo pamoja na wote waliohusika na ujenzi huo wafike ofisi ya Waziri Mkuu mjini Dodoma Machi 11, mwaka huu.

Waziri Mkuu aliyasema hayo jana katika ziara ya kikazi wilaya ya Mkinga mkoani Tanga, ikiwa ni mwendelezo wa ziara ya kikazi mkoani humo.

"Kuta tayari zimeshaanza kuvimba, kwa nini majengo ya TRA yanajengwa kwa kiwango cha chini na kwa nini mmeruhusu majengo haya yatumike," amehoji Waziri Mkuu.

"Hapa ni sura ya nchi ni lazima majengo yawe katika hali nzuri, haiwezekani mgeni anaingia na kuhudumiwa katika jengo chakavu, tutachukua hatua kwa yeyote aliyehusika, hizi ni fedha za umma lazima zitumike vizuri."

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Mkinga, Yona Maki, alisema ujenzi wa jengo hilo ulianza Julai mwaka 2011 hadi Septemba mwaka 2014 na lilianza kutumika Agosti mwaka 2015 likiwa na taasisi 16 za serikali zinazofanyakazi.

Alisema kituo hicho kinakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo ukosefu wa nyumba 62 za watumishi, majisafi na salama pamoja na upungufu wa watumishi. Majukumu ya kituo hicho ni pamoja na kusimamia, kudhibiti uingiaji na utokaji wa raia wa Tanzania na wageni, kufanya doria na misako hasa kwenye vipenyo ambako wale wasiopenda kufuata taratibu hupenda kutumia.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu ameendelea kusisitiza watu wote wanaoingia nchini kupitia mipaka mbalimbali wapimwe afya zao, ili kulinda Taifa na maambukizi ya magonjwa mbalimbali ikiwamo homa ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona.

"Lazima tulinde nchi yetu katika kupambana na kuzuia magonjwa mbalimbali kwa kuhakikisha watu wote wanaingia nchini wawe salama."

Aidha, Waziri Mkuu amewaagiza viongozi wa Jeshi la Polisi mkoani Tanga kuimarisha doria katika maeneo ya mpakani ikiwa ni pamoja na kukagua maroli kwa kuwa yanahusika na ubebaji wa wahamiaji haramu.

Waziri Mkuu amewataka wananchi kutojihusisha na biashara haramu ya dawa za kulevya kwa kuwa madhara yake ni makubwa kwa jamii na Taifa kwa ujumla.

Amesema wananchi wakatae kutumika katika kupitisha dawa za kulevya na atakayekamatwa hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake. "Usikubali gari lako likatumika kubeba wahamiaji haramu wala dawa za kulevya kwani ukikamatwa linataifishwa."

Waziri Mkuu amesema mwaka jana dawa za kulevya aina ya heroine gramu 746, bangi kilo 485, mirungi kilo 880 zilipitishwa katika wilaya hiyo kiwango ambacho ni kikubwa, hivyo amemwagiza Mkuu wa Wilaya aimarishe doria.




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akitoka kwenye jengo la Kituo cha Pamoja cha Huduma za Forodha cha Horohoro mkoani Tanga jana. Kulia kwake ni Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu. **PICHA: OWM**

# Tisa mbaroni tuhuma uhujumu uchumi

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, imewafikisha mahakamani watuhumiwa tisa kwa tuhuma za kuisababishia hasara ya zaidi ya Sh. milioni 16.7 Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Masasi-Nachingwea (Manawasa).

Watuhumiwa hao walifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Masasi jana kwa mashtaka tofauti tofauti, likiwamo ya kughushi nyaraka za serikali na kujipatia fedha kinyume cha utaratibu na kosa la uhujumu uchumi.

Mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi, Rehema Iddi, Mwendesha Mashtaka wa Takukuru Wilaya ya Masasi, Cecilia Mshiko, alieleza kuwa watuhumiwa hao wanadaiwa kutenda makosa hayo Desemba mwaka 2016.

Alidai kuwa watuhumiwa saba kati yao wanadaiwa kujipatia fedha za malipo ya fidia kupitia mradi wa maji ya Mbwinji Masasi-Nachingwea kiasi tofauti tofauti kila mmoja huku wakitambua wao wasio walengwa wa malipo ya fedha hizo.

Aidha, aliieleza mahakama kuwa watuhumiwa wawili wa kesi hiyo ni watumishi wa serikali ambao walikuwa ni watendaji wa vijiji kata ya Mwena Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, ambao ni Shamiro Majani na Keven Milanzi.

Alidai kuwa mtuhumiwa Majani anakabiliwa na shtaka la kutumia nyaraka kwa lengo la kumdanganya mwajiri wake ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri.

Alieleza kuwa kosa hilo ni kinyume cha kifungu (22) cha Sheria ya Kupambana na Kuzuia Rushwa Namba 11 ya Mwaka 2007 na kwa upande wa Milanzi anashtakiwa na kosa la kughushi nyaraka kinyume cha kifungu cha (333) 335 A na 337 cha sheria ya kanuni ya adhabu namba 16 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002.

Mshiko alidai watuhumiwa saba wanakabiliwa na kosa la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu kinyume cha kifungu namba 2002 cha sheria ya kanuni ya adhabu ya mwaka 2002.

Alidai kuwa kosa la tisa ni la kuisababishia Manawasa hasara ya fedha zaidi ya Sh. milioni 16, linalowakabili watuhumiwa wote na wanadaiwa kulitenda Desemba mwaka 2016 wakati wa usanifu wa mradi huo na kulipwa fedha ambazo wao hawakuwa walengwa.

"Makosa haya kwa watuhumiwa hawa yanapatikana katika Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi katika vifungu vya (57) 1 na kifungu cha (62) cha Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi," alisema Mshiko. Watuhumiwa wote walikosa dhamani kutokana na mahakama hiyo kueleza haina uwezo wa kusikiliza kesi za makosa ya uhujumu uchumi. Kesi hiyo iliahirishwa hadi Machi 23, mwaka huu.

# Alalamikia uchafu sokoni

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAFANYABIASHARA wa soko la Kambarage Manispaa ya Shinyanga, wako hatarini kutokana na ghuba la kuhifadhia uchafu kujaa, huku inzi wakienda kwenye biashara zao hali ambayo wamedai inatishia usalama wa maisha yao.

Wakizungumza na Nipashe sokoni hapo, walisema uchafu huo ni tishio kwa afya zao ikiwamo kuathiri biashara zao kwa kukosa wateja wanaonunua nyama.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Yusuf Justine Mgen,i anayeuza nyama, aliiomba serikali kuondoa uchafu huo ambao kwa sasa una takribani wiki tatu haujazolewa, hali ambayo ni hatari kwa afya zao. "Uchafu huu una zaidi ya wiki tatu sasa umejaa na haujazolewa, na kila mwezi tunatoa Sh. 2,000 kwa ajili ya uzoaji wa takataka, lakini tunashangaa hauzolewi na inzi sasa hivi wanatoka kwenye uchafu huo wanaingia kwenye biashara zetu, kama unavyoona inzi walivyo kwenye nyama zangu," alisema Mgeni na kuongeza:

"Dampo hili kwa sasa limekuwa kero na kutishia afya zetu na hata kutukosesha wateja, mfano sisi wafanyabiashara wa kuuza nyama mteja akija na kukuta inzi juu ya nyama hawezi kununua anaondoka, hali ambayo inaathiri pia biashara zetu licha ya kutishia usalama wa maisha yetu."

Naye Mwenyekiti wa soko hilo la Kambarage, Seif Mtete, alisema uchafu huo umekuwa kero sokoni hapo na wamekuwa wakifuatilia ili uzolewe, lakini wanaambiwa kuna uhaba wa vifaa vya kuzolea taka na hivyo kukwamisha uchafu huo kutozolewa na kuendelea kurundikana kwenye soko hilo.

Ofisa Afya wa Kata ya Kambarage, Costansia Michael, alikiri kuwapo na uchafu kwenye soko hilo na la Nguzo Nane, na kueleza changamoto iliyojitokeza ni kuwapo kwa uhaba wa vifaa vya kuzolea taka, huku akibainisha uchafu huo utazolewa leo.

HABARI KIMATAIFA

# Rais apinga wafungwa 5,000 kuachiwa

**KABUL,** Afghanstan

RAIS wa Afghanistan, Ashraf Ghani amesema kuwa serikali yake haitaunga mkono kuwaachilia wafungwa wa Taliban kama ilivyoelezwa kwenye makubaliano waliofikia na Marekani na wanamgambo hao.

Chini ya makubaliano hayo ya kihistoria yaliyofikiwa Jumamosi hii Qatar, wafungwa 5,000 wa Taliban wataachiliwa huru katika mabadilishano ya raia karibia 1,000 wa serikali wanaozuiliwa kufikia Machi 10.

Ghani (pichani chini) alisema kuachiliwa kwa wafungwa namna hiyo hakuwezi kufanyika kabla ya mazungumzo, bali ni lazima hilo liwe sehemu ya majadiliano.

Makubaliano ya Marekani na Taliban yanajumuisha kuondoka kwa majeshi ya Marekani nchini Afghanistan kwa awamu.

Kwa mabadilishano, kundi hilo la Kiislamu lenye msimamo mkali lilikubali kufanya mazungumzo na serikali ya Afghanistan.

Makubaliano hayo pia yalihakikisha kuwa Taliban inazuia kundi la al-Qaeda na makundi mengine yoyote yenye msimamo mkali kuendesha shughuli zake katika maeneo wanayodhibiti.

Marekani iliingilia Afghanistan wiki kadhaa baada ya shambulio la Septemba 2001, New York na kundi la al-Qaeda, wakati huo likiwa na makao yake Afghanistan.

Kundi la Taliban lilitimuliwa madarakani, lakini likawa kikosi kikubwa cha wanamgambo kiasi kwamba 2018, lilikuwa linaendesha shughuli zake kwa zaidi ya theluthi mbili ya maeneo nchini humo.

Katika kipindi cha saa 24 baada ya makubaliano kufikiwa Doha, Rais wa Afghanistan aliwaambia wanahabari katika mji wa Kabul kuwa: "Kusitisha vita taratibu kutaendelea kwa lengo wa kufikia makubaliano ya kusitisha kabisa vita. Lakini hatudhamirii kuachilia huru wafungwa 5,000."

Alisema: "Hatua hii ni haki ya raia wa Afghanistan na kupenda kwao. Huenda kukajumuishwa kwenye ajenda ya mazungumza na pande zote, lakini haliwezi kutimizwa kabla, Mfungwa yeyote kuachiliwa huru siyo kwa idhini ya serikali ya Marekani bali ni kwa mamlaka ya serikali ya Afghan".

Wataliban wapatao 10,000 waliokamatwa wanazuiliwa na Afghanistan. **BBC**



# Wageni walioingia na corona Uganda watengwa

**KAMPALA,** Uganda

RAIA wanne wa kigeni waliowasili nchini Uganda na dalili za virusi vya corona wametengwa katika hospitali ya Entebbe, Waziri wa Afya amethibitisha.

Bila ya kutaja uraia wao, Ofisa Uhusiano wa Waziri wa Afya, Emmanuel Ainebyoona, alisema kuwa raia hao wamechukuliwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Entebbe.

"Sampuli ya vipimo vyao vimepelekwa katika kituo cha utafiti wa virusi nchini humo (UVRI). Na tutautaarifu umma," gazeti la Daily Monitor lilieleza.

Wizara ya Afya Uganda imewataka wananchi kuwa watulivu na kufuata hatua za kujikinga na ugonjwa wa corona kwa sababu hakuna uthibitisho wa kuwa virusi hivyo vimeingia nchini humo.

**Maofisa wa afya wa China walisema kuna maambukizi mapya 202 ya maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona na kufanya idadi ya walioambukizwa kufikia 80,026.**

Uganda inakuwa nchi ya nne kupokea wageni wenye virusi vya corona baada ya Misri, Algeria na Nigeria. Aidha, mwandishi wa Shirika la utangazaji la BBC nchini Uganda alisema kuwa Waziri wa Afya nchini humo, alitoa agizo kwa wageni wanaotoka katika nchi zilizoathirika na virusi vya corona watengwe kwa muda wa siku 14.

Zaidi ya matukio 85,000 ya ugonjwa wa visuri vya corona yamethibitishwa katika nchi 57 kote duniani huku vifo 3,000 vikithibitishwa, kulingana na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Ugonjwa huo ulianza kuenea katika nchi ya China na sasa umeshasambaa katika nchi mbalimbali za Ulaya na Afrika na kwamba idadi kubwa ya wananchi wameanza kuchukua tahadhari.

Wakati huohuo, Idadi ya vifo vinavyosababishwa na ugonjwa huo imefia watu 3,000, baada ya mamlaka nchini China kutangaza jana kwamba kuna vifo vipya vya watu 42 katika Jimbo la Hubei, katikati mwa China, ambapo ugonjwa huo ulianzia.

Maofisa wa afya wa China walisema kuna maambukizi mapya 202 ya maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona na kufanya idadi ya walioambukizwa kufikia 80,026.

Mlipuko wa ugonjwa huo umesababisha vifo vya watu 2,912 nchini China tangu kuzuka kwake, kulingana na takwimu za serikali. Ugonjwa huo hatari unaendelea kusambaa katika bara la Ulaya. **BBC**




Abiria wakiwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa King Khalid, Riyadh Saudi Arabia, kutoka China na maafisa wa afya wakiwapima kuhakikisha hawana kirusi cha corona. **PICHA: REUTERS**

# Rais atawala siku 5, atangaza kujiuzulu

**BISSAU,** Guinea-Bissau

RAIS wa Bunge la kitaifa, Cipriano Cassama, aliyetawazwa kama rais wa mpito siku ya Ijumaa jioni, ametangaza kujiuzulu wadhifa wake.

Kwa sasa Guinea-Bissau inaendelea kukumbwa na mgogoro baada ya uchaguzi.

Katika taarifa fupi aliyoitoa akiwa nyumbani kwake huko Bissau huku akilindwa na askari wa ECOMIB, Kikosi cha Askari wa Jumuiya ya Kiuchumi ya nchi za Afrika ya Magharibi, ECOWAS, na baadhi ya askari wa Guinea, Cassama alisema: "Usalama wangu uko hatarini".

Alisema kwamba Jumamosi jioni, kuna askari walikuja kuwatafuta walinzi wake. Alisema amefikia hatua ya kujizulu kwa sababu anahofia usalama wake na wa familia yake.

Alisema anataka kuepusha mapigano kwa maslahi ya taifa na raia wa Guinea-Bissau na kulaani kitendo cha jeshi kushikilia kwa nguvu makao makuu ya Bunge la Taifa.

Cassama alitawazwa bungeni Ijumaa jioni na wabunge 52, hasa kutoka chama cha PAIGC. Kabla ya hotuba yake, Teodora Gomes, mjumbe wa kamati kuu ya chama cha kihistoria, alimwomba asiachie madaraka na asitoe tangazo hilo la kujiuzulu.

"Nikiangalia vitisho vya kifo vilivyotolewa dhidi yangu, dhidi ya walinzi wangu, naona kwamba usalama wangu uko hatarini. Nimeamua kuchukua uamuzi huu, kuzuia makabiliano kati ya vikosi kutoka upande wa pili na vikosi ambavyo vinanilinda na pia kuzuia vita, sijui kama naweza kuviita vita vya kiraia au umwagaji damu, " alisema Cassama na kuongeza:

"Kwa hivyo nchi yetu inakabiliwa na mgogoro mpya wa baada ya uchaguzi, mgogoro ambao bado haujatatuliwa kati ya wagombea wawili, Umaro Sissoco Embalo na mpinzani wake, Domingos Simões Pereira, ili tuweze kujua mshindi halali," alisema Cipriano.

Waziri Mkuu wa Guinea-Bissau, Aristides Gomes, ambaye alifutwa kazi na Umaro Sissoco Embalo Ijumaa, pia amelaani vitisho vinavyotolewa dhidi yake. **RFI**

RIPOTI MAALUM - 2

# Shule yenye wanafunzi 4 wasomao chini ya mti

## ■CAG aanika hali mbaya kitaifa
## ■Bunge 'lalia' uhaba wa walimu

**SEHEMU ya kwanza ya ripoti hii jana, iliangazia kwa kina shida zinazowapata wanafunzi wa Shule ya Msingi Mgowelo wilayani Kilolo mkoani Iringa kutokana na hali mbaya ya miundombinu ya shule yao na uhaba mkubwa wa walimu. Endelea na sehemu hii ya mwisho, ikiainisha mustakabali huo katika sura pana:**

OFISA Mtendaji wa Kijiji, Antoni Kiwonde, na Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Bakari Mtalula, mbali na kukiri hali mbaya ya shule hiyo na hatua waliyochukua kukusanya michango kutoka kwa wanakijiji kuboresha mapengo ya mahitaji kama vile vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo, walidokeza kikwazo kingine kilicho upande wao.

Viongozi hao kila mmoja alilalamika kuwapo mwamko mdogo kwa baadhi ya wanakijiji, ambao hawapo mstari wa mbele katika uchangiaji miradi ya kuboresha huduma shuleni kwa watoto wao.

Mtalula alifafanua zaidi: "Sisi Serikali ya Kijiji kwa kushirikiana na wanakijiji tupo katika harakati ya kuchangisha pesa kwa ajili ya kununua vifaa vitakavyosaidia ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa, tumefanikiwa kufyatua matofali zaidi kwa ajili ya ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa.

"Sasa tunasubiri msimu wa mavuno kuanzia mwezi wa tano (Mei) hadi wa saba (Julai) ili tuendelee kuchangisha pesa za ujenzi huo."

Ziaka Geda, mkazi wa Mgowelo, iliko shule hiyo, aliiomba serikali kutatua matatizo yanayoikabili shule hiyo ili watoto wapate haki yao ya msingi ya elimu.

"Yaani msimu huu wa mvua unakuta mtoto anarudi madaftari yameloa, watoto wameshindwa kuendelea na masomo na ukiuliza tatizo nini, mtoto anakwambia 'tulikuwa tunasoma nje huku mvua inanyesha'.

"Hivi kweli, hata wewe ndugu mwandishi, unaweza kusoma huku mvua inakunyeshea? Haya, kukiwa hakuna mvua, hilo jua ndiyo usiseme na kama unavyojua, jua la huku kijijini, yaani watoto wanapata tabu sana. Serikali ijitahidi kuwaokoa watoto hawa," alishauri.

Lenea Mnyaonga, mwanafunzi wa darasa la sita katika shule hiyo, alibainisha kuwa baadhi ya siku hawaoni mwalimu akiingia darasani kufundisha, sababu kubwa akiitaja kuwa ni uhaba wa walimu unaoikabili shule yao.

**HALI ILIVYO KITAIFA**

Wakati hali ikiwa hivyo wilayani Kilolo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), anabainisha kwamba kuna uhaba mkubwa wa samani na miundombinu katika shule mbalimbali nchini.

Katika ripoti yake mwaka 2015/16, CAG alisema hali ni mbaya zaidi katika shule za msingi kutokana na miundombinu na samani zake kutokuwa katika hali nzuri na kutokidhi matakwa ya viwango vya ubora.

CAG alibainisha kuwa ukaguzi wake kuhusu miundombinu ya shule za msingi, ulibaini udahili wa wanafunzi umeongezeka, lakini miundombinu ikiwa ovyo na isiyoendana na idadi ya wanafunzi.

Alisema hali ya ukaaji dasarani kwa shule za serikali ni ya wastani wa wanafunzi 77 badala ya 40 katika darasa moja inavyotakiwa kisera.

CAG alisema huduma za choo nazo ni tatizo, akibainisha kuwa wakati kiwango kinachotakiwa kisera ni wanafunzi wa kiume 25 na wanafunzi wa kike 20 kwa tundu moja la choo, Tanzania kwa sasa tundu moja linatumiwa na wavulana 57 huku wasichana 56 wakitumia tundu moja.

Vilevile, katika taarifa yake bungeni wakati wa kikao cha Bunge la Bajeti Mei 22, 2017, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, ilibainisha kuwa Tanzania inakabiliwa na uhaba wa walimu 252,693 wa shule za msingi na sekondari.

Aliyekuwa mjumbe wa kamati hiyo, Mbunge wa Nzega Mjini, Hussein Bashe (sasa Naibu Waziri wa Kilimo), aliliambia Bunge kuwa kati ya walimu hao wanaohitajika, 182,899 ni wa shule za msingi na 69,794 wa sekondari.

**AHADI YA SERIKALI**

Mwishoni mwa mwaka jana, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha, aliambia Nipashe kuwa serikali imechukua hatua kukabiliana na uhaba wa walimu uliopo nchini kwa kuhakikisha inaajiri walimu 18,000 kwa mwaka wa fedha uliopo na inatarajia kuajiri wengine 16,000 mwanzoni mwa bajeti ijayo.

Ole Nasha alifafanua undani wa chanzo cha uhaba uliopo wa walimu kitaifa kwa kiasi kikubwa umechangiwa na hatua ya serikali kuwafuta kazi watumishi waliokosa sifa baada ya kufanyika uhakiki wa watumishi hewa na wenye vyeti feki, walimu wakiwa miongoni mwao.


Katika kipindi hicho cha uhakiki, serikali isitisha kutoa ajira kwa watumishi wa kada karibu zote, isipokuwa chache zinazogusa masuala nyeti ya kitaifa.

Naibu Waziri huyo pia alitoa angalizo kwamba kwa mujibu wa taratibu, mamlaka ya wizara yake ni kuibua madai na wenye mamlaka ya kuajiri walimu ni Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), lakini alisisitiza matarajio ya utekelezaji wa suala hilo la ajira kwa walimu.



Hali ya usomaji ilivyo kwa wanafunzi wa madarasa ya awali katika Shule ya Msingi Mgowelo wilayani Kilolo mkoani Iringa. **PICHA: HALFAN CHUSI**

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA


## PASSPORT IMEPOTEA



**BRIAN VIRGIL SWAI** anatangaza kupotelewa na Hati ya Kusafiria (Passport) yenye namba **TAE 041659.** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Makao Makuu Dar es salaam mwaka 2018. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Control **No. 9910811893000.**

115652002

## VYETI VIMEPOTEA



**JUSTINE KUBOZA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0185-0014** kilichotolewa na **SENGEREMA SEMINARY** mwaka 2009. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0823-0539** kilichotolewa na THAQAAFA SEKONDARI mwaka 2012. Cheti cha Chuo chenye namba B.Ed. **(SPED) 00000639** kilichotolewa na University of Dodoma (UDOM) mwaka 2016. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kwenye kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi: **MWA/IGD/RB/600177/2019.**

115652102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI**
**IDARA YA UHAMIAJI**

**YAH: KUOMBA URAIA**



**Bw IKRAM ULLAH, S.L.P 483 TANGA**

Tangazo limetolewa kwamba, mtu ambaye picha yake imetolewa hapo juu anaomba uraia wa Tanzania kwa Mh. Waziri wa mambo ya Ndani ya Nchi. Mtajwa kwa sasa ni raia wa **PAKISTANI** na anatokea nchi ya **PAKISTANI** pia anajishughulisha **AMEAJIRIWA KATIKA KAMPUNI.** Mtajwa amekuwepo hapa nchini tangu 2010 pamoja na kuishi **TANZANIA** Pia amewahi kuishi **PAKISTANI** kwamba mtu yeyote mwenye taarifa au sababu kwanini mwombaji asipewe uraia apeleke sababu hizo kwa maandishi yaliyosainiwa kwa kamisha Jenerali wa Uhamiaji, **S.L.P 512** Dar es Salaam. **Kumb. DN TA/TP/4318**

**kny. KAMISHNA JENERALI WA UHAMIAJI**

115652502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No; 58/2020**

**Ombi la JOHN KISEGE MWANGINDO Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu CHRISTOPH JOHN MWANGINDO.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 24/03/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 02/03/2020.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

115652302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;43/2020**

**Ombi la MARTIN JOHN MZUANDA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu PAULO MATHIAS MZUANDA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 05/03/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 24/02/2020.

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
YA MWANZO MJINI
MOROGORO

115652402

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**ALICE RWEGELELA AUGUSTINE**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya Boxer yenye namba za usajili MC 960 BSW. Amepoteza kadi hiyo akiwa Katoma Bukoba Vijijini. Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/183317/2020.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi, au awasiliane naye kwa namba **0789-981212.**

15652202


Uza, Chenye Thamani Kubwa

Kwa Kutangaza Nasi Kwa

Bei Poa Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI MICHEZO

# STERLING: MAN CITY TUNATAKA 'NDOO' 3



**MANCHESTER,** England

RAHEEM Sterling amesema Manchester City "wamejizatiti" kumaliza msimu wakiwa na mataji matatu baada ya kuifunga Aston Villa 2-1 kwenye fainali ya Kombe la EFL, Jumapili na kubeba 'ndoo' ya kwanza.

City ilitwaa taji hilo kwa mwaka wa tatu mfululizo na kwa mara ya tano katika misimu saba shukrani kwa mabao ya Sergio Aguero na Rodri yaliyofungwa ndani ya dakika 30 za kipindi cha kwanza pale kwenye dimba la Wembley.

Bao la kichwa la Mbwana Samatta liliwapa matumaini Villa kurudi mchezoni, lakini hadi dakika ya 90 matokeo yalibakia kuwa 2-1.

Sterling alikubali kwamba kikosi chao hakina matumaini ya kuliziba pengo la pointi 22 za vinara wa Ligi Kuu ya England, Liverpool, lakini mshambuliaji huyo anaona kwamba wanaweza kubeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na lile la FA.

Mabingwa hao watetezi wa EPL waliifunga Real Madrid 2-1 kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora, na kesho, Jumatano watakwenda kucheza na Sheffield Wednesday kwenye mchezo wa raundi ya tano ya Kombe la FA.

"Mbio za Ligi Kuu ni ngumu," alisema akiiambia Sky Sports . "Tumeshinda taji moja na bado tupo kwenye mbio za mataji mawili hivyo, tumejipanga na tupo tayari kwa ushindani huo.

"Tunachotakiwa ni kujipanga na ndio tunachokifanya hivi sasa. Ni ngumu kushinda kwa miaka mitatu mfululizo na hicho ndicho tulichokifanya tunachotakiwa kufanya ni kuendelea kupambana kushinda mataji."

# Klopp aitaka Liver sasa kuanza upya

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amewataka Liverpool "kuanza upya" baada ya umwamba wao wa kutofungwa kwenye Ligi Kuu ya England kumalizwa na Watford.

Liverpool walikutana na kichapo cha mabao 3-0 pale kwenye dimba la Vicarage Road Jumamosi, wakimaliza mechi 44 bila kufungwa kwenye Ligi Kuu.

Vijana hao wa Klopp wanarudi tena dimbani leo Jumanne, wakati watakapowavaa Chelsea kwenye raundi ya tano ya Kombe la FA.

Kocha huyo raia wa Ujerumani sasa amewataka Liverpool, ambao wanaongoza msimamo wa ligi kwa pointi 22, kujipanga upya kwa ajili ya miezi iliyobaki kumalizika kwa ligi hiyo.

"Wakati mwingine kuanza upya ni muhimu. Hivyo sioni kitu chochote hasi," alisema Klopp akinukuliwa na magazeti ya Uingereza.

"Kuna wakati kama hauko vizuri vya kutosha, unatakiwa kuangalia matokeo yake. Unayaona si mazuri– nini kinatokea? Kuanza upya.





# Grealish apagawa Villa kutobeba EFL

**LONDON,** England

JACK Grealish amejielezea yeye mwenyewe kama "amepagawa" baada ya Aston Villa kupoteza kwa mabao 2-1 kwenye fainali ya Kombe la EFL dhidi ya Manchester City katika Uwanja wa Wembley juzi, Jumapili.

Grealish alikuwa na matumaini ya kukifunga kikosi hicho cha Pep Guardiola, wakati krosi ya Bjorn Engels ilipomfikia Mbwana Samatta aliyefunga kwa kichwa na kufanya matokeo kuwa 2-1.

"Nimepagawa, lakini tulicheza dhidi ya timu bora Ulaya kwa dakika zote," alisema akiiambia Sky Sports.

"Walikuwa na nafasi na wakazitumia, kama ambavyo tulijua kwamba wangetumia kila nafasi ambayo ingepatikana.

"Bao lao la ushindi halikupaswa kukubaliwa - haikuwa kona. Kwani Gundogan alikuwa nje ya uwanja wakati akipiga mpira.

"Tulitaka maelezo wakati wa mapumziko, lakini hakuweza kutupatia. Klabu kama sisi ambao hatujashinda chochote kwa muda mrefu na tunapoteza kwa bao ambalo halikupaswa kuruhusiwa, haikuwa sawa.

"Tunajivunia kila mmoja. City wapo timu mbili au tatu bora Ulaya. Mara zote tulijua kwamba utakuwa mchezo mgumu kwetu na sasa akili yetu ipo kwenye ligi."

## HABARI MICHEZO

# Mourinho akataa kumlaumu Dele Alli

**LONDON,** England

JOSE Mourinho hatamlaumu Dele Alli kwa kichapo cha Tottenham licha ya kukubali kwamba, kiungo huyo alikosa nafasi nzuri dhidi ya Wolves.

Alli alicheza kama mshambuliaji wa kati kwenye kichapo cha 3-2 nyumbani dhidi ya Wolves Jumapili, huku Harry Kane na Son Heung-min wakiwa nje kuuguza majeraha, na Spurs wakapoteza mchezo wao wa tatu mfululizo kwenye mashindano yote.

Huku Tottenham ikiwa mbele kwa mabao 2-1 kipindi cha pili, mchezaji huyo wa kimataifa wa England alipiga kichwa akiunganisha pasi ya Ben Davies, lakini kilitoka nje.

Dakika mbili baadaye, Diogo Jota alisawazisha na Raul Jimenez akafunga la ushindi, lakini Mourinho anahisi Alli hakuwa na bahati.

"Mechi ilikuwa rahisi na tulikaribia kushinda," alisema Mourinho, ambaye pia alibainisha matokeo hayo si haki kwa wachezaji wake, akiwaambia waandishi wa habari.

"Ukiangalia kwa makini, unaona wazi kabisa kwamba tulikosa nafasi kubwa ya kufunga bao zuri na tungefanya ubao usomeke 3-1. Hayo ndio magumu ya mpira wa miguu, na hakuna wa kumlaumu.

"Ben alikuwa kwenye nafasi nzuri, krosi ilikuwa nzuri na Dele alikiambia na hakuweza kuufikia vizuri ule mpira.

"Kwa uhakika yupo vizuri kwa kuruka ingawa si mshambuliaji. Ni mpigaji mzuri wa kichwa. Hakuwa na bahati."




**MCHEZAJI BORA...**




Mkuu wa Mauzo wa Kanda ya Dar es Salaam na Pwani wa Vodacom Tanzania PLC, George Venant (kushoto), akimkabidhi Mchezaji wa timu ya KMC, Sadallah Lipangile, mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni moja baada ya kuibuka Mchezaji Bora wa Mwezi Februari wa Ligi Kuu ya Vodacom Tanzania Bara. Makabidhiano hayo yalifanyika wakati wa mchezo wa Ligi Kuu kati ya KMC na Simba uliofanyika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam juzi, Simba ilishinda mabao 2-0. Katikati ni Kiongozi Msimamizi wa Vodacom (team leader), Felician Benedict. **NA MPIGAPICHA WETU**

# RAMOS AMJIA JUU PIQUE



**MADRID,** Hispania

SERGIO Ramos amembwatukia Gerard Pique juu ya shutuma zake kwa Real Madrid, akisema amesaini kushinda kila mchezo wa El Clasico hata kama akicheza vibaya kama beki huyo wa Barcelona alivyobainisha.

Mabao ya Vinicius Junior na Mariano Diaz ya kipindi cha pili yaliiwezesha Madrid kupaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ya Hispania dhidi ya Barca, Jumapili.

Lakini kiwango chao hakikumvutia Pique kwani beki huyo wa Barca alisema katika kipindi cha kwanza "Madrid ilikuwa mbovu" na hakuwahi kukutana na timu kama hiyo kwa kipindi chote alichokwenda kucheza pale Santiago Bernabeu.

Lakini nahodha wa Madrid, Ramos amemjibu kwa kusema kwamba yeye ana furaha kushinda kila Clasico kama ilivyotokea.

"Kila mtu ana mawazo yake na yanaheshimiwa. Nilisajiliwa hapa kushinda Clasico zote bila kujali nitacheza vibaya kwa kiasi gani," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Kipindi cha kwanza kilikuwa tofauti. Mambo hayakwenda vizuri na hatukucheza mpira kwa staili yetu.

"Tulionekana kutokuwa fiti, lakini jambo la msingi ni kwamba tulion doka na ushindi baada ya dakika 90."

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# VINICIUS AMPIKU MESSI EL CLASICO

## Ni kwa kuwa kinda aliyecheka na nyavu akiwa na umri mdogo zaidi, Zidane akunwa...

**MADRID,** Hispania

STRAIKA kinda wa Real Madrid, Vinicius Junior, amempiku mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi kama mchezaji kinda zaidi kuwahi kufunga kwenye El Clasico katika karne hii.

**Kwa umri wake wa miaka 19 na siku 233, Vinicius aliachia shuti lililozama kimyani mwa lango la Barcelona katika dakika ya 71 na kuifanya Madrid kuwa mbele katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Santiago Bernabeu juzi, Jumapili.**

Kwa bao hilo, mshambuliaji huyo sasa anampiku nyota wa Barca, Messi, ambaye wakati anafunga bao lake la kwanza Clasico Machi 2007, alikuwa na miaka 19 na siku 259, amkimzidi Vinicius kwa umri wa siku 26 zaidi.

Messi alikuwa mhimili muhimu wakati Madrid wakiwapiku mabingwa hao, Barca kwa pointi moja zaidi na kukwea kileleni mwa msimamo wa LaLiga, katika mechi hiyo ambayo mtokea benchi, Mariano Diaz alikamilisha ushindi wa mabao 2-0 kwa Madrid katika dakika ya 90.

Kocha Mkuu wa Real Madrid, Zinedine Zidane, akizungumzia ushindi huo, amewapongeza wachezaji wake kwa kuweza kusahau kipigo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Manchester City na kushinda dhidi ya Barcelona katika LaLiga El Clasico.

Presha katika mchezo huo ilikuwa zaidi kwa Madrid kufuatia Jumatano kupoteza kwa mabao 2-1 dhidi ya Manchester City kwenye mechi ya mkondo wa kwanza ya hatua ya 16-Bora ya Ligi ya Mabingwa.

Madrid iliruhusu mabao mara mbili katika dakika 12 za mwisho dhidi ya Man City, hata hivyo, kikosi hicho cha Zidane kiliweza kusahau machungu hayo na kuweza kurejea mchezoni kwa kushinda 2-0 dhidi ya Barca juzi.

Zidane alielezea furaha yake kwa kuwaambia wanahabari: "Majibu leo yamekuwa muhimu. Chumba cha kubadilishia hakigusiki. Ilikuwa wiki ya kuchanganya, lakini tulijiandaa kwa mchezo huu vizuri. Hiyo ina maana wachezaji wapo ndani na wanataka.

"Tulicheza dakika 78 vizuri sana na mwishoni tulipoteza. Leo tumeshinda kucheza vizuri kuanzia mwanzo hadi mwisho. Tunahitaji kushikilia kile tunachoamini, lakini tunajua kwamba itakuwa vigumu hadi mwishoni. Tunahitaji kujizatiti wenyewe kila saa tunapocheza.

"Tulistahili ushindi kwa sababu kila kitu tulifanya kwa kujilinda na kutibua," Zidane aliongeza. "Kipindi cha kwanza usukumaji mashambulizi wetu haukuwa sahihi. Kipindi cha pili tulijizatiti na tulikuwa wazuri mbele."

## ZISIKUPITE

### SANCHO AZIPOTEZEA UTD, LIVER

WINGA wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho, 19, hafikirii kuhusu mustakabali wake wa baadaye licha ya tetesi zinazomhusisha na kujiunga na Manchester United ama Liverpool majira ya joto. ***(Mail)***

### ARTETA KUBINYWA USAJILI

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, anaweza kuwa na bajeti ndogo ya usajili majira haya ya joto kama atakosa nafasi ya kushiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao huku pia kukiwa na taarifa ya hali mbaya ya kiuchumi klabuni hapo. ***(Goal)***

### CORONA YATISHIA SERIE A

MKURUGENZI Mkuu wa Inter Milan, Giuseppe Marotta anadhani msimu wa Serie A pengine unaweza usimalizike kama hawataweza kutafuta suluhisho la kudhibiti janga la virusi vya corona. ***(Mail).***

### SPURS YAJIPANGA KWA FOSTER

TOTTENHAM inajipanga kwenda kumsajili kipa wa Watford, Ben Foster. Kipa huyo raia wa England mwenye umri wa miaka 36, atamaliza mkataba wake na miamba hiyo ya Vicarage Road majira ya joto. ***(Sun)***

### ROMA, SPURS KWA SMALLING

SPURS inataka kuipiku Roma katika kumsajili jumla beki wa Manchester United, Chris Smalling. Beki huyo mwenye umri wa miaka 30, kwa sasa anacheza kwa mkopo klabu hiyo ya Italia. ***(Calciomercato, in Italian)***

### KOULIBALY KITAELEWEKA UTD

MANCHESTER United ipo katika hatua nzuri zaidi ya kumsajili beki wa kati wa Napoli, Kalidou Koulibaly. Nyota huyo wa kimataifa wa Senegal mwenye umri wa miaka 26, pia anawindwa na Real Madrid na Paris St-Germain. ***(Express, via Corriere dello Sport)***

### KUICHANGANYA CHELSEA

CHELSEA inamuwinda Dries Mertens, 31, lakini anakaribia kusaini mkataba mpya na Napoli. Nyota huyo mkataba wake unafikia mwisho majira haya ya joto. ***(Sun)***

### ARTETA KUIBOMOA ATLETICO

MIKEL Arteta anatazama uwezekano wa kumfanya kiungo mkabaji wa Atletico Madrid, Thomas Partey kuwa usajili wake mkubwa tangu atue hapo Arsenal kama kocha mkuu, kwa mujibu wa taarifa. ***(The Sun)***

### WAKALA DE BRUYNE AFUNGUKA

WAKALA wa Kevin De Bruyne, Patrick De Koster hakuhudhuria mechi ya Manchester City ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Real Madrid kwa sababu alihofia angezua cheche za tetesi za usajili. ***(Daily Express)***

### BARCA, REAL KWA HAALAND

REAL Madrid na Barcelona wote watakuwa sokoni kuisaka saini ya straika wa kiwango cha juu duniani majira haya ya joto na Erling Braut Haaland anaongoza katika tetesi za klabu hizo mbili. ***(Daily Express)***

### COLLINS ATEGWA UNITED

MANCHESTER United imeelekeza mitego yake kwa beki wa Stoke City, Nathan Collins, 18. Nyota huyo wa kimataifa wa Jamhuri ya Ireland wa U-21 amecheza mechi 12 katika kikosi cha kwanza cha Potters hao. ***(Sun)***

## HABARI MICHEZO

## Mtibwa yatamba makali kurejea

**Na Shufaa Lyimo**

TUMEZINDUKA! Hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila ambaye ameahidi timu yake imerejea katika kasi mpya baada ya kufanya vibaya katika michezo yake iliyopita ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Katwila aliliambia gazeti hili wamejipanga kufanya vizuri katika mechi zao zinazofuata na hii inatokana na wachezaji wake kufahamu walipokuwa wanakosea.

Alisema kila mechi ya ligi ni ngumu na hii inasababishwa na timu zote kujiandaa vema msimu huu.

Kocha huyo alisema pia michezo ya mzunguko wa pili huwa na ushindani zaidi baada ya kila timu kutaka kuvuna pointi katika kila mechi na kutimiza malengo waliyojiwekea wakati msimu unaanza.

"Sasa hivi timu imeanza kukaa sawa baada ya kutofanya vizuri katika michezo ya nyuma, ninaahidi kurudi kivingine, tunajua bado tunauwezo wa kupata matokeo mazuri," alisema Katwila.

Kocha huyo alisema anatumia nguvu nyingi kuhakikisha timu yake inarudi kwenye mstari na kurudisha heshima waliyokuwa nayo ambayo iliwapa ubingwa wa mashindano ya Kombe la Mapinduzi.

"Kikosi kinaendelea vizuri kwa ajili ya mchezo wetu wa keshokutwa (kesho), dhidi ya Namungo FC, ni mchezo ambao utakuwa na ushindani mkubwa, tunapaswa kuingia kwa tahadhari kubwa," Katwila alisema.

Mtibwa Sugar ambayo iliwafunga Simba katika fainali ya Kombe la Mapinduzi, ilizinduka kwa kupata ushindi wa mabao 2-0, dhidi ya Ndanda FC na kufikisha pointi 27.

## Ramani uwanja wa Dodoma kubadilika

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema inapitia upya ramani ya uwanja wa kisasa wa michezo unaotarajiwa kujengwa jijini hapa.

Akizungumza jijini hapa juzi, Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Dk. Hassan Abbas, alisema Rais John Magufuli aliagiza serikali ijenge yenyewe uwanja huo ambao awali ulitarajiwa kujengwa kwa msaada wa serikali ya Morocco.

"Morocco waliahidi kutusaidia kujenga huu uwanja, lakini umechelewa na Mheshimiwa Rais alishatoa maelekezo uwanja ule tunaujenga wenyewe, kwa sasa wanarekebisha ramani kwa sababu ramani ya kwanza ilikuwa imethibitishwa na wenzetu wa Morocco, kwa hiyo tunarekebisha kidogo ili kufanana na mazingira ya Kitanzania," Abbas alisema.

Pia alisema serikali inatarajia kuandaa mchakato wa kuanza kurekebisha sehemu za kuchezea za viwanja mbalimbali nchini ili viwe katika viwango bora.

# MALALAMIKO YA MAREFA BARA YATINGA SERIKALINI

**Augusta Njoji,** DODOMA

KUFUATIA kuwapo sintofahamu ya uwezo wa waamuzi wanaochezesha mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara ambapo sasa iko katika hatua ya lala salama, serikali imesema imepokea rasmi malalamiko kutoka kwa wadau wa michezo huo hapa nchini.

**Akizungumza jana jijini hapa, Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbas amesema wadau hao wanalalamika kuwapo kwa upendeleo katika baadhi ya michezo unaofanywa na waamuzi ambao wamepewa dhamana ya kuchezesha.**

Abbas alisema malalamiko mengine ni kuwapo tuhuma za upangaji wa matokeo na madai ya rushwa katika baadhi ya mechi na ili kumaliza tatizo hilo, ofisi yake imeliagiza Baraza la Michezo la Taifa (BMT), kufuatilia na kuchunguza kwa kina malalamiko hayo.

Kiongozi huyo alisema ofisi yake inataka kuona malalamiko na kero hizo zinafanyiwa kazi haraka.

"Naamini wiki ijayo (wiki) nitaonana nao (BMT), na kuangalia nini kinaendelea," alisema Abbas.

Sambamba na hilo, alivitaka vyama vya michezo nchini kuwa na utawala bora katika utendaji kazi wao.

"Tunataka utawala bora kwenye vyama vya michezo kama soka, TFF (Shirikisho la Soka Tanzania), ihakikishe kwamba kuna utawala bora zipo kamati sijui za saa 24 zifanye kazi," alisema.

Katibu Mkuu huyo pia alimwagiza Mkurugenzi wa Maendeleo ya Michezo nchini, Yusuph Singo, kuhakikisha kila chama kinakuwa na bajeti ili kujua kiasi cha fedha ambacho inapata kwa kila mwaka.

"Baadhi ya vyama vimekuwa vikipokea ruzuku pamoja na kukusanya tozo na michango mbalimbali, lakini linapokuja suala ya timu ya Taifa huanza kutembeza bakuli la kuomba kwa serikali, pia tupate ratiba ya vyama vyote, umekaa ofisini ghafla anaibuka kiongozi wa timu ya vinyago inaenda sijui wapi, mmekaa kidogo kuna mashindano ya rede Pakstani," aliongeza.

Katika hatua nyingine, kiongozi huyo alisema anaamini mchezo wa watani wa jadi, Simba na Yanga utakaochezwa Jumapili utakuwa mzuri na kuahidi atakuwapo uwanjani kushuhudia mechi hiyo.

**HONGERA...**



Mkuu wa Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Absa Tanzania, Aron Luhanga (kushoto), akimpongeza mmoja wa wakimbiaji wao aliyeshiriki mbio za kilomita 42 wakati wa mashindano ya Kilimanjaro Marathon 2020 pamoja na wakimbiaji wengine mjini Moshi juzi. Absa ilikuwa mmoja wa wadhamini ikigharamia kituo cha kutoa maji ya kunywa na viburudisho kwa wakimbiaji. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Absa Tanzania yaahidi makubwa michezoni*

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

BENKI ya Absa Tanzania imesema itaendelea kudhamini michezo mbalimbali nchini baada ya kufanya hivyo kwa mafanikio katika mashindano ya mwaka huu ya Kilimanjaro Marathon yaliyofanyika katika Uwanja wa Chuo cha Ushirika Moshi moani Kilimanjaro juzi.

Akizungumza wakati wa mashindano hayo mjini Moshi, Mkuu wa Masoko na Mawasiliano wa Absa Tanzania, Aron Luhanga, alisema kama inavyojulikana kuwa Kundi la Benki ya Absa ni mdhamini mkuu wa Ligi Kuu ya Uingereza (EPL) na ile ya Afrika Kusini, hivyo haoni kipingamizi kwa Absa Tanzania kutanua wigo wa udhamini wake katika michezo mingine mbali na riadha.

"Absa tunaamini katika kitu kinaitwa 'U-africanacity' hii ni kumsaidia mtu ama mteja katika kutimiza malengo yake, kwa kudhamini Kilimanjaro Marathon tunaamini tunawasaidia wanariadha katika kutimiza malengo yao.

"Hii ni mara ya pili kudhamini Kili Marathon, kama Absa Tanzania tunayo furaha kubwa kuwa sehemu ya mafanikio ya Kili Marathon, kama wadau wa mchezo huu wa riadha na pia kwa maendeleo ya michezo nchini," aliongeza Aron.

"Tunahimiza watu washiriki michezo kama hii kwani ni muhimu kwa afya, lakini wajiunge na benki ya Absa Tanzania kwa ajili ya kupata huduma bora za kifedha tukiwa tumeboresha huduma zetu zaidi baada ya kubadilisha jina letu," alisema.

Licha ya kudhamini kituo cha maji na viburudisho kwa wakimbiaji, Absa pia ilipeleka baadhi ya wafanyakazi wake na wateja ili kushiriki mashindano hayo.

# Michezo

Jumanne Machi 3, 2020

Nipashe





Vinicius ampiku Messi El Clasico UKURASA 30

SAMAGOL...




Mshambuliaji wa kimataifa wa Tanzania na Aston Villa, Mbwana Samatta 'Samagoal' akiifungia timu yake bao pekee kwa kichwa wakati wakilala 2-1 kwenye fainali ya Kombe la Ligi England (EFL Cup) huku kipa wa Manchester City, Claudio Bravo akiwa hana la kufanya katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Wembley juzi usiku. **HABARI UK. 28**

# SABABU AZAM FC KUMTIMUA CHECHE

●●● Mrundi amrithi, ni siku mbili kabla ya kuvaana na Simba Taifa, pia msemaji Jaffary Maganga naye...

**Na Saada Akida**

WAKATI zikiwa zimebaki siku mbili kabla ya kuvaana na Simba kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara, uongozi wa Azam FC, umefanya mapinduzi makubwa katika benchi lake la ufundi kwa kumtimua Kocha Msaidizi wa muda mrefu, Iddi Nassor 'Cheche' huku nafasi yake ikichukuliwa na mwalimu wa timu ya Vijana U-20, Vivier Bahati raia wa Burundi.

**Mbali na Cheche kutimuliwa pia wamembadilishia majukumu Ofisa Habari wao, Jaffary Iddi Maganga na sasa anasubiri kupangiwa kazi nyingine ndani ya Azam.**

Azam iliyopo chini ya Kocha Mkuu, Mromania Aristica Cioaba, inatarajiwa kushuka Uwanja wa Taifa kesho, Jumatano kuvaana na Simba, wakati huu ikiwa katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu na pointi zake 48 baada ya mechi 25.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Mtendaji Mkuu wa Azam, Abdulkarim Amin 'Popat' alisema wamemwondoa kabisa Cheche katika timu hiyo huku nafasi yake ikichukuliwa na Mrundi huyo.

Alisema maamuzi hayo yalifanyika jana, baada ya kukubaliana na sababu kubwa ikitokana na kuangalia mwenendo wa timu yao katika michezo mitatu iliyopita.

"Ni kweli Cheche tumemwondoa katika timu, maamuzi hayo ni baada ya uongozi kukutana na kujiridhisha huku mrithi wa nafasi yake tukiamua kumpandisha kocha wa timu ya vijana, Vivier. Pia Jaffary anasubiri kupangiwa majukumu mengine," alisema Popat.

Alisema Jaffary atapangiwa majukumu mengine ndani ya timu hiyo na mrithi wa nafasi yake atatangazwa mapema.

Hata hivyo, Nipashe lilimtafuta Cheche kwa njia ya simu yake ya mkononi likitaka kupata machache kutoka kwake kuhusu hatua hiyo iliyofikiwa na mwajiri wake, lakini simu yake iliita bila majibu.

Na lilipomtafuta Jaffary, yeye alifunguka wazi kwa kueleza: "Ni kweli kuanzai leo (jana), rasmi sitakuwa, Ofisa Habari ila nitakuwa katika majukumu ndani ya Azam, ila kwa sasa sijajua majukumu gani, kikubwa ushirikiano uwapo kati ya huyo ambaye atakuja kwani sote ni ndugu.

"Nitabaki kuwa mwanafamilia wa Azam kwenye majukumu mengine," alisema.

Cheche alianza kuinoa timu hiyo tangu ikiwa Ligi Daraja la Kwanza na ilipoanza kucheza Ligi Kuu msimu wa 2008/2009 hadi kibarua chake kinafikia ukingoni jana.

## Samatta aelezea alivyoitungua Manchester City

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya mshambuliaji wa kimataifa wa Tanzania na nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta kuungana na nyota wengine wanne wa Afrika waliowahi kufunga kwenye mechi ya fainali ya Kombe la Ligi nchini England (EFL Cup), hatimaye amefunguka alivyowatungua wapinzani wao, Manchester City.

Samatta amekuwa mchezaji wa tano Afrika kufunga katika mechi ya fainali ya EFL akiungana na Didier Drogba (aliyefunga manne), Joseph-Desire Job, Obafemi Martins na Yaya Toure.

Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Wembley juzi, Samatta alifunga bao hilo dakika ya 41 kwa kichwa akiunganisha kimyani krosi iliyochongwa kutoka wingi wa kushoto na Anwar El Ghazi wakati wakiwa nyuma kwa mabao 2-0 yaliyofungwa na Sergio Aguero na Rodri dakika ya 20 na 30.

Akizungumzia na mwandishi wetu, Samatta alisema walijua mechi itakuwa ngumu kutokana na ubora wa Manchester City, lakini waliingia dimbani kwa lengo la kupambana kupata matokeo, hata hivyo haikuwa bahati yao.

Kuhusu alivyofunga bao hilo, Samatta alisema: "Wakati mpira unapigwa [na Anwar El Ghazi] ulikuja nadhani nyuma ya Fernandinho [beki wa Man City] na alishakata tamaa kurudi kuuwahi, hivyo nilichokuwa nafikiri ni kuuweka sehemu sahihi."

Kwa ushindi huo unaifanya Manchester City kutwaa kombe hilo kwa mara ya tatu mfululizo, lakini likiwa mara ya nne kwao katika misimu mitano.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042